# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TISA

### Kikao cha Tano – Tarehe 13 Novemba, 2017

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Tukae.

Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

### MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Maswali Waheshimiwa, tunaanza Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Ritta Kabati.

Na. 54

### Kuridhia Mkataba Namba 189 wa *ILO*

**MHE. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Serikali ya Tanzania ilisaini Mkataba Namba 189 wa Shirika la Kazi Duniani *(ILO)* tangu tarehe 16 Juni, 2011 na Rais Mstaafu Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete alishawahi kutamka kuwa, Tanzania haina tatizo na Mkataba huo.

Je, kuna kikwazo gani kinachokwamisha kuridhia Mkataba huo wa *ILO* Namba 189 wa Kazi za Staha kwa Wafanyakazi wa Majumbani wakati Baraza la Wafanyakazi *(LESCO)* limeshapendekeza kuridhia?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Tanzania kama nchi mwanachama wa Shirika la Kazi Duniani ilishiriki kikamilifu katika majadiliano na upitishwaji wa Mkataba ya Kimataifa wa *ILO* wa Wafanyakazi wa Majumbani Namba 189 wa mwaka 2011 ambao unalenga kukuza kazi za staha kwa wafanyakazi wa majumbani. Aidha, hadi kufikia tarehe 30/08/2017 mkataba huo umeridhiwa nan chi 24 kati ya nchi wanachama 187 ambapo nchi za Afrika zilizoridhia mkataba huu ni tatu ambazo ni Afrika Kusini, Mauritius na Guinea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha napenda nielezee kuwa Serikali inathamini mchango wa wafanyakazi wa majumbani katika kujenga uchumi wa nchi. Hii ndio maana Bunge lako Tukufu lilitunga Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Namba 6 ya mwaka 2004, ambayo inazitambua haki za wafanyakazi wa majumbani kama ilivyo kwa wafanyakazi wengine. Vilevile kwa upande wa Zanzibar ipo Sheria ya Ajira, Namba 11 ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuridhia mikataba yote ya kimataifa ikiwemo ya Shirika la Kazi Duniani siku zote Serikali imekuwa ikizingatia maslahi mapana ya nchi na ustawi wa wananchi ikiwemo wafanyakazi kwa ujumla. Endapo Serikali itajiridhisha kuwa mazingira na ustawi wa wafanyakazi kwa sheria zilizopo hakuna ustahimilivu, Serikali itafanya maamuzi stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kuwa kwa kushirikiana na wadau wote vikiwemo vyama vya wafanyakazi na vyama vya waajiri, Serikali itaendelea kuimarisha utekelezaji wa sheria za kazi, ili kulinda haki za wafanyakazi wa majumbani pamoja na kujenga uelewa wa wadau kuhusu matakwa ya mkataba na haki za sheria za wafanyakazi hao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kabati.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo mawili na nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake.

Je, Serikali inasaidiaje kufuatilia wafanyakazi wahamiaji nchi za Uarabuni na kwingineko ambako wanateseka bila kuridhia mkataba huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa tumekuwa tukishuhudia baadhi ya watu ambao wamekuwa wakitafutiwa kazi kupitia hizi wakala za ajira *(Employment Agency),* lakini kumekuwa na malalamiko ya kupunjwa haki zao.

Je, Serikali inachukua hatua gani ili kulinda haki za wafanyakazi ambao wanapata ajira zao kupitia wakala hawa, pamoja na madalali ambao wamekuwa wakiwatafutia wafanyakazi wa majumbani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la kwanza, kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi ya kwamba tuendelee kuangalia mazingira bora ya namna ya ku-*ratify* mkataba huu hasa pale ambapo kama nchi tutakuwa tumejiridhisha kwamba, mazingira ni rafiki na hivyo kuusaini mkataba huo ambao utasaidia sana katika kulinda haki za wafanyakazi wa ndani, lakini vilevile ambao wanatoka nje ya nchi, kwa maana ya Watanzania.

Mhweshimiwa Mwenyekiti, la pili la kuhusu Wakala wa Ajira; kama nilivyokuwa nikijibu katika maswali mengine ambayo yamewahi kuulizwa katika eneo hili, ni kwamba pale katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Kazi, Vijana na Ajira, ipo taasisi ambayo inashughulikia masuala ya ajira kwa maana ya wakala wa ajira ambaye anaitwa *TaESA.* Na rai yetu ilikuwa ni kwamba, wafanyakazi wote wa kitanzania ambao wanakwenda kufanya kazi nje ya nchi ni lazima wapitie *TaESA,* ili tuwatambue tujue na katika nchi ambazo wanakwenda. Tumefanya hivyo kwa sababu wakienda katika njia ambazo si sahihi, sisi kama Wizara si rahisi sana kuweza kufahamu akina nani wako wapi na ndio maana tunawataka kwamba wote wapitie katika ofisi zetu na sisi huwa tunaongea na Balozi husika, ili waweze kushughulikiwa matatizo pale wanapopatwa na matatizo nje ya nchi, ikiwemo ukosefu wa mikataba na haki nyingine.

Na. 55

**Serikali Kusaidia Miradi ya Ujenzi wa Vituo vya Afya**

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE** aliuliza:-

Wananchi wa Jimbo la Msalala kwa kusaidiana na Mbunge wao wameanza ujenzi wa Vituo vya Afya Bugarama, Mega, Ngaya na Isaka na miradi hiyo ipo katika hatua nzuri.

(a) Je, Serikali imejipangaje kusaidia miradi hiyo ya ujenzi wa Vituo vya Afya?

(b) Je, Serikali imejipangaje kukamilisha maboma zaidi ya 28 ya zahanati kwenye vijiji mbalimbli Jimboni Msalala?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa kujibu maswali, naomba uniruhusu nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijalia afya na nguvu kuweza kusimama

mbele ya Bunge lako Tukufu. Pili, naomba nimshukuru Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Uongozi wote wa Bunge kwa malezi na maelekezo ambayo nimepata, bila kusahau Kamati ya Bajeti, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Hawa Ghasia kwa malezi na ushirikiano ambao nimekuwa nikiupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani yake kwangu kwa kuniteua kuhudumu katika nafasi ya Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Uteuzi uliopokelewa kwa mikono miwili kwa wananchi wa Kalambo na Mkoa wa Rukwa kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mbunge wa Msalala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Msalala kwa jitihada anazofanya katika kuwahamasisha wananchi wake kuibua na kuanzisha miradi mingi ya ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya katika Jimbo lake la Msalala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Msalala ina jumla ya vituo vya afya vitatu ambavyo ni Lunguya, Chela pamoja na Bugarama vilivyosajiliwa kwa mujibu wa sheria. Kati ya vituo hivyo, ni vituo viwili ambavyo ni Kituo cha Afya cha Lunguya na Chela ndivyo vinavyotoa huduma za upasuaji wa dharura kwa akina mama wajawazito.

Aidha, ujenzi wa vituo vingine vitatu ambavyo ni Isaka, Ngaya na Mega upo kwenye hatua mbalimbali za ujenzi ambapo lengo la Serikali ni kuwa ifikapo mwaka 2020 vituo hivi viwe vimekamilisha miundombinu muhimu inayohitajika kustahili kuwa vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Msalala ina jumla ya maboma 31. Miongoni mwa maboma hayo, matatu ni vituo vya afya tarajiwa ambavyo ni Isaka, Mega na Ngaya. Aidha, kwa sasa Vituo vya Mega na Ngaya maboma yamepauliwa katika jengo la wagonjwa wa nje *(OPD)* ambapo Boma la Kituo cha Afya cha Isaka lipo kwenye hatua za lenta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali iliweza kukamilisha ujenzi wa zahanati mpya nne kwa gharama ya kiasi cha shilingi milioni 277 na saba ambazo zote zipo katika kata ambazo zilikuwa hazina huduma za afya kabisa. Zahanati hizo zipo katika Vijiji vya Nyaminje, Mbizi, Mwanase na Mwakata ambapo kukamilika kwake kumepunguza adha ya wananchi kutembea umbali mrefu kutafuta huduma ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika mpango wa kitaifa wa kuboresha vituo vya afya kwa ajili ya kutoa huduma za dharura kwa upasuaji wa akina mama, Halmashauri ya Wilaya ya Msalala imepatiwa kiasi cha shilingi milioni 400 kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya kujenga wodi ya wanawake, nyumba ya watumishi, jiko, jengo la kuhifadhia maiti na ukarabati wa miundombinu ya nyumba za watumishi iliyochakaa katika Kituo cha Afya cha Chela. Kituo cha Afya cha Chela tayari kina jengo la upasuaji, wodi ya wazazi, maabara, kichomea taka, shimo la kutupia kondo la nyuma na mfumo wa maji safi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo katika bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali imetenga kiasi cha shilingi 336,742,394 za ruzuku ya maendeleo( *CDG)* kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati katika vijiji saba vya Nyamigege, Gula, Ikinda, Kalole, Jomu, Buchambaga na Ndala, kati ya hayo maboma 31.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maige.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini naomba kwa

sababu ndiyo nazungumza mara ya kwanza baada ya sakata la makinikia kuwa limepata mwelekeo, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa hatua alizochukua. Hatua ambazo zimekuwa ni kilio changu na kilio cha wananchi wa Msalala kwa miaka yote toka Mgodi wa Bulyanhulu ulipokuwepo pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa sababu, wananchi kama ambavyo Mheshimiwa Waziri amesema, wameitikia vizuri sana katika kukabiliana na tatizo la uhaba wa huduma za afya katika Halmashauri na jimbo lao na kwa sababu, changamoto ambayo ipo ni upatikanaji wa fedha Serikalini na kwa bahati nzuri tayari tumeshapata uhakika kwamba, tutalipwa zaidi ya bilioni 700 kutika kwenye makinikia.

Je, Serikali inaweza sasa ikakubaliana na ombi langu kwamba ni vizuri tukapata angalao shilingi bilioni 3.4 ambazo zinatakiwa kuyakamilisha maboma yote haya, ili wananchi hawa wasione nguvu zao zikiharibika kwa sababu mengine yana zaidi ya miaka saba toka yalipoanzishwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa tayari tumeshaletewa shilingi milioni 400 kwa ajili ya uboreshaji wa Kituo cha Afya cha Chela, fedha ambazo pamoja na kwamba ni nyingi, lakini bado hazitoshi kwa sababu, malengo ni makubwa zaidi. Je, Serikali inaweza ikakubaliana na ushauri wangu kwamba, kwa sababu lengo nikupeleka huduma kwa wananchi wengi zaidi na kuna maboma tayari kwenye Vituo vya Afya vya Isaka, Mega na Lunguya ambavyo kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri kwamba viko kwenye hatua mbalimbali. Je, Waziri anaweza akatukubalia ombi letu kwamba fedha hizi tuzigawanye kwenye hivi vituo, ili angalao navyo viweze kufunguliwa halafu uboreshaji utakuwa unaendelea awamu kwa awamu kadri fedha zinavyopatikana kuliko kukaa na kituo kimoja na vingine vikaishia kwenye maboma kama ilivyo sasa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya ombi la uwezekano wa kutizama hii bilioni 3.4 zitumike ili kukamilisha ujenzi wa vituo vya afya pamoja na zahanati; kimsingi hitaji ni kubwa sana, lakini si rahisi kabla ya kufanya hesabu kujua katika mahitaji mengine kiasi gani kiende upande wa afya, kwani vipaumbele ni vingi. Kwa hiyo, ni vizuri, ni wazo jema likachukuliwa likafikiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya shilingi milioni 400 ambazo zimepelekwa, Mheshimiwa Mbunge anaomba kwamba ziruhusiwe zihame kwenda kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi ili tuweze kukamilisha kituo cha afya kwa mujibu wa *standard,* lazima tuwe na uhakika chumba cha upasuaji kipo, wodi ya wazazi kwa maana ya akina mama na watoto, wodi ya akina baba ipo, maabara, nyumba za watumishi za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachowaomba na niziagize halmashauri zote, pale ambapo pesa zimeletwa na Serikali si lazima, eti pesa hiyo iishie hapo, itumike busara kuhakikisha kwamba, kwa utaratibu wa *Force Account* tunatumia pesa ili ikibaki tukiwa na *serving* hakuna dhambi ya kuhakikisha kwamba, pesa hizo zinaweza zikahamia kwenda kumaliza matatizo mengine. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Qambalo atafuatiwa na Mheshimiwa Bonny.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni sera ya Serikali kuwa na hospitali katika ngazi ya Wilaya ili kutoa huduma ya afya kwa wananchi wetu. Wilaya ya Karatu ina umri wa zaidi ya miaka 20 na haina Hospitali ya Wilaya. Ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Karatu? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi naomba niziase Halmashauri zote, ni wajibu wetu wa kuhakikisha kwanza tunaanza kwa kutenga maeneo kwa ajili ya ujenzi wa hospitali za afya, lakini kama hiyo haitoshi, kwa kushirikisha wananchi ni vizuri tukaanza halafu Serikali ikaleta nguvu yake. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbatia.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Kata ya Marangu Magharibi yenye vijiji saba haina zahanati hata moja na hasa vijiji vya Kiraracha na Kitowo wako kwenye hali mbaya sana. Mbunge kwa kushirikiana na wananchi wameweka nguvu zao wanajenga zahanati kwa sasa na imefikia hatua za mwisho.

Nini *commitment* ya Serikali angalau milioni 20 ya dharura, ili kata hii iweze kupata kituo cha afya cha kisasa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika fursa niliyopata ya kutembelea Mkoa wa Kilimanjaro nilijionea. Nilienda Moshi Vijijini nikakutana na wananchi wa Kiafeni, nikakuta kwamba hawakai wakasubiri Serikali ifanye, kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge na yeye anakiri na wana utaratibu mzuri, wanasema siku ya utawala wanakwenda kushiriki wananchi kwa ujumla wake. Nguvu ambayo inatolewa na wananchi ukishirikisha na nguvu ya Serikali nina imani hata hiyo kazi ambayo imefanywa na wananchi anaosema Mheshimiwa Mbatia, hakika kwa kutumia uwezo wao wa ndani, kwa maana ya *commitment* kutoka katika Halmashauri, naomba niitake Halmashauri ihakikishe kwamba wanajibana ili huduma ambayo inahitajika kwa wananchi iweze kufikiwa kwa kumalizia zahanati.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Ghasia.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante na mimi napenda kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Mtwara Vijijini, Kata ya Mambo Pacha Nne na Kata ya Tangazo, Kijiji cha Kilambo, wameanza mchakato wa kujenga vituo vya afya na michango ya wananchi inaenda kwa kasi kubwa.

Je, Serikali itatusaidiaje katika kukamilisha ujenzi wa vituo vya afya katika Kata ya Tangazo, Kijiji cha Kilambo na Kata ya Mango, Pacha Nne?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa sababu, miongoni mwa maeneo ambayo alileta kama *request* katika Jimbo lile la Mtwara ni eneo hilo kwa sababu liko linapakana na Msumbiji.

Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika vipaumbele vyetu vya sasa katika programu tunayoanza nayo kabla ya mwezi wa pili, maeneo yale tumeyapa kipaumbele na tumeyaingiza katika mpango wetu wa bajeti ya muda katika hizi *funds* ambazo tunazipata kutoka kwa wafadhili mbalimbali. *(Makofi)*

Na. 56

**Kuboresha Miundombinu ya Elimu – Mji wa Tarime**

**MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza:-

Kufuatia utoaji wa elimu ya msingi bure, shule za msingi na sekondari ndani ya Halmashauri ya Mji wa Tarime zimekuwa na upungufu mkubwa wa madarasa na madawati hadi kufikia walimu kulazimika kufundishia chini ya mti na wanafunzi walio madarasani wanakaa kwenye

sakafu kwa idadi kubwa kinyume na matakwa ya Sera ya Elimu.

Je, ni nini mpango wa Serikali wa kuhakikisha shule hizo ndani ya Halmashauri ya Mji wa Tarime zinaondokana na changamoto za miundombinu ya kufundishia na kujifunzia ili kutoa elimu bora?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Tarime Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya miundombinu ya elimu nchini ni matokeo ya mwitikio mkubwa wa wananchi katika utekelezaji wa Mpango wa Elimu Bila Malipo ambao umetoa fursa kwa watoto wote wenye umri wa kwenda shule kupata fursa hiyo. Shule 30 za msingi katika Halmashauri ya Mji wa Tarime zinahitaji vyumba vya madarasa 625, vyumba vya madarasa vilivyopo ni 215 na upungufu ni vyumba vya madarasa 410. Aidha, madawati yanayohitajika ni 8,888; madawati yaliyopo ni 6,066 na upungufu ni madawati 2,823.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule nane za sekondari katika Halmashauri ya Mji wa Tarime zinahitaji kuwa na vyumba vya madarasa 133, madarasa yaliyopo ni 104 ma upungufu ni madarasa 29. Aidha, katika shule hizo kuna ziada ya madawati 421 kutokana na mwitikio mzuri wa wananchi na jitihada za Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo kupitia fedha za kuchochea Maendeleo ya Mfuko wa Jimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali imetenga shilingi 119,000,000.00 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa 16, matundu 19 ya vyoo na kuongeza madawati 154 katika shule za msingi. Vilevile Serikali imetenga shilingi 172,500,000 kupitia ruzuku ya

maendeleo na mapato ya ndani kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 22 na matundu ya vyoo 72.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kufuatia majibu ya Mheshimiwa Waziri, ni dhahiri kabisa imeonyesha ni jinsi gani miundombinu ya kujifunzia na kujifunza katika Halmashauri ya Mji wa Tarime hairidhishi na inapelekea matokeo mabaya kwa ufaulu wa wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wananchi wa Tarime wameitikia sana wakishirikiana na wadau mbalimbali ikiwepo mimi mwenyewe Mbunge. Tumejenga madarasa mengi lakini mengi yamekaa bila kuezekwa na kwa kuwa kuna Shule ya Msingi Mtulu ambayo imejengwa na wananchi kwa kujitolea madarasa sita pamoja na ofisi lakini Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji amezuia ile shule wananchi wasiendelee kujenga kwa kile anachokiita kwamba ni mgogoro wa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa sasa kupitia Wizara hii ambayo ipo chini ya Ofisi ya Rais na Rais ana mamlaka ya kubadilisha matumizi ya ardhi, wawatie moyo wananchi wale waliojenga yale madarasa ili sasa waweze kuamuru ile shule iendelezwe ili kupunguza adha ya upungufu wa madarasa katika Halmashauri ya Mji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika Halmashauri ya Mji kuna shule moja ambayo inatumiwa na shule tatu, Shule za Msingi Azimio, Mapinduzi na Sabasaba. Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kipindi hicho akiwa Naibu Waziri alitembelea sisi kama Halmashauri ya Mji tunataka ile shule ijengwe ghorofa ili sasa walimu wasikae kwenye mti kama Ofisi, wanafunzi wasifundishiwe nje chini ya mti, wanafunzi wasirundikane 120 kwenye darasa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini sasa Serikali isiweze kutumia ile asilimia tano ambayo walisema Waziri anaweza akapeleka kwenye matumizi mbalimbali kama

tulivyoona ilivyoenda Chato kwenye uwanja wa ndege. Kwa nini msijenge ghorofa katika shule ile kwenye zile asilimia tano ambazo ni zaidi ya shilingi trilioni 1.7 ili sasa kupunguza adha ya ukosefu wa madarasa katika Mji wa Tarime? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema ukisikia upande mmoja, hakika upande ambao haujasikilizwa utakuwa lazima umekosa. Itakuwa ni vizuri tukajiridhisha sababu ambazo zimesababisha Mkurugenzi azuie uendelezaji wa hiyo shule ili tunapokuja kutoa taarifa iwe ni taarifa ambayo iko *balanced. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie mbunge, miongoni mwa maeneo ambayo nitatembelea ni pamoja na kwenda kutazama uhalisia wa hiki ambacho nakisema kwa sababu lengo ni kuhakikisha kwamba tunapunguza msongamano wa vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaase Waheshimiwa Wabunge na viongozi kwa ujumla, kwamba katika Wilaya ya Tarime, vijana ambao wanamaliza kuanzia darasa la kwanza mpaka darasa la saba wapo 25,000 lakini vijana ambao wanajiandaa kuingia darasa la kwanza wapo 13,000; kwa hiyo, unaweza ukaona sisi kama taifa kuna mambo ambayo lazima tu-*address* namna ya *population growth* inavyokwenda, tukiacha tukatizama hivi tukidhani kwamba Serikali peke yake inaweza hakika haiwezekani. Ni vizuri tukashirikishana pande zote ili kutatua matatizo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya swali lake la pili juu ya ujenzi wa ghorofa, ghorofa jambo zuri na ningependa na mimi nijiridhishe halafu tuone na uwezo wetu maana unapotengeneza chakula lazima ujue na unga upo kiasi gani kwa sisi tunaokula ugali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na juu ya asilimia tano nitaomba niwasiliane na Mheshimiwa Mbunge tuone hiyo asilimia tano na tutayamaliza ili tatizo hili liweze kutatuliwa lakini siamini kwamba asilimia tano inajenga ghorofa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Malecela, atafuatiwa na Mheshimiwa Mollel. Mheshimiwa Waziri subiri kidogo ili uyamalize yote.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kuwapongeza wananchi wa Tanzania, wanajenga sana zahanati, madarasana mifereji.

Je, Serikali haiwezi kuwa na mpango Maalum kwamba wananchi wakijenga kiasi fulani Serikali nayo inakuwa na kiasi fulani inachukua kumalizia kwa sababu watanzania wanajenga mno? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge ni kama amerudia yale ambayo nilikuwa nawaasa Waheshimiwa Wabunge, kwamba hakika kwa kushirikishana wananchi pamoja na Serikali kwa pamoja tunafika na ndiyo maana nikatoa mfano nilivyokuwa nimeenda Moshi Vijijini, Kituo cha Afya ya Kiaseni nimekuta wananchi wamejitoa na Serikali nayo ikapeleka nguvu, hakika tukishirikishana tutaweza kutoka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mollel.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nampongza Mheshimiwa Rais kwa utaratibu wa kutoa elimu bure kwani wanufaika wakubwa ni watoto wenye ulemavu ambao siku za nyuma hawakuweza kupata nafasi hiyo. Hata hivyo, pamoja na jitihada hizo, changamoto ndio bado zipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende katika suala zima la madawati, madawati ni kweli kabisa yametolewa lakini hayakuzingatia uhitaji hasa kwa watoto wenye ulemavu ambao wengine bado wanalazimika kukaa chini kutokana na hali zao haziwawezeshi kukaa katika madawati hayo.

Je, Serikali ina mpango gani ili basi kuzingatia mahitaji ya watoto hao wenye ulemavu ili waweze kufurahia maisha na kusoma vizuri ili waweze kutimiza ndoto za? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nia thabiti ya Serikali kuhakikisha kwamba makundi yote yanazingatiwa katika kutengeneza miundombinu, na ndiyo maana katika hizi siku za karibuni nilivyopata fursa ya kutembelea Mkoa wa Arusha, nikafika Kituo cha Afya Muriet, pale unakuta miundombinu kwa ajili ya walemavu nayo imewekwa. Naomba niwatake Wakurugenzi wote wa Halmashauri, jambo lolote kuhusiana na miundombinu inapotengenezwa sasa hivi lazima tuhakikishe hitaji la watu maalum.

Na. 57

**Mpango wa Uendeshaji wa Shughuli za Serikali kwa Uwazi *(OGP)***

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO** aliuliza:-

Serikali ya Awamu ya Tano imekuwa mstari wa mbele kupambana na ufisadi kiasi cha kumwagiwa sifa duniani; na moja ya silaha kubwa dhidi ya rushwa ni uwazi.

Je, ni kwa nini Serikali ya Awamu ya Tano imeamua kujiondoa kwenye Mpango wa Uendeshaji wa Serikali kwa Uwazi *(OGP)?*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako ninaomba nijibu swali la Mheshimiwa Kabwe Ruyagwa Zitto, Mbunge wa Kigoma Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Kuendesha Shughuli wa Serikali kwa Uwazi *(Open Government Partnership)* ulitokana na wazo la Rais wa Marekani wakati huo Mheshimiwa Barack Obama aliyekuwa na nia na lengo la kuzifanya nchi mbalimbali duniani kuwa wazi katika uendeshaji wa shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huo ulizinduliwa kama Taasisi Isiyo ya Kiserikali *(NGO)* tarehe 20 Septemba, 2011 na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilijiunga tarehe 21 Septemba 2011 baada ya kukidhi vigezo vya kujiunga ambavyo ni pamoja na kuzingatia misingi ya utawala bora. Mpango huo ni wa hiari ambapo nchi inaweza kujiunga baada ya kutimiza masharti na hata kujitoa bila kuwepo na kizuizi chochote.

Hadi sasa nchi wanachama dunia nzima ziko 70 tu na kati ya nchi hizo kumi tu ndizo zinatoka Barani Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Serikali kushiriki utekelezaji wa mpango kwa zaidi ya miaka minne imeamua kujitoa. Tanzania si nchi pekee iliyojiunga na mpango huo na kisha kujitoa, nchi nyingine kama Hungary na Urusi zilijiunga na baadae kujitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Serikali ya Tanzania tangu kupata uhuru imekuwa na mashirikiano ya kikanda na kimataifa katika kutekeleza falsafa ya uwazi na uwajibikaji. Katika kutekeleza falsafa hii , Serikali imejiunga na kutekeleza mipango ya kikanda na kimataifa kama vile Mpango wa Nchi za Kiafrika wa Kujithamini katika Nyanja za Utawala Bora na Mapambano Dhidi ya Rushwa *(APRM),* Shirikisho la Kupambana na Rushwa Afrika Mashariki na Shirikisho la Taasisi za Kuzuia na Kupambana Rushwa kwa Nchi za Jumuiya za Madola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali yetu imesaini mikataba mbalimbali ya mapambano dhidi ya rushwa kama vile *African Union Advisory Board on Anti- Corruption* pamoja na Mkataba wa Umoja wa Mataifa Dhidi ya Rushwa. Ni maoni ya Serikali kuwa shughuli zinazotekelezwa kupitia vyombo hivyo zinatosha kwa nchi kuendelea kujijengea misingi imara ya uendeshaji wa shughuli za Serikali kwa uwazi, kuongeza uwajibikaji na mapambano dhidi ya rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Tanzania kujitoa katika Mpango wa Kimataifa wa Kuendesha Shughuli za Serikali kwa Uwazi *(OGP)* hakuna madhara yoyote. Mipango inayotekelezwa ndani ya nchi kama ilivyoelekezwa hapo juu inajitosheleza kuendeleza na kuimarisha misingi ya uwazi na uwajibikaji na mapambano dhidi ya rushwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Zitto halafu Mheshimiwa Khatib.

**MHE. KABWE Z.R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mifano ambayo Serikali imeitoa ya nchi za Hungary na Russia, nchi hizi ni miongoni mwa nchi ambazo duniani

zinatuhumiwa kwa kuendeshwa bila misingi ya kidemokrasia na kidikteta. Ni aibu sana kwamba nchi yetu inaweza ikaiga nchi ambazo tayari zinaonyesha kabisa kwamba hazifuati misingi ya kidemokrasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukwaa haya ya kimataifa yanatengeneza ushawishi wa nchi kwenye mataifa. Leo hii Mwenyekiti wa *OGP* ni nchi ya Canada, juzi Rais ame...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto uliza swali.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Ndio swali langu la kwanza hilo.

**MWENYEKITI:** Uliza swali *please.*

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Rais amesema kwamba amemwandikia barua Waziri Mkuu wa Canada kuhusiana na suala la *Bombardier*. Je, Serikali haioni kwamba iwapo Tanzania ingekuwa imeendelea kuwa mwananchama wa *OGP* na Canada ndio Mwenyekiti wa *OGP.* Ombi hili la Rais lingeshughulikiwa kwa uzito zaidi kwa sababu ya mahusiano yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Manispaa ya Kigoma Ujiji ni miongoni mwa Miji 15 duniani ambayo inashiriki katika *OGP* kwa uhuru kabisa na haizingatiwi kama nchi iko kwenye *OGP* au la. Serikali inatoa kauli gani kuhusiana na ushiriki si tu wa Manispaa ya Kigoma Ujiji ambayo inafaidika sana kwenye *OGP* lakini pia na Miji mingine ya Tanzania ambayo inataka kuingia kwenye *OGP,* Serikali inatoa kauli gani kuhusu hili? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Zitto ametoa mfano wa nchi zailizojitoa kwamba zinaendeshwa kwa udikteta na nini na nini. Nataka nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba

Tanzania ilipofanya maamuzi haya, imefanya kwa kupima vigezo kwa Tanzania ilivyoona inafaa, hatujamuiga mtu. Sisi ni Taifa huru, linalojitawala, linalofanya maamuzi yake yenyewe bila kushurutishwa na Taifa lolote, liwe kubwa ama dogo duniani. Kwa hiyo, kwamba nchi yetu imeiga mawazo hayo si sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema kwamba Rais wetu amemwandikia Rais wa Canada na kwamba Canada ni Mwenyekiti wa hili, mahusiano yetu pengine jambo lingekuwa hili. Nataka nimweleze ndugu yangu Zitto Kabwe, sisi na Canada ni wanachama wa Jumuiya ya Madola, sisi tuna ubalozi Canada, *with or without OGP* yaani kuwepo ama bila kuwepo *OGP* mawasiliano yetu na Canada haiwezi kuwa tatizo. Na juzi Mheshimiwa Waziri Mkuu walikuwa kule Canada. Kwa hiyo mambo haya ya *Bombardier* na *OGP* wala sijui yanaendaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimefurahi kweli, swali lako la pili nimefurahi sana Ndugu Zitto Kabwe anataka kujua Serikali inatoa kauli gani juu ya ushiriki wa Kigoma Ujiji. Andiko lile la mradi ule linasema nchi ikijitoa, washirika wake wote waliomo ndani ya ile nchi na wao uanachama wao shughuli zao zinakoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inayo taarifa kwamba Manispaa ya Kigoma Ujiji mpaka sasa wanawasiliana na *OGP* na *OGP* wamemuandikia Waziri wa Mambo ya Nje kwamba wana nia ya kuendelea kushirikiana na ninyi. Sasa nataka kupitia Bunge lako Tukufu kuionya Manispaa ya Kigoma Ujiji, nchi inayozingatia utawala bora, haiwezi Serikali Kuu ifanye maamuzi Baraza la Madiwani wakasema sisi hatuta-*comply,* haijatokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nionye Manispaa ya Kigoma waache mara moja, watekeleze maamuzi ya Serikali na wakiendelea kufanya mawasiliano kama wanavyofanya sasa Serikali itachukua hatua kali zaidi. Na ninyi mnajua Serikali kwenye Manispaa sheria kali kuliko zote ni kuvunja Baraza la Madiwani na kuweka Tume ya Manispaa. *(Makofi)*

Nawaomba huko mliko Waheshimiwa Madiwani wa Kigoma na ndugu yangu Zitto Kabwe, msiifikishe Serikali huko. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Khatib.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Dhana ya utawala bora ni pamoja na utoaji wa haki na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sasa katika magereza ya nchi zetu yamejaa mrundikano ya washtakiwa ambao mashtaka yao yameshindwa kuthibitishwa ndani ya mahakama na kuifanya mahakama kuchelewa kutoa haki. Hii ikiwemo ni pamoja na Masheikh wa Uamsho kutoka Zanzibar ambao kwa sasa wana miaka mitano wanasota magerezani na Serikali upande wa mashtaka wameshindwa kuthibitisha makosa yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali inatoa kauli gani kuhusiana na kushindwa kutekeleza utoaji wa haki na kwa wakati kwa watuhumiwa waliopo magerezani? Ahasante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khatib swali hili umelichomekea, halipo katika utaratibu wa swali la msingi. Kwa hiyo, nakuomba *though* unaweza ukalipeleka katika hatua zingine lakini sio katika swali hili. Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Kakoso, kwa niaba ya Mheshimiwa Zainab Katimba. *(Makofi)*

Na. 58

**Vitendea kazi kwa Wavuvi Wadogo wa Ziwa Tanganyika**

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA (K.n.y. MHE. MOSHI S. KAKOSO)** aliuliza:-

Wavuvi wadogo wadogo wa Ziwa Tanganyika wana tatizo la vitendea kazi.

Je, ni lini Serikali itawapatia wavuvi hao vitendea kazi vya kutosha?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako, kwanza naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, kumshukuru Mheshimiwa Spika, wananchi wenzangu wa Mkuranga na kwa namna ya kipekee kabisa kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuniamini kushika nafasi hii ya Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo, naomba sasa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, nijibu swali la Mheshimiwa Moshi Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuhamasisha wadau wa uvuvi, ikiwemo sekta binafsi na jamii ya wavuvi wenyewe kuwekeza katika matumizi ya zana bora za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha mapato yao, baadhi ya mikakati iliyotekelezwa ni kuwawezesha wavuvi wadogo kuanzisha vyama vya ushirika vya msingi kupitia halmashauri husika na pia wawekezaji wakubwa kuwekeza kwenye viwanda vya kutengeneza boti na zana mbalimbali za uvuvi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ziwa Tanganyika, tunacho Kituo chetu cha Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi *(FETA)* pale Kibirizi Kigoma, ambapo tunayo mipango kama Serikali kukiimarisha ili kiweze kuunda boti za kisasa na pia kuendelea kutoa mafunzo na elimu inayohusu sekta ya uvuvi kwa wanafunzi na jamii za wavuvi na wadau wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali inatekeleza Sheria ya *VAT* ya mwaka 2007 ambayo imetoa msamaha wa kodi ya zana za uvuvi na malighafi nyingine ikiwemo injini za

kupachika, nyuzi za kushonea nyavu na vifungashio vyake. Vilevile katika jitihada nyingine za kuwasaidia wavuvi, Serikali hii ya Awamu ya Tano ya Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, katika mwaka 2015/2016 ilitenga jumla ya fedha shilingi milioni mia nne ambapo jumla ya injini za boti 73 zilinunuliwa na katika hizo boti 49 zilishachukuliwa na vikundi vya wavuvi mbalimbali nchini kupitia Halmshauri zao katika mtindo wa ruzuku ambapo Serikali inachangia asilimia 40 na vikundi vya wavuvi vinachangia asilimia 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka hivi sasa tunazo boti takribani 24 ambazo zinawasubiri wavuvi mbalimbali waliopo nchini ikiwa ni pamoja na wavuvi walioko Mpanda na Ziwa Tanganyika lote kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shime kwa Waheshimiwa Wabunge, tuhamasishe vikundi hivi vya wavuvi, mashine hizo bado tunazo, waweze kuja kupitia halmashauri zao kwa kufuata utaratibu kuzipata na kuweza kuimarisha shughuli zao za uvuvi kwa ajili ya kujipatia kipato zaidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Katimba.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali imefanya jitihada gani ili kuhakikisha kwamba wavuvi wanaweza kuzifikia na kunufaika na hizi fursa alizozizungumzia Mheshimiwa Naibu Waziri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali imechukua hatua gani kuhakikisha inasimamia kwa ukamilifu sekta hii ya uvuvi ili kuhakikisha inaepusha uvuvi haramu ambao utaleta uharibifu kwa mazingira?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza ni jitihada gani ambazo Serikali imeshakufanya. Kama nilivyojibu katika swali la msingi ya kwamba, la kwanza, tumeendelea kuhamasisha wavuvi kujiunga katika vikundi mbalimbali ili waweze kutumia fursa zinazojitokeza, kama vile fursa niliyoitaja ya ruzuku ambapo katika mwaka huu wa 2017/2018 tumeshatenga shilingi milioni 100 ili kuweza kuendelea kuwasaidia wavuvi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Sheria ile ya Fedha ya mwaka 2007 tunaendelea kuisimamia kuhakikisha ya kwamba zana za uvuvi zinaendelea kupatikana kwa bei nafuu. Pia tunalo dirisha katika Benki yetu ya Rasilimali ambalo linahusu wakulima, wavuvi na wafugaji ili waweze kupata mikopo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni juu ya hatua gani Serikali inachukua kukomesha uvuvi haramu ili kulinda rasilimali zetu. La kwanza kabisa Serikali inaendelea kutoa elimu kwa wavuvi na jamii za wavuvi ili kulinda rasilimali zetu kwa ajili yetu na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali imejishirikisha katika kufanya doria mbalimbali ambazo zimeleta matunda chanya ya kuhakikisha kwamba uvuvi haramu unapigwa vita ikiwa ni pamoja na uvuvi wa matumizi ya mabomu na uvuvi wa nyavu zisizoruhusiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho katika kupambana na uvuvi haramu, Serikali inakusudia kuleta maboresho ya Sheria yetu ya Uvuvi Namba 22 ya mwaka 2003 ili kuipa meno zaidi kuhakikisha tunaendelea kulinda rasilimali za nchi yetu. Nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Kemi halafu Mheshimiwa Dau.

**MHE. KEMILEMBE J. LWOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tatizo kubwa sana la wavuvi, hasa wa Kanda ya Ziwa na wa Ziwa Victoria kuchomewa nyavu zao na kusababishiwa hasara kubwa sana na Serikali. Ni lini sasa Serikali itatoa maamuzi ya kukataza nyavu hizi kutengenezwa kwenye viwanda ili wananchi wetu wasiendelee kupata hasara ya kuchomewa nyavu zao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali itaendelea kutoa elimu ya kuhakikisha kwamba wananchi wanapata kujua nyavu gani ambazo haziruhusiwi na nyavu gani ambazo zinaruhusiwa.

Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kupitia sheria zetu za uvuvi tutaendelea kushirikiana na wavuvi wetu na jamii yote ya wavuvi ili kuhakikisha kwamba zile nyavu zisizoruhusiwa hatutaziacha, lakini nyavu zinazoruhusiwa ambazo zipo katika vipimo vya kisheria zitaendelea kutumika. Vilevile kuwahamasisha wawekezaji zaidi waweze kutengeneza nyavu zinazoruhusiwa kwa ajili ya kulinda mazingira yetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu ndani ya Bunge. Mheshimiwa Dau atafuatiwa na Mheshimiwa Lupembe.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya wavuvi wadogo katika Ziwa Tanganyika yanafanana sana na matatizo ya wavuvi wadogo katika Kisiwa cha Mafia. Taasisi ya Hifadhi ya Bahari Mafia imekuwa ikiwanyanyasa na kuwabambikia kesi wavuvi wadogo wa Mafia na kuwanyang'anya nyavu zao. Je, Mheshimiwa Waziri utakuwa tayari kufanya ziara Mafia na kutukutanisha sote ili kupata ufumbuzi wa tatizo hili?

**MWENYEKITI:** Jibu lake, anataka kujua tu kama uko tayari kwenda ziara.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie kaka yangu, Mheshimiwa Mbaraka Dau, Mbunge jirani wa Mafia ya kwamba nipo tayari kwenda nyumbani Mafia kwa ajili ya…

**MWENYEKITI:** Inatosha Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Lupembe, baadaye Mheshimiwa Bilago.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Ziwa Tanganyika, Kalema, Ikola pamoja na Kapalamsenga, vijana wale wako duni sana kwa ajili ya uvuvi wa lile Ziwa Tanganyika. Je, Waziri yuko tayari kwenda na mimi ili akaone hali halisi ya vijana wale?

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Waziru, uanze na safari ya kwenda Ziwa Tanganyika kwanza.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anna Lupembe kwamba niko tayari kwenda Ziwa Tanganyika kuonana na wavuvi wa ziwa hilo wakati wowote baada ya kumaliza shughuli za Bunge hapa.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Bilago.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaruhusu nyavu zisizotakiwa zinaingia nchini na Serikali hiyo hiyo inachukua kodi kwa waingizaji wa nyavu ambazo hazifai, nyavu zikishauzwa anayepata hasara ni mwananchi aliyenunua nyavu zile ambazo kumbe Serikali inafahamu hazihitajiki na

ilichukua kodi. Sasa kama Serikali inaweza ikazuia madawa ya kulevya yasiingie nchini inashindwaje kuzuia nyavu zisizofaa kwa wavuvi zisiingie nchini na hivyo kuwatia hasara baada ya kuwa wameshazinunua? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu, nyavu nyingi zinaingia kwa njia ya magendo.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi jambo hili la nyavu lina mkinzano. Zipo nyavu ambazo zinaruhusiwa katika bahari lakini *size* hiyo hiyo ya nyavu inaweza isiruhusiwe katika maziwa yetu; wapo wafanyabiasara ambao wanaweza kuagiza nyavu kwa nia ya kusema wanazipeleka katika bahari lakini wakishafika na kuzitoa bandarini wakazipeleka kwenye maziwa pasiporuhusiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hila hii wataalam wetu na sisi kama Wizara tunaendelea kukabiliana nayo na hata sasa tunazo kesi mahakamani za jambo la namna hii. Sisi tunaomba uungwaji mkono wa kuhakikisha kwamba mkanganyiko huu tunautatua ilimradi tuhakikishe kwamba wafanyabiashara wetu, wazalishaji wetu wa nyavu, wote wanakwenda kwa matakwa ya sheria, kanuni na taratibu zetu zinazo-*guide* shughuli nzima hii ya uvuvi. Uvuvi ni maisha yetu, lakini ni lazima tuhakikishe tunalinda mazingira kwa ajili ya vizazi vya leo na vya kesho. Nashukuru sana.

Na. 59

**Hitaji la Umeme wa Uhakika – Mkoa wa Mtwara**

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA** aliuliza:-

Katika Mkoa wa Mtwara kuna tatizo kubwa la kukatika kwa umeme mara kwa mara jambo ambalo linaathiri wananchi ikiwemo wafanyabiashara ambao wanategemea sana umeme na hivyo kusababisha wakati mwingine biashara hizo kuharibika na kuwasababishia hasara wananchi hao.

Je, ni lini Serikali itawahakikishia wananchi wa Mtwara kupata umeme wa uhakika?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shamsia Aziz Mtamba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa wananchi katika maeneo mbalimbali nchini wanapata umeme wa uhakika ili kuboresha maisha yao. Serikali kupitia *TANESCO* imeweka jitihada kubwa kuhakikisha kuwa umeme wa kutosha katika Mikoa ya Mtwara na Lindi unapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kufanya ukarabati mkubwa wa mitambo yote tisa iliyopo Mtwara yenye uwezo wa kuzalisha megawati 18. Ukarabati huu ulianza mwishoni mwa mwezo Oktoba, 2017 na utakamilika mapema mwezi Desemba, 2017. Gharama ya matengenezo kwa mitambo yote ni shilingi 4,800,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ukarabati huo, Serikali imeagiza mitambo miwili mipya kutoka Kampuni ya *Caterpillar* yenye uwezo wa kuzalisha jumla ya megawati nne kwa gharama ya shilingi 8,300,000,000. Ufungaji wa mitambo hiyo unatarajiwa kuanza mwezi Januari, 2018 na kukamilika mwezi Aprili, 2018. Mitambo hiyo itaongeza uwezo wa mashine zilizopo kufikia megawati 21.75.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *TANESCO* imeanza utekelezaji wa mradi wa kuzalisha umeme wa megawati 300 kwa kutumia gesi asilia Mkoani Mtwara. Kazi inayoendelea kwa sasa ni kukamilisha upembuzi yakinifu kupitia Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japani *(JICA).* Mradi huo unategemewa kuanza mwezi Aprili, 2018 na kukamilika mwezi Desemba, 2019. Mradi huu utakapokamilika utatoa suluhisho la kudumu la upatikanaji

wa umeme wa kutosha katika Mikoa ya kusini ikiwa ni pamoja na Lindi na Mtwara.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shamsia.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza, pamoja na kupita bomba la gesi katika maeneo mengi ya Mtwara na Lindi, bado vijiji na mitaa mingi haina mtandao wa umeme. Je, ni lini *REA III* itamaliza tatizo hili kwa mikoa ya kusini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, mkandarasi aliyepewa kusambaza mtandao wa umeme Mtwara yupo *slow* sana. Je, Serikali inachukua uamuzi gani kwa mkandarasi huyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge ameuliza; ni lini *REA III* itamaliza tatizo la kusambaza umeme katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Mtwara. Nataka nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kuwa Mkandarasi wa Mkoa wa Mtwara ni *JV Radi Service Limited* na ameshalipwa asilimia kumi na yupo Mkoani Mtwara akiendelea na kazi ya upimaji wa njia ya umeme, na kwa kuwa Wizara tumetoa maelekezo kwamba vifaa vyote vya mradi huu *REA III* vipatikane ndani ya nchi, wakandarasi wanachoendelea nacho sasa ni namna ya kutafuta vifaa vyote na kuagiza ndani ya nchi, na nimhakikishie kazi hii itafanyika kwa mujibu wa ratiba iliyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili anaulizia hatua gani zitachukuliwa dhidi ya mkandarasi huyu. Naomba nimwambie ratiba ya *REA* iko awamu mbili, awamu ya

kwanza ni 2017 hii Julai mpaka 2019, kwa hiyo mkandarasi huyu yupo ndani ya muda. Na kwa kuwa amelipwa asilimia 10 na ameanza kazi, nimthibitishie tu zoezi la upelekaji umeme katika Mtwara kwa mkandarasi huyu *JV Radi Service* itakamilika kwa wakati.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Nape, ajiandae Mheshimiwa Aisharose.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali katika kutatua tatizo la umeme kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara, baada ya mateso makubwa tuliyoyapata katika kipindi hiki cha miezi miwili/mitatu cha kukosa umeme kwa zaidi ya siku nne. Serikali inaambatanishaje juhudi hizo na ukarabati wa miundombinu hasa nguzo, kwenye yale maeneo ambayo nguzo zake ni mbovu. Kwa hiyo, hata wakikamilisha uzalishaji bado usambazaji wa umeme kwenye haya maeneo ambayo nguzo zake ni mbovu bado itakwama.

Sasa Serikali imejipangaje kuambatanisha juhudi hizo mnazoendelea nazo na ukarabati wa nguzo kwenye yale maeneo ambayo nguzo zimechoka?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini niwape pole sana Waheshimiwa Wabunge wa Mikoa ya Mtwara na Lindi kwa kipindi ambacho Mheshimiwa Nape amezungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli zipo juhudi za makusudi ambazo sasa tunachukua kama Serikali, tuliporekebisha umeme katika Mkoa wa Mtwara tarehe 16 mwezi uliopita tuliacha *feeder* mbili ambazo matengenezo yake yanaendelea. Wananchi wa Mkoa wa Lindi kwa sasa

wanapata umeme kutoka kwenye *sub station* ya Maumbika. Sasa *sub station* ya Maumbika marekebisho ya *engine* yake yanakamilika kesho. Kwa hiyo wananchi wa Mtwara, Lindi na maeneo mengine yategemee kupata umeme kuanzia kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la nguzo kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amezungumza, tumeagiza nguzo mpya kutoka hapa nchini, tumeacha sasa kuleta nguzo kutoka nje ambazo zilikuwa zinakaa kwa muda mrefu mipakani. Nguzo zitakuwa mpya, kwa hiyo, niwahakikishie wananchi watapata nguzo na ukarabati utaendelea vizuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Aisharose, ajiandae Mheshimiwa Ngombale.

**MHE. AISHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Tatizo lililopo Mtwara halina tofauti na tatizo lililopo katika Jimbo la Singida Kaskazini. Vijiji vingi vya Jimbo la Singida Kaskazini ambavyo vilikuwa katika Mpango wa *REA II* mpaka sasa havijapatiwa umeme. Vijiji hivyo ni Mrama, Madasenga, Mipilo, Meria, Mitula na Msange. Kwa kuwa sasa tunaelekea kwenye Tanzania ya Viwanda; je, ni lini sasa Serikali itavipatia vijiji hivyo umeme ukizugatia kwamba tupo katika Mpango wa *REA III?* Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muhusika.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mkoa wa Singida mkandarasi ambaye alipewa kazi alikuwa na jukumu la kukamilisha masuala ya mikataba. Taratibu za mikataba amekamilisha juzi, siku ya Ijumaa, na hivyo ataanza kuingia *site* kuanzia Ijumaa wiki hii, kwa hiyo wananchi wa Singida na maeneo mengine watapata mkandarasi huyo.

Lakini cha pili Singida tunawapatia mkandarasi aliyeshindwa kukamilisha kazi katika *REA II,* Kampuni ya SPENCON iliondolewa kwa hiyo, tunawapa mkandarasi

mwingine. Kwa hiyo, Mkoa wa Singida utapata wakandarasi wawili pamoja na mkandarasi wa *REA III.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ngombale.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Kwa kuwa chanzo cha umeme pale Somanga Fungu kinashindwa kufanya kazi vizuri na kupelekea matatizo makubwa ya umeme kwa Wilaya ya Kilwa na Rufiji kwa sababu ya mitambo ile kuchelewa kufanyiwa ukarabati na kwa kuwa sasa tatizo hilo linaendea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itatuunganisha watu wa Kusini na Gridi ya Taifa kwasababu sasa umeme imeshafika pale Kilwa? *(Makofi).*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge Ngombale kwamba mitambo ya Somanga Fungu inatarajia kufanyiwa ukarabati hivi karibuni na kampuni ya *RENCO* ya Italy. Na Serikali kupitia *TANESCO* wameshasaini mkataba na ukarabati huo utakamilika Desemba, 2018 ambapo mitambo itakuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 7.5 na matumizi ya Kilwa ni megawati tatu. Kwa hiyo naomba nimtaharifu kwamba hilo linafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili ameuliza ni lini…

**MWENYEKITI:** Mjibu swali moja tu, swali moja tu hili lingine yeye kachomekea, si swali la msingi, linatosha Mheshimiwa Waziri, ahsante kwa majibu mazuri.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Mheshimiwa Godifrey Mgimwa kwa niaba ya Mheshimiwa Malongo.

Na. 60

**Tatizo la Umeme Katika Baadhi ya Vijiji - Kalenga**

**MHE. EDWARD F. MWALONGO (K.n.y. MHE. GODFREY W. MGIMWA)** aliuliza:-

Tatizo la umeme bado ni kubwa licha ya jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali.

Je, ni lini Serikali itatatua tatizo hili na hatimaye kuvipatia umeme Vijiji vya Kipera, Lupalama, Itagutwa na Lyamgungwe?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa, Mbunge wa Kalenga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* inatarajia kuvipatia umeme Vijiji vya Kipela, Lupalama, Itagutwa, Ikongwe na Lyamgungwe katika Awamu ya Tatu ya uetekelezaji wa Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini *(REA III)* inayoendelea kwa sasa. Aidha, kwa Mkoa wa Iringa miradi hiyo inatekelezwa na mkandarasi Kampuni ya *Sengerema Engineering Group* na tayari yupo katika eneo *(site)* akifanya upimaji wa awali kwenye vijiji tajwa pamoja na vijiji vingine 145 vya Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kupeleka umeme katika vijiji hivyo tajwa inajumuisha ujenzi wa njia za umeme wa msongo wa kilovolti 33 na 11 zenye urefu wa kilometa 22; msongo wa kilovolti 0.4 yenye urefu wa kilometa 18; na uwekaji wa transfoma tisa pamoja na kuwaunganisha umeme wateja 215. Gharama ya kutekeleza miradi hiyo ni jumla ya shilingi bilioni 2.3.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwalongo.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Pamoja na majibu hayo naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Kalenga pamoja na kazi nzuri inayofanyika wakandarasi hawa wanapeleka umeme lakini hawafikishi kwenye Taasisi za umma kama zahanati shule.

Je, Serikali inatoa msisitizo gani na kuwafariji hawa wanchi wa Kalenga juu ya utekelezaji wa mradi huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; katika Jimbo ya Njombe Mjijini yupo mkandarasi anayetekeleza mradi wa Makambako - Songea. Mradi hule ulikuwa-*designed* miaka mingi sana, matokeo yake ni kwamba mitaa imepanuka na maeneo yamepanuka na yule anatumia mchoro wa miaka mingi iliyopita.

Je, Serikali inatusaidiaje sasa ili kusudi mradi ule wa Makambako - Songea inaopisha umeme katika vijiji, umeme ule uweze kufika vitongoji vyote na taasisi za umma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza lilijielekeza kwenye taasisi za umma ambazo hazifikiwi na Mradi wa *REA* unaoendelea. Ningependa kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba kwenye Mkoa wa Iringa kuna mradi wa *densification* unaotekelezwa kwa ajili ya maeneo ambayo yalirukwa kwenye Awamu wa Pili. Inaangalia maeneo ya umma, taasisi mbalimbali, iwe hospitali, ziwe shule za msingi na kadhalika. Kwa hiyo nimuhakikishie kwamba mradi wa *densification* unafanya hiyo kazi katika Mkoa wa Iringa na mkandarasi anaendela na kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, aliulizia juu ya mradi wa Makambako - Songea. Naomba nimthibitishie

Mheshimiwa Mbunge kwamba kwamba katika mradi huu wa Makambako Songea ujenzi wa laini wa msongo wa KV 220 kwanza kazi inaendela vizuri lakini pia swali lake alikuwa anauliza je maeneo ambayo vijiji vinavyopitiwa na msongo huo usambazaji wa umeme ukoje. Nimthibitishe Mheshimiwa Mbunge kwamba kazi ya kusambaza umeme itaendelae na maeneo ambayo yataachwa *REA III* itaendelea kuya-*cover* kwasababu mpango wa Serikali ya Awamu Tano ni kuhakikisha kwamba vijiji vyote vinapata umeme ifikapo 2020/2021. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mwamoto, atafuatiwa na Mheshimiwa Mkundi.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mradi wa *REA III* tayari umeanza na vijiji vingi vimepimwa, lakini sasa hivi kuna baadhi ya vijiji ambavyo vilisahaulika na baadaye tukaleta kuomba tena viingizwe.

Sasa Serikali inatuambiaje hasa katika Wilaya ya Kilolo, je, vijiji ambavyo vilisahaulika vitaongezwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kama nilivyosema, mradi wa *REA* una awamu mbili, na lengo lake ni kuvifikia vijiji 7,823. Awamu ya kwanza vijiji 3,559 na awamu ya pili vijiji 4,313. Nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba vijiji vyote vitafikiwa umeme ifikapo mwaka 2020/2021. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mkundi.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, maeneo ya Kakelege na eneo la uwanja wa ndege Kata ya Nkilizia yapo katikati ya mji wa Nansio. Lakini maeneo haya yamerukwa na huduma ya umeme, jambo

linalofanya wananchi wa maeneo haya waone kama wametengwa. na Mheshimiwa Waziri nimekuwa namuwasilishia tatizo hili mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali langu nataka kujua Serikali imefikia hatua ipi kuhakikisha kwamba maeneo haya yaliyo katikati ya mji wa Nansio yote yanapata huduma za umeme?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika maelezo yangu ya awali Serikali inatekeleza mradi pia wa *densification* ambao sasa hivi Awamu ya Kwanza na ni kwa Mikoa sita. Baada ya kukamilika kwa mikoa hiyo Serikali itaendelea pamoja na wafadhili wa Norway kutekeleza awamu ya pili. Nia ya mradi huu ni kusambaza umeme katika maeneo kaya, vitongoji na taasisi za umma zilizorukwa. Kwa hiyo, nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba Awamu ya Pili ya mradi huu itafikiwa katika maeneo ambayo ameyataja.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Kitandula.

**MHE. DUNSTAN. L. KITANDULA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Serikali ilihaidi kwamba Kata ya Mwakijembe ambayo iko mpakani na Kenya vijiji vyake vilisahaulika lakini kuna umuhimu wa kiulinzi vijiji vile kupata umeme. Serikali ilihaidi kwamba kabla mkandarasi hajaondoka kufanya *survey* wataagizwa ili jambo hilo lifanyike. Je, ni lini jambo hili litakamilika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kata anayoitaja Mheshimiwa Mbunge ya Mwakijembe ni kata ambayo iko mpakani, laikini kama alivyosema aliliwasilisha ombi lake hilo. Kwa kutambua umuhimu wa maeneo ambayo yako mpakani suala lake linashughulikiwa na mkandarasi wa Mkoa wa Tanga katika

maeneo ambao Wilaya ya Mkinga na Wilaya zinginezo ni *Delimiki Electric Company Limited* yupo *site* anaendelea na hiyo kazi. Kwa hiyo nimtoe wasi wasi Mheshimiwa Mbunge, kwamba Serikali inashughulikia. Na kwa kuwa nia yetu ni kusambaza umeme katika maeneo yetu hilo jambo litafanikiwa, ahsante.

Na. 61

**Sheria ya Sekta Binafsi ya Ulinzi Nchini**

**MHE. ALMAS A. MAIGE** aliuliza:-

Sekta binafsi ya ulinzi ilianzishwa mwaka 1980 ikiwa na kampuni mbili tu na ikiwa haina miongozo yoyote.

(a) Kwa kuwa sasa sekta hii ina kampuni zaidi ya 850 nchini kote, je, Serikali italeta Sheria ya Sekta Binafsi ya Ulinzi ili pia kuanzisha mamlaka ya sekta binafsi ya ulinzi?

(b) Je, Ofisi ya Inspekta Jenerali wa Polisi *(IGP)* ina mpango gani wa kushirikiana na Chama cha Sekta Binafsi ya Ulinzi ili kuimarisha ulinzi wa raia na mali zao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Almas Athumani Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba sekta ya ulinzi binafsi imekuwa sana hapa nchini na kwamba Serikali inatambua umuhimu wa sekta hii na ilishaanza maandalizi ya kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Makampuni Binafsi ya Ulinzi. Katika kufanikisha jambo hili Wizara ya Mambo ya Mambo ya Ndani ya Nchi iliandaa walaka kupeleka Baraza la Mawaziri kwa hatua za awali. Ili kukamilisha hatua hii

yanahitajika maoni ya wadau kutoka pande mbili za Muungano. Serikali imeweka utaratibu wa kupata maoni kutoka katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na mara yatakapopokelewa waraka huu utawasilishwa mapema iwezekanavyo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Inspekta Jenerali wa Polisi imekuwa ikishikiana na sekta binafsi ya ulinzi katika nyanja mbalimbali. Kwa mujibu wa Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi Namba 322 Rejeo la mwaka 2002. Jeshi la polisi limekuwa likitoa mafunzo kwa makampuni binafsi ya ulinzi, kufanya ukaguzi kuchukua alama za vidole kwa watumishi, kutoa vitambulisho na kutoa ushauri kwa makampuni hayo ili kuboresha na kuhakikisha huduma ya ulinzi inatolewa katika viwango vinavyostahili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maige.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kuniruhusu niulize maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, mimi nasikitika sana Serikali haisemi kwamba mimi ndiye niliyeleta Muswada Binafsi wa Sekta ya Ulinzi Binafsi *(Private Security Industry Bill)* wa mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa je, Serikali iko tayari kunilipia kunirudishia gharama hata nusu ya ghalama niliyoitumia katika utafiti huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, na la pili, kwa kuwa mchakato wa kuipata sheria hii ya sekta ya ulinzi binafsi unakuwa mrefu sana, je, Serikali sasa iko tayari kutunga *GN* ambayo itatumika wakati huu wa mpito kwa sababu makampuni haya yalianzishwa bila *GN* wala sheria yoyote?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na swali lake la kwanza,

awali napenda kuchukua furusa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Maige kwa mchango mkubwa sana ambao amekuwa akiutoa katika sekta binafsi ya ulunzi na hivyo kama Serikali tunathamini sana mchango wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Mheshimiwa Maige kuwasilisha muswada wake binafsi hapa Bungeni majibu ya Serikali yalikuwa kwamba Serikali itafanya kazi hiyo, kwa maana ya kuleta muswada huo ili ujadiliwe mbele ya Bunge na sheria hii iweze kutungwa.

Kwa hiyo, nimuombe tu Mheshimiwa Maige kwamba ile kazi kubwa aliyoifanya aichukulie kama ni sehemu ya mchango wake kwa Taifa hili; na yeye kama akiwa mzalendo namba moja basi aone kama ni mchango wake katika kusaidia Serikali katika kukamilisha utungwaji wa sheria hii. Ninafahamu sana kwamba Mheshimiwa huyu ni mzalendo, itakuwa ni sehemu ya mchango wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, la juu ya *GN,* katika majibu yangu ya msingi nimesma taratibu za utungwaji wa sheria zinaelekea kukamilika na hivyo namshauri Mheshimiwa Mbunge kwa sababu tumeshapitia kote huko, hatua hii ilibaki atupe nafasi Serikali kuwasilishwa muswada huu ili sheria hii itungwe na baadaye zitakuja hizo *GN* zingine kwa ajili ya ku-*regulate* maswala ya ulinzi katika sekta binafsi.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Ruth halafu Mheshimiwa Ester Mahawe.

**MHE. RUTH. H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Serikali ndiye msimamizi mkubwa wa usalama wa raia na mali zao, ningepa kufahamu ni kwa jinsi gani Serikali inasimamia kwa uhakika hizi sekta binafsi za ulinzi ili kuhakikisha wale wote walioajiriwa hawana historia ya uhalifu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia taasisi zake mbalimbali imekuwa ikihakikisha kwamba kuanzia katika eneo la usajili wa makampuni haya ambayo pamoja na kwamba utaratibu wa usajili wake ni kupitia *BRELA,* lakini bado Jeshi la Polisi nalo lina nafasi ya kuweza kupitia na kuyatathimini maombi ambayo yanapekwa ili kujihakikishia. Kwa sababu kazi ambayo inakwenda kufanywa hapa na sekta ya ulinzi binafsi ni kazi ambayo vilevile ni ya kulisaidia Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu kwa mujibu wa viwango vya Umoja wa Mataifa askari mmoja anapaswa kulinda watu na 450, lakini sisi kwetu askari mmoja analinda kuanzia watu 1,150 mpaka 1,300. Kwa hiyo, ndiyo maaan kama Serikali tunatoa kipaumbele na ndiyo maana katika shughuli mbalimbali za sekta ya ulinzi binfsi tunahakikisha kwamba tunashirikiana nao katika kutoa elimu, lakini vilevile na kuzisimamia kuona kwamba zinayanya kazi ile iliyokusudiwa ili hatimaye isije ikaleta madhara makubwa kwa sababu na yenyewe pia ni sehemu ya ulinzi katika nchi yetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mahawe.

**MHE. ESTER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Swali langu lilikuwa kuhusu ukosefu wa nyumba za polisi katika Mkoa wa Manyara ikiwemo Ofisi ya *RPC.* Ni lini sasa Serikali itaona kwamba kuna umuhimu wa Jeshi la Polisi kupatiwa nyumba ili waweze kufanya kazi yao kwa ufanisi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ni swali lingine lakini lijibu kwa sababu wewe ni mtaalum na unafanya kazi vizuri. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunatambua kwamba tunayo changamoto kubwa sana ya ukosefu wa nyumba za

askari wetu, lakini katika mipango ya Wizara tumejiwekea utaratibu kwamba pindi pale bajeti itakaporuhusu tutahakikisha kwamba tunaifikia Mikoa yote ili kuwaondolea adha ya ukosefu wa nyumba watumishi wa Serikali hasa wa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuondolee hofu Mheshimiwa Mbunge bajeti ikikaa vizuri basi tutafikia katika maeneo yote katika kuondoa hadha hii.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Bhagwanji.

**MHE. BHAGWANJI MAGANLAL MEISURIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kinipa nasafi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazipongeza Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Muungano kwa sababu katika Jimbo langu wamejenga kituo cha polisi Chwaka na Jozani. Lakini mimi naomba Serikali, wameniomba nizungumze Serikali ya Muungano pamoja na Zanzibar wapatiwe gari za doria, Chwaka na Jozani.

La kwanza kwa kuboresha wananchi wangu wapate hitaji lao, lakini lingine mimi mwenyewe binafsi nimetoa gari mbili hospitali za Chwaka na Kongoroni. Lakini hii gari ya polisi lazima tuhudumie tupate na mimi nimesaidia Jozani polisi walikuwa wanahitaji *computer* na nimewasaidia, lakini hii gari mnipatie zote mbili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Bhagwanji hakuuliza swali, ilikuwa ni ombi la gari la doria na mimi tu kwa niaba ya Serikali tumepokea ombi lake na tutalifanyia kazi pindi pale nafasi itakaporuhusu basi tutaona namna ya kuweza kufanya.

Na. 62

## Kodi za Zimamoto kwa Wananchi Wanaopimiwa Ardhi

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI** aliuliza:-

Jitihada za wananchi kukaa katika maeneo yaliyopimwa zinakabiliwa na changamoto ya malipo ya shilingi 150,000 ambayo ni kodi ya zimamoto pale wanapotaka kupimiwa ardhi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kufuta kodi hiyo ili kupunguza ongezeko la makazi holela?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mbunge wa Mpanda Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linafanya ukaguzi kwa mujibu wa Sheria Namba 14 Sura Na. 427 *(Fire and Rescue Force Act)* ya mwaka 2007 kupitaia kanuni zake za ukaguzi na vyeti ya mwaka 2008 ikisomwa pamoja na ya mwaka 2014 *[Fire and Rescue Force; (Safety Inspections, Certificate and Fire Levy) Regulalations]* za mwaka 2008 na mwaka 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Ukaguzi za mwaka 2014 *(Fire Levy Category No. 58)* kanuni inaelekeza kutozwa tozo ya usomaji na ushauri wa michoro au ramani za majengo. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya Majengo ya mwaka 2005 *[The Fire and Rescue Force, (Fire Precautions in Buildings) Regulations], 2015* Na. 248 Jeshi la zima moto na Ukoaji limekuwa likishiriana na Halmashauri za Miji, Manispaa na Majiji kukagua ramani za ujenzi ili kuhakikisha kuwa nyumba zinajengwa kwa kuzingatia

tahadhari na kinga dhidi ya moto na majanga mengine. Kupitia ushauri huu Jeshi la zimamoto na uokoaji hutoza tozo ambapo kiasi cha tozo huzingatia aina ya ramani iliyowasilishwa na kukaguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia umuhimu wa ujenzi unaozingatia tahadhari na kinga dhidi moto, Serikali haikusudii kufuta tozo hii kwa sasa. Aidha, Serikali kupitia Jeshi la Zimamoto na uokoaji inawaasa Wananchi kwa kujenga nyumba zao kwa kufuata Sheria na Kanuni zinazosimamia mipango miji ili kuwa na miji salama hivyo kupunguza athari zitokanazo na moto na majanga mbalimbali na kuwezesha utoaji wa huduma za kijamii kwa urahisi zaidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kapufi.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa kibali cha Halmashauri kinatozwa shilingi 16,000, kiwango ambacho ni nafuu, je, zimamoto kutoza 150,000 haioni kwamba kiwango hicho ni kikubwa na hivyo inapelekea wananchi wengi kujenga bila kuwa na kibali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, mchanganuo wa tozo kwa mjenzi wa nyumba ya kawaida anatozwa hiyo hiyo shilingi 150,000 sawa na mjenzi wa ghorofa, hii imekaaje?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la kwanza ametaka kujua tozo ya shilingi 150,000 kwamba ni kubwa na hivyo inawafanya wananchi washindwe kupata kibali hiki na hivyo kujenga majengo holela. Tozo hizi ni kwa mujibu wa Kanuni na Sheria ambazo tumejiwekea, ukiacha ile Halmashauri ambayo ni shilingi 16,000 anayosema yeye, lakini

kwa mujibu wa taratibu ambazo tumejiwekea kwa maana ya Sheria yetu hasa katika Kanuni ile ya *[The Fire and Rescue Force, (Fire Precautions in Buildings) Regulations], 2015* Na. 248 imezungumza kiwango ambacho kinapaswa kutozwa ukianzia katika Majiji, Halmashauri, Wilaya lakini vile vile na katika vijiji. Kwa hiyo kiasi kilichowekwa hapa cha shilingi 150,000 ni kwa mujibu wa Sheria yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili ametaka kujua kuhusu utofauti wa utozwaji wa tozo hizi. Tozo hizi zinatofautiana kutokana na kiwango cha ukubwa wa jengo au vile vile mita za ujazo wa jengo. Kwa hiyo, haiwezi ikawa kuna mfanano kwa namna ambavyo tozo hizi zimewekwa. Kikubwa kinachoangaliwa hapa ni mita za ujazo. Kwa hiyo, mita za ujazo zinavyozidi kuwa kubwa zaidi ndiyo tozo zenyewe zinazidi kuongezeka.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Dkt. Kikwembe.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na swali la Mheshimiwa Kapufi kuhusiana na hizi kodi za zimamoto, ninachojiuliza na wananchi wanachojiuliza hasa wa Jimbo la Kavuu wanataka kujua, kwa nini hizi tozo zimeanza kutozwa sasa, na watu gani wameshirikishwa? Kwa sababu zinaoneka zimeibuka, hata kama zilikuwepo kwa ujibu wa Sheria, zimeibuka kiasi kwamba hata wale wenye *guest houses* sasa hivi zimamoto wamekuwa wakiwavamia na kuwa-*charge* hizi kodi. Kwa hiyo, tunaomba ufafanuzi ni gazeti namba ngapi zilizoruhusu hizi kodi zianze kutumika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi ya awali kabisa ni kwamba tozo hizi

zinatokana kwa mujibu wa Sheria na Kanuni ambazo tumejiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwasababu Mheshimiwa Mbunge ameonyesha *interest* ya kufahamu namba ya *GN* ambayo siponayo hapa hiyo namba nitampatia, lakini ni kwamba tozo hizi zinafanyika kwa mujibu wa *regulations* ambayo niliisema pale awali ya *The fire and rescue force fire precaution in buildings regulations* ya mwaka *2015.* Hivyo kinachofanyika hapa hata ilikuwa ifanyike hapo awali lakini utekelezaji wa Sheria unaendelea kuwa ni halali kwa sababu ilikuwepo Kanuni hii na sasa ndiyo utekelezaji wake unafanyika.

Na. 63

**Kuutangaza Mkoa wa Tabora Kwa Utalii**

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA** aliuliza:-

Mkoa wa Tabora umepata usafiri wa uhakika wa ndege ya *ATCL* na kwa kuwa Tabora ina historia mbalimbali na kumbukumbu za mambo ya kale.

Je, Serikali ipo tayari kuutangaza Mkoa wa Tabora kwa utalii?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne Ismail Mchemba, Mbunge wa viti maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Tabora umo katika Kanda ya Kati inayounganisha Mikoa ya Dodoma, Singida na Kigoma. Ni kweli kabisa kuwa Mkoa wa Tabora kama sehemu ya Kanda ya Kati una historia mbalimbali na kumbukumbu za mambo ya kale ikiwa ni pamoja na Tembe lililokaliwa na *missionary* Dkt. Livingstone, ambaye ni mpinga biashara ya utumwa kutoka Uingereza mwaka 1871 akiwa

njaini kuelekea Ujiji - Kigoma. Pia kuna kituo cha njia ya kati ya biashara ya utumwa na vipusa vilivypo Ulyankulu eneo la Mtemi Mirambo na Gofu lililokuwa hospitali ya kwanza ya Kijerumani katika Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tembe la Dkt. Livinstone limekarabatiwa na kuna Watumishi ambao wanatoa maekelezo kwa wageni wanaotembelea kituo hicho. Katika mwaka wa fedha 2013 hadi 2017 kituo kilitembelewa na wageni 1,642 na jumla ya shilingi 2,292,000 zilikusanywa kutoka kwa watalii wa ndani na nje. Aidha, mipango ya usimamizi wa maeneo mengine niliyoyataja hapo juu imeandaliwa ili yaendelezwe kuwa vituo vya kumbukumbu na taarifa kwa matumizi mbalimbali yakiwemo ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufanisi wa utangazaji, utalii wa Mkoa wa Tabora juhudi za utangazaji zinahusu vivutio vingine zaidi ya vivutio vya mambo ya kale vinavyopatikana katika eneo hilo. Juhudi hizo zinahusu utamaduni, wanyamapori, mazao ya nyuki na historia pana ya harakati mbalimbali za kijamii za nchi yetu zilizofanyika Mkoani Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa juhudi za kuendeleza na kuutangaza Mkoa wa Tabora kiutalii zimekuwa zikiendelea hata kabla ya kuwepo kwa usafiri wa ndege ya *ATCL.* Kwa kuwa sasa Mkoa umepata usafiri wa uhakika wa ndege ya *ATCL,* Serikali itaongeza juhudi za kuutangaza Mkoa wa Tabora nje na ndani ya nchi ili kuhakikisha wageni wengi wanatembelea Mkoa huo kwa lengo la kukuza utalii na kuongeza pato la Taifa.

**MWENYEKETI:** Mheshimiwa Mwanne.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo yamekidhi lakini naomba niongeze kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mkoa wa Tabora una historia nyingi sana ukizingatia pia na historia ya Baba wa Taifa, lakini wakati anajibu majibu yake Baba wa Taifa hakuwepo, hawakuongeza, kwa hiyo, niombe Wizara ya utalii iongeze kuitangaza historia ya Baba wa Taifa.

Lakini lingine kuna historia ya miembe ambayo ina umri wa miaka 100 nayo ipo kwenye njia ya watumwa. Kwa hiyo niombe niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa hivi sasa njia ya utmwa inatambulika, je, Serikali iko tayari kuikarabati ile njia kutoka Tabora hadi Kigoma - Ujiji ili iwarahisishie watalii kupita?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lingine, je, Serikali iko tayari kuwatuma wataalam kuhakikisha vivutio vyote ambavyo vipo katika Mkoa wa Tabora vinaorodheshwa? Ukilinganisha na mapato yaliyopatikana tangu 2013 mpaka 2017 ni milioni mbili, milioni mbili kuna nini? Kwa hiyo nasema kwa uchungu kwamba bado tunahitaji utangazaji wa utalii kwa Mkoa wa Tabora ni muhimu sana naomba izingatiwe, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi, halafu ajiandae Mheshimiwa Selasini.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kukarabati hii njia ambayo inatoka Tabora hadi Kigoma hili tutalifanyia kazi, tutaangalia kadri upatikanaji wa fedha utakavyokuwepo katika bajeti zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, kuhusu kuorodhesha vituo, ni kweli kabisa Tabora ina historia ndefu sana ikiwa ni pamoja na hiyo aliyoisema ambapo Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliweza kusoma katika Mkoa ule na mambo mengine mengi na mimi mwenyewe nimefika katika yale maeneo, nimetembelea na nimeyaona. Kwa hiyo orodha tuliyonayo ni kubwa na tutaendelea kuifanyia kazi,

kuiuhisha ili tuweze kuongeza mapato yatokanayo na utalii katika Mkoa huu wa Tabora.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina vivutio vingi sana vya utalii ukiacha mbuga zetu na mlima na kadhalika, wazee wetu wa zamani, machifu wana vitu vyao ambavyo walikuwa wanatumia. Tuna ngoma zetu na vitu hivi vinaaza kupotea. Sasa Wizara hii ya Maliasili na Utalii ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba vivutio kama hivi, miji yetu kama Mji wa Kilwa vinahifadhiwa kwa ajili ya vizazi vinavyokuja?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nchi yetu na ina vitu vingi ambavyo ni vivutio vya utalii. Ni azma ya Wizara yetu kuhakikisha kwamba hivi vyote vinahifadhiwa ili viweze kutumika na vizazi vijavyo viweze kuvielewa na viweze kufaidika na matunda ya hivyo vitu vyote. Kwa hiyo ni azma ya Wizara yetu, itaendelea kulishughulikia, kuvilinda na kuvihifadhi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwakasaka, halafu tunaendelea.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nukipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Mkoa wa Tabora una vivutio vingi vya utalii ukiwemo uwandaji. Ni lini Serikali itafanya uhakiki wa vitalu vya uwindaji vilivypo Tabora? Kwa sababu kuna taarifa kwamba vitalu vya uwaindaji vilivyopo vinasomeka ni vichache kuliko uhalisia wa vitalu vilivyopo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri mahibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kuna vitalu viko vingi katika nchi yetu na kazi yetu kubwa ambayo tunaifanya sasa hivi, tunapitia upya vitalu vyote ili tuweze kuvibaini na kuona vipi vinafaa na vipi havifai. Kwa hiyo badaa ya kukamilisha hilo zoezi ni wazi kabisa Mheshimiwa Mbunge atafahamu ni vitalu vingapi ambavyo vinapatikana katika Mkoa wa Tabora.

Na. 64

**Ulipaji wa Fidia Barabara ya Morogoro**

**MHE. JOHN J. MNYIKA** aliuliza:-

Eneo la hifadhi ya barabara ya Morogoro katika Jimbo la Kibamba ni pana kuliko barabara kuu nyingine nchini na inaingia katika makazi ya asili ya wananchi.

(a)Je, ni lini Serikali itawalipa wananchi fidia kwa ardhi ya asili ya tangu kabla ya uhuru ambao walihamia wakati wa vijiji vya ujamaa?

(b)Je, ni lini Serikali itawasilisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria husika ili eneo la hifadhi ya barabara iwiane na barabara kuu nyingine nchini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano napenda kujibu swali la Mheshimiwa John John Mnyika, Mbunge wa Jimbo la Kibamba, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Barabara ya mwaka 1932 *(The Highway Ordinance Cap.167)* kifungu namba 52 eneo la hifadhi ya barabara ya Morogoro kuanzia maili 10.02 yaani kilometa 16 kutoka Posta ya Zamani

mpaka maili 23.12 yaani kilometa 37 ni futi 400 ambazo ni sawa na takribani mita 120 kila upande kutoka katikati ya barabara. Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kupitia *TANROADS* imeweka nguzo za kuonesha mipaka ya eneo la hifadhi ya barabara katika eneo tajwa na maeneo mengine nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya barabara ya Morogorio kati ya kilometa 16 na kilometa 37 iko ndani ya Jimbo la Kibamba ambapo hifadhi ya barabara ni mita 120 kila upande kutoka katikati ya barabara. Hivyo Serikali haitalipa fidia kwa mwananchi yoyote wa Jimbo la Kibamba aliyejenga au aliyefanya maendelezo yoyote ndani ya eneo la hifadhi ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haina mpango wa kuwasilisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria ili kufanya eneo la hifadhi ya barabara Morogoro liwiane na barabara kuu nyingine nchini kwa kuwa eneo la hifadhi ya barabara ya Morogoro lililotengwa linahitajika kwa ajili ya upanuzi wa barabara ili kuwaiana na mahitaji ya sasa na ya miaka ijayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika majibu yake imesema kwamba upana huo wa mita 120 ni kwa mujibu wa Sheria ya Barabara ya mwaka 1932; sheria ambayo kwa sasa haipo, kwa sababu kwa mujibu wa Sheria ya Barabara ya mwaka 2007, kifungu cha 62.41 sheria hiyo ya mwaka 1932 ilifutwa. Kwa hiyo, tafsiri yake nini? Serikali ilifanya bomoa bomoa haramu, ambayo ni kinyume cha sheria. Sasa kwa kuwa Rais Magufuli akiwa Mwanza alitoa kauli ya kibaguzi yenye kueleza kwamba...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika uliza swali

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** ...nauliza swali sasa.

**MWENYEKITI:** Uliza swali

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Nauliza swali, kwa kuwa Rais maguful alitoa kauli ya kibaguzi yenye kuonesha kwamba wananchi wale wa Mwanza hawatabomolewa...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika chunga lugha zako, nakuomba uchunge lugha zako.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Swali ninalotaka kuuliza Serikali; kama Mheshimiwa Rais Magufuli si mbaguzi, Serikali itoe kauli hapa ya kuwalipa fidia wananchi wa Jimbo la Kibamba waliobomolewa kwenye barabara ya Morogoro.

**MWENYEKITI:** Mheshimwia Waziri majibu kwa kifupi.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Swali la pili.

**MWENYEKITI:** Unaanza maneno mengi mpaka unanichanganya hapa. *(Kicheko)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu serikali imesingizia Sheria, mimi nilichukua hatua kama Mbunge Rais alipopiga Mbezi akasema kwamba kama Wabunge wanataka upana wa barabara urekebishwe wapeleke Muswada wa Sheria Bungeni nilileta muswada wa sheria wa marekebisho ili barabara yote iwe mita 60 lakini Serikali ikaa njama na Katibu wa Bunge aliyekuwepo Dkt. Kashililah kuzuia muswada huu. Ni lini sasa Serikali itaachana na hizi njama na itakubaliana na kauli ya Mheshimiwa Rais na muswada utaletwa hapa Bungeni ili barabara hii iwe na upana wa mita 60 kama zile barabara nyingine nchini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la barabara limeainishwa vizuri katika

sheria kuanzia sheria niliyoitaja katika jibu la msingi, sheria ya mwaka 1932. Vilevile nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba iko pia Sheria Namba 27 ya mwaka 1959, ipo Sheria Namba 40 ya mwaka 1969, pia iko Sheria Namba 13 ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hizi zilivyokuwa zikitungwa zilikuwa zinatazama maendeleo ya barabara siku za usoni na wala siyo siku za nyuma na ukizisoma sheria hizi zilikuwa zinaainisha barabara. Kwa mfano hii sheria ya mwaka 1932 ilitaja kabisa barabara kutoka Dar es Salaam kwenda mpaka Ruvu na maeneo gani yawe na ukubwa gani, eneo lipi liwe na ukubwa upi kwa ajili ya kuzingatia maendeleo na ukuaji wa shughuli za kibinadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimshauri Mheshimiwa Mnyika, ziko taratibu za kuhakikisha kwamba kama kuna barabara inatakiwa itajwe na kufanyiwa maboresho ziko taratibu zinaanzia katika Halmashauri na Mamlaka ambazo zinasimamia barabara. Atumie fursa hiyo kuwasiliana na mamlaka yake upande wa Serikali ya Manispaa ya Kibamba ili kweza kuleta maombi. Na kwa hii Sheria Namba 13 inampa nafasi Mheshimiwa Waziri kupitia maombi kutoka kwenye mamlaka zinazosimamia barabara kuona kama kuna eneo linaweza likafanyiwa jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hakuna njama yoyote na suala la fidia itakwenda kwa mujibu wa sheria.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waziri *Chief Whip*, Waheshimiwa kaeni chini C*hief Whip* amesimama.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze kwanza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana ambayo ameyatoa hivi punde. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninayo majibu machache tu ya nyongeza. Kwa mujibu wa kanuni

zinazoendesha Bunge sehemu ya Nne ya kanuni zetu zinaonesha mpangilio wa shughuli katika Bunge letu. Sehemu ya Tano ya kanuni zetu inaonesha mpangilio wa namna majadiliano yatakavyofanywa ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwa faida ya Watanzania, si kweli, si kweli, si kweli kwamba Serikali ilikula njama na Ofisi ya Bunge ili kuzuia muswada wowote ambao uliletwa katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hiyo, ili kuweka majibu ya Serikali vizuri katika swali la nyongeza la Mheshimiwa Mnyika tunaomba tulieleze Bunge lako Tukufu kwamba swali la nyongeza lililoulizwa na Mheshimiwa Mnyika si swali ambalo lina tafsiri ya ukweli wa hali halisi iliyojitokeza katika muswada wake, na Bunge hili linaongozwa kwa kuzingatia kanuni na taratibu na sisi Serikali hatuna utaratibu wowote wa kula njama na Bunge hili.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Felister Bura.

Na. 65

**Ujenzi wa barabara ya Mbande - Kongwa - Mpwapwa**

**MHE. FELISTER A. BURA** aliuliza:-

Wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu mwaka 2015 aliyekuwa mgombea Urais kupitia tiketi ya CCM Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliwaahidi wananchi wa Kongwa na Mpwapwa kujenga barabara ya Mbande – Kongwa - Mpwapwa kwa kiwango cha lami.

Je, ni lini barabara hiyo itaanza kujengwa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano napenda kujibu swali la Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Mbande – Kongwa – Mpwapwa yenye urefu wa kilometa 49.19 ilifanyiwa usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami na usanifu ulikamilika mwaka 2013. Baada ya kukamilika kwa usanifu Serikali imeanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami kwa awamu ambapo mwezi Julai, 2017 sehemu ya barabara yenye urefu wa kilometa 11.7 kutoka Mbande kuelekea Kongwa ilianza kujengwa. Hadi mwishoni wa mwezi Oktoba, 2017 kiasi cha kilometa tano za sehemu ya barabara ya Mbande - Kongwa zimekamilika kujenga hadi tabaka la juu *(basic course)*. Mkandarasi anaendelea na kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bura.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali na kuipongeza kwa kuanza ujenzi wa barabara ya Mbande – Kongwa – Mpwapwa kwa kiwango cha lami. Naamini mwaka ujao wa fedha barabara hii itakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali; kwa kuwa mji wa Dodoma na viunga vyake unakua kwa kasi sana kutokana na Serikali kuhamia Dodoma, na kwa kuwa tusingependa mji wa Dodoma ukawa na msongamano kama Dar es Salaam; je, Serikali iko tayari na ina mkakati gani madhubuti wa kuhakikisha kwamba barabara za mzunguko katika mji huu zinaanza kujengwa kupunguza Msongamano unaoweza kuwepo mji utakapokua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, ni lini Serikali itajenga barabara nyingine baada ya barabara iliyokuwa inatoka *Shabiby Petrol Station* na *Area* D kufungwa kwa ajili ya upanuzi wa uwanja wa ndege na sasa wananchi wa *Area D*, Mlimwa, Majengo Mapya na maeneo mengine

wanazunguka mpaka Swaswa ndipo waje mjini, je, ni lini barabara hiyo itaanza kujengwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kwamba Dodoma ndiyo makao Makuu na mpango mzima wa kuhamia Dodoma unaendelea. Pia Serikali inatambua umuhimu wa kuboresha barabara zake ili kuondoa usumbufu ambao unaweza kujitokeza kutokana na ukuaji wa mji wa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeshaweka mkandarasi kwa ajili ya usanifu wa barabara za mzunguko za Dodoma ambazo zitakuwa na ukubwa wa kilometa 96. Tulitenga fedha kiasi cha shilingi 959,812,000 kwa ajili ya kuhakikisha kwamba usanifu unakamilika; na usanifu wa barabara za Dodoma utakamilika mwezi wa tano mwaka 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba hatua iliyofikiwa sasa hivi tuko zaidi ya asilimia 25 ya zoezi la usanifu na mimi ni wito wangu tu kwa maana kwamba hii kazi isimamiwe vizuri na upande wa *TANROADS* iliusanifu ukamilike ikiwezekana mapema kabla ya muda huu ili harakati za kutafuta fedha na kujenga barabara za mzunguko wa Dodoma ziweze kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, tunatambua usumbufu ambao unajitokeza na sasa hivi pia tunaona kuna foleni zimeanza kuonekana. Hii barabara anayoitaja Mheshimiwa Mbunge ambayo inaleta usumbufu kwa wakazi la eneo la *Area D,* Mlimwa na Majengo Mapya kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema ninatambua urefu wa kilometa kama mbili; barabara hii mawanzoni ilikuwa inasimamiwa na *CDA* kabla haijavunjwa. Kwa hiyo, upande wa Serikali tumechukua jukumu la kuhakikisha sasa kipande hiki cha barabara kinatengenezwa haraka ili Waheshimiwa

Wabunge wakiwa Dodoma pamoja na wananchi wa Dodoma kwa ujumla wasipate shida kutokana na shida ambayo imejitokeza baada ya ujenzi wa uwanja ule wa ndege kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo zoezi la kutafuta fedha kwa ajili ya kukamilisha kipande hicho pamoja na kusimamia maeneo ambayo yametengewa fedha kwa tija tutapokuwa na *balance* kidogo imebakia tutaanza kupeleka eneo lile ili barabara iweze kujengwa, Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, ameshakuelewa, Mheshimiwa Chikambo.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Kwanza nianze kuwapongeza Mawaziri na Manaibu Mawaziri kwa kazi nzuri wanayoifanya, Mheshimwa Rais amewaona ninyi na sisi Wabunge wenzenu tuna imani na ninyi katika kutatua kero za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize swali la nyongeza. Wakati wa Kampeni za Uchaguzi Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan aliahidi ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami, barabara inyoanzia Wilayani Namtumbo katika vijiji vya Mtorapachani, Ligusenguse na kuelekea Mchoteka na Lasi hadi Tunduru. Naomba nijue ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara hiyo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri anataka kujua ni lini tu.

**NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwa ufupi kabisa tunaratibu ahadi zote za Mheshimiwa Rais, ahadi zote za Makamu wa Rais kwa maeneo ambayo yanahusu ujenzi wa barabara. Nimuahidi tu kwamba katika kipindi cha miaka mitano hivi zoezi hili litakuwa linaendelea kukamilisha barabara zote zilizoko kwenye ahadi, ahsante.

Na.66

**Kutumia mfumo wa kununua *unit* katika maji nchini**

**MHE. SEIF K. GULAMALI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaamua kubadili mita zote za maji ili wananchi wanunue maji kwa mfumo wa *unit* wao wenyewe kama ilivyo kwenye umeme?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali, Mbunge wa Manonga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na tatizo sugu la baadhi ya wateja wa Mamlaka za Maji kutolipa ankara za maji na kulimbikiza madeni, Wizara yangu inafanya majaribio ya kutumia mfumo wa malipo kabla ya huduma yaani *prepaid system.* Kupitia mfumo huo, mteja hufungiwa kifaa maalum kinachomwezesha kulipia kwanza kiasi cha maji anachohitaji kabla ya kutumia. Hata hivyo, mfumo huo una gharama kubwa kiuwekezaji na kimatunzo ikilinganishwa na mfumo unaotumika sasa. Kwa sababu hiyo ya gharama Wizara imeagiza baadhi ya Mamlaka kuzifunga mita hizo kwa wateja wake wenye tabia ya kulimbikiza madeni ya ankara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi mwezi Oktoba, 2017 jumla ya Mamlaka za maji saba zimeanza kutumia mfumo huo kwa baadhi ya wateja wao. Mamlaka hizo ni za Miji ya Makao Makuu ya Mikoa ya Iringa, Arusha, Dodoma, Mbeya, Songea, Tanga na *DAWASCO* ya Jiji la Dar es Salaam. Mpaka sasa mfumo umeonesha mafanikio makubwa. Hata hivyo, kutokana na ukubwa wa gharama za mfumo huo, Wizara imeziagiza Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira za Daraja ‘A’ zinategemea kwa gharama zote za uendeshaji kuhakikisha kuwa zinatenga fedha katika bajeti zao ili

kuwezesha kuendelea na ufungaji wa mfumo huo kwa kadri hali ya kifedha itakavyoruhusu.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Gulamali, ajiandae Mheshimiwa Bashe atafuatiwa na Mheshimiwa Jacqueline.

**MHE. SEIF K. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kufahamu, je, Serikali ina mpango gani ya kusambaza huduma hii nchi nzima hasa katika Wilaya ya Igunga na Mkoa wa Tabora na ukifuatilia kwamba katika Wilaya ya Igunga na Mkoa wa Tabora hivi karibuni tutaweza kupata maji ya Ziwa Victoria?

Mheshimiwa, la pili, nilikuwa nataka kujua juu ya Wizara hii ya Maji, inatoa tamko gani kwa baadhi ya Mamlaka za Maji nchini ambazo zinatoa bili kubwa kwa watumiaji wa maji kuwabambikiza bili kubwa watumiaji wa maji kuliko matumizi halisi ya wananchi wanaotumia kwenye maji? Nataka kujua tamko la Serikali juu ya ubambikizaji wa gharama za maji, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru lakini nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa namna anavyopigania wananchi wake. Lakini kikubwa napenda kujibu maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ni kuhusu suala zima la usambazaji mkakati wetu kama Serikali. Safari ni hatua na hatua tumeshaianza ya kutekeleza mamlaka saba na kwa kuwa safari moja huanzisha nyingine sisi kama Serikali kwa kupata nafasi ya kuweza kutekeleza mamlaka saba tunaziagiza mamlaka zote zenye uwezo wa kujitosheleza kigharama kutenga bajeti kuhakikisha kwamba

wanatengeneza mifumo hii ili kuweza kuyafikia maeneo ya mbali katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, katika baadhi ya mamlaka kuwabambikia wananchi ama wateja gharama ambazo si halisia haipendezi, wala haifurahishi, kuona baadhi ya mamlaka zinawabambikia bei wananchi. Mimi nataka niziagize mamlaka zote nchini kwamba watoe bei halisia ambazo zimeidhinishwa na *EWURA.* Kama kuna mtu au mamlaka itakayokaidi hata kama ana mapembe marefu kiwango gani tutayakata ili kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata huduma bila usumbufu wowote.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Bashe, atafuatia Mheshimiwa Jacqueline, halafu Mheshimiwa Mtulia.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nilitaka nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri au niombe tamko la Serikali, kwenye bajeti mwaka huu tulitaka Halmashauri zote ambazo ni *class three* ambazo zina madeni Serikali Kuu kupitia *funds* zinazokusanywa na *EWURA* zipelekwe Wizara ya Maji ili madeni hayo walipwe. Leo ni wiki ya pili Halmashauri ya Mji wa Nzega imezimiwa umeme na *TANESCO* kwa sababu ya madeni yaliyotokana na Serikali Kuu kutokupeleka fedha za *utilities* kwenye Halmashauri kwa miaka mingi.

Je Serikali iko tayari leo kuitaka *TANESCO* iweze kuruhusu watu wa Nzega waweze kupata maji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nishati.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Bashe. Tumetoa maelekezo na tumeshakaa na wadau wote kwamba taasisi zote muhimu za Serikali; afya, maji, usalama na maeneo mengi waje tukae tuweke utaratibu. Hatukati umeme kama tumeshaweka utaratibu, lakini tukishaweka utaratibu halafu utaratibu ukakiuka kwa kweli sisi tunakata umeme. Nichukue nafasi hii tutakaa na Mheshimiwa Bashe

na Waheshimiwa wengine tuone namna gani ya kulifanya jambo hili ili wananchi waendelee kupata maji.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Jacqueline, ajiandae Mheshimiwa Mtulia.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto iliyoko katika Jimbo la Manonga linafanana kabisa na changamoto iliyoko katika mkoa wangu wa Ruvuma. Katika mkoa wa Ruvuma kuna changamoto ambayo itaenda sambamba na tatizo la kubadili mita za maji kutokana na mfumo wa kupata maji kwa maana ya mita ibadilike kuwa wananchi wapate maji kwa mfumo wa *unit.* Sambamba na hilo, iko miradi ambayo nilikuwa nikisema hapa mara nyingi katika mkoa wangu wa Ruvuma ambayo kimsingi inaonekana kwamba imekamilika laikini haitoi maji, na miradi hiyo inataokana na *World Bank.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *World Bank* wamefanya hiyo kazi na miradi inaonekana kwamba sasa tayari inatoa maji, lakini katika miradi hiyo kuna mradi wa maji wa Mkako (Mbinga), Ruhuwiko (Songea Mjini), Matemanga na Ndembo (Tunduru), Litola (Namtumbo)...

**MWENYETKITI:** Uliza swali Mheshimiwa Jacqueline.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango gani ya kuhakikisha miradi hii inafanyiwa marekebisho ili iweze kutoa maji na wananchi waweze kufaidika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri subiri kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni kwenye Jukwaa la Spika ambao ni Balozi mpya wa China Mheshimiwa Wang Ke, amefatana na Mheshimiwa Liang Lee na Yang Han Chin na Ndugu Liang Lee Mkurugenzi wa Siasa

na Mheshimiwa Yang Han Chin ni Katibu wa Balozi. *Thank you very much for visiting the parliament in Dodoma now I believe you have an appointment with Speaker, your free to go to the Speaker now thank you very much. (Makofi)*

Mheshimiwa Waziri endelea.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema kwamba miradi imekamilika lakini maji haitoi kwa wananchi. Lengo la Serikali kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maji na fedha zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ile. Lakini cha kushangaza miradi imekamilika haitoi maji. Labda nimuombe Mheshimiwa Jacqueline kwamba baada ya Bunge tuongozane pamoja tukaone sababu gani zinazosababisha mradi ukamilike lakini hazitoi maji? Kama kuna mtu ambaye anasababisha au kukwamisha ili maji isitoe tutalala naye mbele ili wananchi wetu waweze kupata maji.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mtulia.

**MHE. MAULUD S. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii na mimi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubaliana kwamba maji ni uhai na kila mwananchi anahitaji maji; lakini tunakubaliana pia kwamba zamani tulikuwa na mabomba yetu ya Serikali ambayo wananchi walikuwa wanapata maji bure, lakini sasa hayapo.

Je, Serikali ian mpango gani kuyarejesha yale mabomba yetu ili wananchi wetu wapate maji bure kwa wale ambao hawana uwezo ukizingatia kwamba kuhitaji maji hakutegemei uwezo wa fedha za mtu? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba zamani kulikuwa na

mabomba ambayo yalikuwa yanatoa maji bure na hivyo kusaidia wale watu wasiojiweza, lakini kwa sasa mamlaka zote zimepewa maelekezo na zina sheria kwamba kila mamlaka kwenye mkoa inashirikiana na uongozi wa mkoa kubaini wananchi wote ambao hawana uwezo kama wazee na wagonjwa, kwa hiyo wakiorodheshwa wanaendelea kupata kupata huduma ya maji bure.

Na. 67

**Ujenzi wa Mahakama Chemba**

**MHE. JUMA S. NKAMIA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Mahakama ya Wilaya ya Chemba?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Suleimani Nkamia, Mbunge wa Chemba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali ni kusogeza huduma karibu na wananchi. Juhudi kubwa zinaendelea kufanyika kuhakikisha kuwa kila Wilaya nchini inakuwa na mahakama. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali imepanga kujenga jingo la Mahakama Wilaya ya Chemba.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nkamia.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri na ya uhakika ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nilikuwa na swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya Chemba ni moja kati ya Wilaya kubwa sana katika Mkoa huu wa Dodoma na pengine kwa Tanzania kwa ujumla. Je, Serikali wakati inasubiri kujenga jengo la Mahakama katika Makao Makuu

ya Wilaya iko tayari sasa kuimarisha mahakama za Mrijo na kwa Mtoro ili kupunguza adha inayowafanya wananchi kutembea zaidi ya kilometa 170 kufuata huduma za mahakama Wilayani Kondoa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli anachokisema Mheshimiwa Mbunge kwamba Wilaya ya Chemba ni kubwa sana, na kwa sababu mahakama hii ya wilaya itaanza kujengwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019 niseme tu kwamba nimepokea ombi na mawazo ya Mheshimiwa Mbunge na sisi kama Serikali tutaona namna bora ya kuweza kuimarisha huduma katika maeneo ya Mrijo ili wananchi wasipate shida kutembea umbali mrefu kwa sababu alipokusema huko Mheshimiwa Nkamia ni mbali sana mpaka kufika katika makao makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kama Serikali katika mpango wetu wa kuhakikisha kwamba tunasogeza huduma hizi kwa wananchi tutahakikisha pia tunalifanyia kazi jambo hilo la kuboresha huduma za mahakama katika maeneo hayo ili wakati tunaendelea kujipanga katika ujenzi wa Mahakama ya Wilaya wananchi waendelee kupata huduma katika maeneo ya Mrijo na maeneo mengineyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali umekwisha. Sasa ni muda wa wageni.

Waheshimiwa Wabunge, wageni watatu wa Mheshimiwa Jumaa Aweso (Mbunge), Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji ambao ni ndugu zake kutoka Jimboni kwake Pangani Mkoani Tanga. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni walikuja kwa ajili ya mafunzo, kuna wanafunzi 36 na walimu watano kutoka shule ya msingi ya Mtakatifu Felister ya Mkoani Dodoma.

Pia kuna Wachungaji 12 ambao ni wanachama wa Kanisa la *Evangelistic Assemblies of God Tanzania* kutoka Ilazo Mkoani Dodoma, karibuni Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Idara ya Shughuli za Bunge inawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba wale ambao hawajachukua Kamusi Kuu ya Kiswahili katika Mkutano wa Nane wa Bunge wafike eneo la mapokezi kwa ajili ya kuchukua Kamusi hizo.

Tangazo lingine ni kuwa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* Mheshimiwa William Ngeleja anapenda kulitaarifu Bunge kwamba siku ya Jumapili tarehe 12 Novemba, 2017 baadhi ya Wabunge walishiriki mbio za *marathon* zilizofanyika kuanzia uwanja wa Jamhuri hapa Mjini Dodoma. Mbio hizo ziliratibiwa na uongozi wa Mkoa wa Dodoma, zilidhaminiwa na Kampuni ya Simu ya *Tigo.* Mgeni Rasmi alikuwa Naibu Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni Mheshimiwa Juliana Shonza. *(Makofi)*

Kwa upande wa Bunge, wanaume mshindi wa kwanza alikuwa Mheshimiwa Abdallah Haji Ally, wa pili alikuwa Mheshimiwa Venance Mwamoto na wa tatu alikuwa Mheshimiwa William Ngeleja. Kwa upande wa wanawake mshindi alikuwa Mheshimiwa Oliver Semuguruka. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wengine walioshirika na kujishindia medali walikuwa ni Mheshimiwa Mussa Mbarouk, Mheshimiwa Richard Mbogo, Mheshimiwa Salum Rehani, Mheshimiwa Ali Salim Khamis na Mbunge mwenyeji na Naibu Waziri Mheshimiwa Antony Mavunde. *(Makofi)*

Pia Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla alitia fora kwenye mbio za kilometa 21. Aidha mbio hizo zilihudhuriwa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Luhaga Mpina. Uongozi wa *Bunge Sports Club* unawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge walioshiriki mbio hizo. *(Makofi)*

Katibu!

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Bado kuna Miongozo?

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo.

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Mbatia, Mheshimiwa Mollel na Mheshimiwa Mbarouk. Tuanze na Mheshimiwa Mollel.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Kanuni ya 68(7) ningependa kutoa/kuelezea/kusema alichokisema hapa Mheshimiwa Mnyika kuhusu Miswada ya Wabunge na Serikali kutoruhusu kuja Bungeni au kusomwa na Wabunge husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe ni mfano, mwezi wa pili mwaka 2016 niliandika Muswada Binafsi wa Kulinda Rasilimali za Umma kwa kushirikiana na wanasheria wa humu na wa nje. Ikapokelewa na Ofisi ya Katibu wa Bunge, lakini ikafika kwenye *stage* ya mawasiliano kati ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Bunge kwamba Mwanasheria Mkuu sasa aweze kuuleta Bungeni ili uweze kujadiliwa na nina barua zaidi ya tatu za Katibu wa Bunge akimkumbusha Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuleta huo Muswada. Kilichotokea baadaye niliona imeletwa huku kama Muswada wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi ninachoweza kusema kwa sababu dada yangu Jenista amesisitiza zaidi ya mara tatu akionesha kwamba Serikali haifanyi hivyo kusema kwamba ni kweli Serikali imekuwa ikiwafanyia Wabunge hivyo na mimi niliyesimama hapa nimefanyiwa hivyo. Kwa hiyo kwa manufaa yetu sisi Wabunge wote, tupinge hili jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako sasa. Kwanza kwa nini Serikali inafanya hivyo? Kwa nini

inazuia Miswada binafsi ya Wabunge na inafikiriwa nini sasa kama kweli Wabunge tuko kwa ajili ya kutunga sheria na kuisaidia Serikali na Serikali yenyewe sasa imekuwa inatukatisha tamaa kukaa chini na kufikiri namna ya kuisaidia Serikali hii. Tufanye nini? Mwongozo wako ni nini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nafikiri Serikali ilitoa majibu sahihi na alieleza kwa upana mkubwa. Lakini labda inawezekana hukuelewa. Mheshimiwa Jenista, hebu mueleze tena akuelewe, inawezekana alikuwa...

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tena hapa nimeshika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 97(1) na mwenye Katiba ningeomba aifungue na sitaki kupoteza muda kwa sababu Wabunge wote wana Katiba; na wakienda Ibara ya 97(1) utaratibu wa kutunga sheria utaratibu huo umeainishwa. Hata hivyo, Katiba hiyo hiyo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imelipa Bunge lako Tukufu madaraka ya kusimamia shughuli zote za Serikali ndani ya Bunge kwa kuzingatia Kanuni ambazo tunazitunga sisi wenyewe Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenye wajibu wa kuleta Muswada ndani ya Bunge lako si Serikali. Serikali haina madaraka yoyote ya kutengeneza *Order Paper* wala utaratibu wa Shughuli za Bunge na kuzileta shughuli hizo za Bunge ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachotaka kumwambia Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine wote ni kwamba sisi kama Serikali Miswada tunayoileta ndani ya Bunge imepata ridhaa ya kuingia ndani ya Bunge kwa mujibu wa Kanuni hizi ambazo zinaliongoza Bunge lako. Si kwamba Miswada hiyo tumeileta kwa kupata ridhaa kutoka kwa mtu mwingine yeyote, hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ninachotaka kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge, Muswada wowote binafsi wa Mbunge yeyote na Muswada huo na wenyewe kama utakuwa umekidhi vigezo vinavyotakiwa kwa mujibu wa Kanuni hakuna haja yoyote ile ya kusema kwamba Serikali imeuzuia Muswada ule, Muswada huo utaingia Bungeni kwa mujibu wa Kanuni zinazotuongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nitaendelea kusimama na kusema kwamba si kweli kwamba Serikali kazi yetu ni kuzuia Miswada ya Waheshimiwa Wabunge kuingia Bungeni, hapana! Utaratibu wa shughuli za Bunge unaongozwa na Kanuni na unaongozwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Niwaombe sana Wabunge wasiendelee kuibebesha Serikali mizigo ambayo haiwahusu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante umejibu vizuri sana. Mheshimiwa Mollel nafasi yako imepita. Mheshimiwa Mollel tafadhali! Ndiyo Kanuni hizi zinavyosema, sasa kama Kanuni hii inakushinda hii ya miswada kweli utaiweza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mbatia, ajiandae Mheshimiwa Mbarouk halafu Mheshimiwa Matiko.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba kutumia Kanuni ya 68(7) pamoja na ile ya 64(1)(a). Kwa kuokoa muda sitazisoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kuhusu swali namba 64 lililojibiwa leo hapa Bungeni na Serikali la Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *The Road Act* ya mwaka 2007 kile kifungu cha 62(4)(1) kinasema; *The Highways Act is hereby repealed* na kwenye sheria hiyo haielezei utaratibu wa upana wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba mwongozo wako ili kuweka kumbukumbu za Bunge vizuri.

Serikali ilivyotumia sheria kwamba ndiyo iliyoweka upana wa mita 120 na 120 si sheria imeweka hiyo huwa ni *regulations.* Kwa hiyo, ingependeza Serikali ijibu swali hili upya ili ilete taarifa sahihi Bungeni kwa sababu taarifa hizo hazikuwa sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na (b) ni Serikali itumie hekima tu kwa wananchi wa Kibamba. Upana wa barabara wa zaidi ya robo kilometa yaani mita 240 sio jambo la kheri kwa maendeleo endelevu ya Taifa letu.

**MWENYEKITI:** Unayo Kanuni hapo ? Ulikuwa unaisoma nafikiri.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Ninayo.

**MWENYEKITI:** Soma Kanuni ya 45(3).

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Kanuni ya 45?

**MWENYEKITI:** Kanuni ya 45(3).

**MHE. JAMES F. MBATIA:** "Iwapo Spika ataridhika kuwa swali la msingi au nyongeza halijapata majibu ya kuridhisha, ataagiza lijibiwe kwa ufasaha zaidi katika kikao kingine cha Bunge."

**MWENYEKITI:** Haya, tutalipokea hilo. Mheshimiwa Mbarouk.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Mimi nimesimama ka Kanuni ya 68(7) na Mwongozo wangu kwako ni kama ufuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati likijibiwa swali namba 63 kwenye maswali ya nyongeza lilizungumzwa suala la utalii hapa kwa vivutio ambavyo vipo katika Mkoa wa

Tabora. Sasa katika Jiji letu la Tanga kuna kivutio kikubwa ambacho ni cha kihistoria lakini pia yawezekana ikaja ikawa ni urithi wa dunia kwa siku za baadae cha *Amboni Sulphur Bath.* Kwa wale wenyeji wa Tanga, *Amboni Sulphur Bath* kwa Kiswahili tunasema Amboni Maji Moto, kwamba ni maji ambayo kama mtu ana ugonjwa wa ngozi au ana matatizo ya tumbo akitumia yanaweza kumsaidia. Lakini naona kama vile kimesahaulika na kwa sasa hivi kufuatia ujenzi wa Kiwanda kile kikubwa cha Saruji kutaka kuongeza eneo yawezekana lile eneo likatolewa kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanda cha Saruji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Mwongozo wako kwa Wizara ya Maliasili na Utalii. Haioni kwamba iko haja ya kutumia chanzo kile cha kitalii na cha kihistoria kukipeleka katika *UNESCO* ili ikawa ni urithi wa dunia? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa hiki sio kipindi cha maswali na majibu, tunafanya tu mahsusi kwa sababu tunajua Wabunge mnayo kiu ya kutaka kujua *what is happening!* Serikali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni suala jipya na sisi kama Serikali tunaomba lije kwa utaratibu maalum ili na sisi tuweze kuwa tunalifahamu vizuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nimesimama kwa Kanuni ya 47(1) kuhusu jambo la dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Wabunge wote watakuwa *aware* kwamba nchi yetu sasa hivi imekuwa na sintofahamu ya usalama wa raia. Tumeshuhudia mambo mengi yakiendelea kama kuokotwa kwa maiti kwenye fukwe za bahari na Ziwa Victoria. Juzi waliokotwa watu watatu

wanaosadikika ni wafanyabiashara wamefungwa, wametupwa kandokando ya Ziwa Victoria upande wa Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo langu la Tarime tumeshuhudia kuna kijana anaitwa Leonard Marwa ameuawa, kafungwa na mawe katupwa kwenye Mto Msati. Juzi tumeshuhudia kijana anaitwa Hassan hapa Merriwa; mimi nakaa Merriwa; ameuawa ametupwa kwenye bonde. Lakini hatuishii hapo, kuna watu/raia wanne juzi walitekwa tarehe 7 Novemba, 2017 Dar es Salaam kwenye *Pub* ya Sebrin; ilienda gai aina ya Noah rangi ya *silver* wakajitambulisha kwamba ni askari polisi wakawateka hao wananchi wa Tanzania, Sayuni Nsoo na wenzake. Mume wa huyu raia wakafuatilia wakaenda mpaka Mabatini na kwingineko, walivyo *trace* simu zao zikawa zinaishia maeneo ya Mikocheni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikizingatiwa kwamba Bunge hili hili...

**MWENYEKITI:** Uliza Mwongozo wako, usianze maelezo...

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Najenga hoja!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili hili lililopita baada ya tukio la Mheshimiwa Lissu tuliunda Kamati teule ambayo ingetoa uwanda mpana wa kuweza kujadili Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama ambayo ingetoa uwanja wa kuweza kujadili usalama wa nchi yetu. Wananchi wana hofu sasa hivi hata za kufanya shughuli zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi kile mkasema Mwenyekiti anahitaji siku tatu, lakini mpaka sasa ripoti haijaja. Kwa hiyo naomba hili jambo liwe la dharura leo, nitoe hoja tu-*discuss* na Waheshimiwa Wabunge waniunge kwa sababu nchi imekuwa tete. Kuendelea kuokota maiti, watu kutekwa. Naomba kutoa hoja ili tuweze kujadili hili jambo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge Mwongozo wako Mheshimwa Matiko ulishatolewa *ruling* na Kiti. Kwa vile umetaja mambo mengi, orodha ya watu wengi, Bunge hapa tutajadili nini bila ya kuwa na taarifa sahihi. Kama una hoja hiyo ambayo unaiona ni ya msingi ipeleke kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Sasa ndiyo *ruling* ninayoisema, sasa kama huitaki hiyo *ruling* yangu usiulize maswali kwenye Kiti.

Katibu!

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

## Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

## KAMATI YA MIPANGO

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Kamati ya Mipango.

Tukae!

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuchangia Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, eneo hili ni muhimu

ambalo Serikali ililipa umuhimu mkubwa sana. Ili Serikali ijipunguzie mzigo wa kubeba miradi mingi mikubwa ambayo yote ina dhamira ya kuliletea Taifa maendeleo, mimi sioni sababu kwa nini Serikali isichukulie mradi wa Daraja la Kigamboni na Mradi wa Mabasi ya Mwendo Kasi Dar es Salaam kama kielelezo cha mfano. Tatizo lipo wapi? Inaonekana wazi kuna hofu katika eneo hili ambayo haina msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo mifano duniani ambako nchi nyingi zimepiga hatua kupitia utaratibu huu. Naomba Serikali iwekeze katika sekta ya barabara, hospitali, kilimo, usafiri wa anga, reli pamoja na usafiri wa maji kupitia *public private partnership (PPP)* hii njia pekee itafanya nchi isonge mbele, kwani nchi yote ni kubwa na kila mkoa, wilaya na jimbo ina changamoto tofauti, tusipochukua hatua itachukua miaka kama si karne kutimiza matarajio ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ya kilimo, mifugo, uvuvi, wanyamapori na misitu, hili pia ni eneo ambalo Serikali anabidi kuweka msisistizo ili kufanya nchi iongeze Pato la Taifa. Yapo maeneo mengi ambayo yana fursa, kama yangetumika vema basi uchumi ungeongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengi ya nchi yetu hasa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini yanalima sana mahindi. Hivi ni lini Serikali itatoa utaratibu wa kuhakikisha kuwa eneo hili linakuwa eneo maalum kwa ajili ya uzalishaji wa mazao ya mahindi ili nchi izalishe kwa ajili ya ndani, pia ili tuweze kuuza nje ya nchi? Hili linawezekana tukiweka utaratibu wa kulima kwa njia ya kisasa. Wananchi wa maeneo haya kupata pembejeo za kisasa, mikopo ya riba nafuu na kupatiwa ruzuku kama nchi nyingine duniani wanavyofanya. Hii pia itafanikiwa katika sekta nyingine za mifugo, uvuvi, wanyamapori na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bomba la mafuta kutoka Hoima (Uganda)- Chongoleani (Tanga), niipongeze Serikali kwa mradi huu mkubwa ambao utatoa fursa kubwa

ya kiuchumi katika nchi na hasa katika mkoa wetu wa Tanga ambapo bomba la mafuta litapita katika Wilaya nyingi ikiwemo Wilaya ya Kilidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona Serikali itatengeneza barabara ya kiwango cha lami kutoka Handeni hadi Singida ambapo barabara hii itapita. Jambo hili ni zuri sana na niipongeze Serikali. Ni dhahiri kwa ukubwa wa mradi huu na thamani si busara eneo la bomba linapopata kuwa na barabara mbovu. Niiombe Serikali itenge fedha kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ili ijenge barabara hii kama ilivyokusudia. Aidha, barabara hii ni kiungo muhimu cha mikoa minne ya Tanga, Manyara, Dodoma na Singida na zipo shughuli nyingi tu za kiuchumi kwa barabara hii. Wakati muafaka umefika kujenga barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Wakala wa Barabara Vijijini *(TARURA),* uanzishaji wa Wakala wa Barabara ya Vijijini utasaidia kufungua mawasiliano ya barabara za vijiji vyote; hii itasaidia sana kutimiza uchumi wa wananchi wote. Ni wazi maeneo mengi ya nchi yetu hususan barabara za vijiji vyote bado yana changamoto za kutopitika. Niishauri Serikali iimarishe Wakala wa *TARURA* kwa kupatiwa wataalam wa kutosha na iongeze ujuzi wa kutosha hasa katika barabara hizi, hii itasaidia sana kuunganisha barabara za vijiji na barabara kuu. Aidha, wakala huyu wapatiwe vitendea kazi vya kutosha vinginevyo utendaji utazorota.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pamoja na pongezi naomba nichangie Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2018/2019 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miundombinu ya barabara, naomba niipongeze Serikali kwa hatua

mbalimbali za kuboresha barabara zetu hapa nchini. Hata hivyo kuna dosari kadhaa ambazo zinatakiwa kupatiwa ufumbuzi wa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano barabara za Mkoa wa Dar es Salaam, barabara ya Tabata Dampo kuelekea Tabata Segerea - Kinyerezi - Malamba Mawili - Msigani mpaka Mbezi, barabara hii imekuwa kero kubwa na adha ya foleni hasa nyakati za kuanzia saa 12.00 asubuhi mpaka saa 4; na saa 10.00 jioni hadi saa 3.00 usiku, na ikizingatiwa barabara ndiyo lango la kubebea mitambo mikubwa ya Mradi wa Gesi Kinyerezi. Kwa sababu hizo na nyingine tunaiomba Serikali ipanue barabara hiyo kutokana na idadi kubwa ya watu na watumiaji wengine kama mradi wa Kinyerezi (Mradi wa Gesi).

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Segerea Sheli kuelekea Seminari hadi Majumba Sita, tumeiomba Serikali iweke barabara hii kwenye mpango wa dharura wa muda mfupi na pia iwekwe kwenye mpango wa kujenga barabara hiyo na Daraja la Seminari ili wananchi waweze kutumia barabara hiyo kwa manufaa. Barabara hii Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania John Pombe Magufuli, wakati wa Kampeni ya Uchaguzi Mkuu 2015 akiwa Vingunguti aliahidi kuwa barabara ya Segerea Shelil *(Oil Com)*kupitia Segerea Seminari hadi Majumba Sita ijengwe kwa kiwango cha lami na daraja lake. Kwa muda huu yafanyike matengenezo ya dharura hasa pale eneo la Sheli *(Oil Com)* ambapo njia inapitika kwa shida sana. Wakazi wa eneo hilo wamekata tamaa. Kwa kuanzia angalau kifusi cha mawe ili kunyanyua barabara maana pamechimbika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara kuu na barbara za mitaa; barabara nyingi hazifanyiwi matengenezo kwa wakati, hali hii inasababisha Serikali yetu ya CCM ilaumiwe. Naomba Serikali iweke kitengo madhubuti kitakachofanana na kuendana na kasi ya Mheshimiwa John Pombe Magufuli Rais wetu ili kitengo hiki cha ukaguzi wa barabara kuu na barabara za mitaani kiweze kutambua

tatizo mapema kuliko tatizo litolewe na vyombo vya habari. Hali hiyo huwa inaleta fedheha kubwa, ikizingatiwa kuna viongozi na watendaji katika ngazi za kata na kadhalika walitakiwa kujua tatizo kabla. Kitengo cha ukaguzi kiongezewe vitendea kazi kama magari na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maji Dar es Salaam. ninaipongeza Serikali kwa kuboresha upatikanaji wa maji katika Mkoa wa Dar es Salaam kwa asilimia 70; wananchi wa Dar es Salaam wamefurahi sana kwa kupata maji. Hata hivyo tunaiomba Serikali iharakishe upatikanaji wa maji katika maeneo ambayo hutegemea chanzo kingine cha maji, kwa mfano wananchi wa Kipera – Pugu, Majohe, Chanika, Msongola, Kitunda, Chamazi na maeneo ya Mwinuko ambao hawapati maji ya uhakika. Tunaomba kasi iongezwe zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu ya ufundi na ujuzi, Serikali iangalie kwa upana zaidi kwa kuanzisha vyuo vingi vya ufundi ili viweze kutengeneza rasilimali watu wenye ujuzi wa fani mbalimbali kama mafundi wa mitambo midogo midogo, mafundi wa kutengeneza vifaa vya umeme, vifaa vya ujenzi; vifaa ambavyo soko lake litatokana na matumizi yetu ya kila siku sisi Watanzania. Kwa mfano kutengeneza vifaa vya ngozi (viatu, mikanda, mabegi, vifaa vya umeme aina zote za majumbani, vifaa vya ujenzi pamoja na vifaa (vipuri) vya mitambo midogomidogo pamoja na ujuzi wa aina nyingine ambazo zinaweza kuleta mabadiliko makubwa ya kiteknolojia na kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili la mafunzo ya ufundi na ujuzi itasaidia kuruhusu vijana wengi wanaomaliza darasa la saba, kidato cha nne na kidato cha sita, kupata mafunzo na baada ya hapo kupelekwa kwenye viwanda husika. Serikali si vibaya ikafuata mfumo uliotumika katika nchi ya Singapore ya kufanya mapinduzi ya kuwafundisha vijana wao wengi mafunzo ya ufundi na ujuzi kwa kuanzisha vyuo vingi vya ufundi na ujuzi mbalimbali na walitilie nguvu katika masuala ya vifaa vya umeme.

Mheshimwia Mwenyekiti, naunga mkono hoja pamoja na maoni yangu, nawasilisha.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Mradi wa Umeme wa Makaa ya Mawe Mchuchuma; Serikali imekuwa na kigugumizi cha kuanza utekelezaji wa mradi wa Mchuchuma. Naomba Serikali sasa ianze mara moja kutekeleza Mradi wa Mchuchuma na Liganga kwa sababu ahadi zimekuwa kwa muda mrefu lakini hakuna utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madini na gesi, naiomba Serikali ihakikishe inakusanya mapato kwenye madini kama kodi za wawekezaji kwani tuna migodi mingi lakini hatukusanyi mapato mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kodi, vyanzo vyote vya mapato vimechukuliwa na Serikali Kuu. Halmashauri zinashindwa kujiendesha kwa sababu hazirudishwi kwenye Halmashauri. Hii inakatisha tamaa kwani watendaji wetu wanashindwa kabisa kuendesha Halmashauri; Halmashauri zinakufa. Naiomba Serikali irudishe vyanzo hivyo vya mapato kwenye Halmashauri zetu ili utendaji wake uwe bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kilimo, asilimia kubwa ya Watanzania ni wakulima. Tunapanga kwenda kwenye Tanzania ya viwanda, hatuwezi kwenda kwenye Tanzania hiyo kama hatujaboresha kilimo. Bado Watanzania tunalima kwa mikono, pembejeo ni gharama, bei ya vyakula ni chini. Tunawezaje kuingia kwenye ushindani wa masoko? Kwa vyovyote vile hakuna soko tena. Matokeo yake hatuwezi kuondoa umaskini katika nchi hii. Naiomba Serikali ione namna gani itaboresha kilimo na kuwasaidia wakulima. Naiomba Serikali ipunguze bei za pembejeo na pembejeo zifike mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara wananyanyasika sana, wanabanwa kila upande, wanatozwa kodi kubwa ambayo hailingani na mitaji yao, hasa wafanyabiashara wadogo. Wafanyabiashara wengi

wamefunga biashara zao kwa sababu ya usumbufu mkubwa wanaoupata hapa nchini. Naiomba Serikali iangalie namna ya kuwatoza kodi wafanyabiashara hawa bila kuwanyanyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mungu kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyopo mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wanaopata nafasi ya kujiunga na masomo ya elimu ya juu wamekumbana na changamoto ya kupata mikopo, hasa wanafunzi wenye mahitaji. Ninatambua pia umuhimu wa kutoa fursa zaidi kwa wanafunzi wanaochukua masomo kusomea taaluma zenye upungufu, sayansi *etc.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapendekeza Sera ya Elimu ya Juu na Kanuni zake zipitiwe upya, kwa sababu wanafunzi wanaofaulu kwa kiwango cha juu kidato cha sita ni wale waliosoma shule binafsi zenye mazingira mazuri ya kujifunzia, walimu, vitabu, maabara na kadhalika, matokeo yake, hao wenye uwezo ndio wanapata mikopo wakati si wahitaji. Karo za shule walizosoma ni ghali kuliko ya vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, lile lengo la kutoa mikopo kwa wahitaji na wanaotoka kwenye familia zenye uchumi mdogo/duni, halikufikiwa. Kwa wakati huu, utaratibu wa kutoa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu ufanyiwe mapitio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti ya Benki ya Dunia katika uzinduzi wa Ripoti ya Kumi ya Mwenendo wa Uchumi Tanzania imeonesha wazi kwamba katika nusu ya kwanza ya mwaka huu wa 2017, uchumi umeshuka kutoka 7.7% hadi 6.8% ukilinganisha na kipindi kama hicho mwaka jana (2016). Ripoti hii inanipa

wasiwasi juu ya jinsi mpango huu unaoandaliwa utakavyotekelezwa kama mapato yetu ya ndani yatapungua siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari zetu *(TPA)* hasa ya Dar es Salaam mizigo imepungua sana kutokana na ongezeko la tozo kwa mizigo iendayo nchi za jirani pamoja na mifumo mibovu ya bandari yetu. *TPA* imeshindwa kuboresha mifumo na miundombinu yake kutokana na kwamba mapato yake yanapokusanywa na *TRA* yanapelekwa kwenye *Consolidated Fund Account* na ama hayarudishwi au yanarudishwa baada ya muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri wakati atakapojibu hoja za Waheshimiwa Wabunge aeleze kama fedha/mapato ya *wharfage* ya *TPA* yanarudishwa kwa wakati au Mheshimiwa Waziri anaweka *time frame* ya mapato hayo kurudishwa *TPA.* Vinginevyo bila *modernization* ya *TPA,* wateja wengi watapitishia mizigo yao Durban, Beira au Maputo na matokeo yake bandari itakufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kilimo cha umwagiliaji, napenda kuunga mkono kwamba fedha zitengwe za kutosha katika sekta ya kilimo, hasa kilimo cha umwagiliaji, kilimo cha kutegemea mvua kimeongeza umaskini kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta za mifugo na uvuvi; nchi yetu inajivunia sana kuwa na mifugo wengi, ikiwa ni ya pili Barani Afrika baada ya Ethiopia. Mifugo inaweza kubadilisha sana kiwango cha maisha ya wafugaji kama mkazo utawekwa katika ufugaji wa kisasa. Ufugaji una faida nyingi licha ya nyama na maziwa, ngozi yake inaweza kuliingizia Taifa fedha nyingi. Serikali pia inashauriwa kudhibiti kwa uingizaji wa nyavu ndogo badala ya kuzichoma na hivyo kuongeza kiwango cha umaskini kwa wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Benki ya Wanawake na Benki ya Kilimo, benki hizi mbili zingeweza kuchochea maendeleo ya wananchi wa kima cha chini. Bahati mbaya

Serikali na *BOT* wameshindwa kuisimamia Benki ya Wanawake na hivyo mtaji wake kushuka chini ya kiwango kinachokubalika kisheria. Serikali pia imeshindwa kutimiza ahadi zake za kuiongezea Benki ya Kilimo mtaji kama ilivyoahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *out of Tshs. 800 billion* ambazo Serikali ilikuwa iipatie *TADB,* ni *Tshs. 60 billion* tu ambazo kati ya hizo, ni *Tshs. 10 billion* tu za kukopesha tangu mwaka 2015, mpango ulikuwa *TADB* ipatiwe *Tshs. 10 billion* kila mwaka. Hii *undercapitalization* ya benki hii itaifanya isiweze kukopesha wakulima na hivyo kilimo kuzorota.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kati ya hizo *Tshs. 10 billion,* ni *Tshs. 2 billion* tu ndiyo wamekopeshwa wakulima. Fedha nyingine zimekopeshwa benki nyingine. Katika kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, naomba Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge kwamba atahakikishaje *TADB* inaongezewa mtaji wa *Tshs. 10 billion* kila mwaka na jinsi Mheshimiwa Waziri anavyoweza kuisimamia benki hii ili fedha ziwafikie wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umeme wa vijijini *(REA),* viwanda haviwezi kuanzishwa bila kupeleka umeme kwenye vijiji. Pamoja na kuanzishwa kwa *Rural Energy Fund, TANESCO* wameshindwa kuwasilisha fedha, kiasi cha *Tshs. 7.4 billion* kwa Mfuko wa *REA* zitokanazo na *levy* pamoja na faini ya ucheleweshaji. Ni vyema Mheshimiwa Waziri wa Fedha atueleze kwa nini *TANESCO* hailipi deni hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashirika ambayo Mpango huu katika ukurasa wa 48 unalenga kuyaimarisha na kuyatumia katika kuleta mageuzi ya viwanda nchini, ni vizuri Mheshimiwa Waziri akayaangalia upya kama watumishi waliopo wanaweza kwenda na kasi ya Sera ya Viwanda. Kwa mfano *SIDO, STAMICO, CARMATEC* na *COSTECH* wana rekodi ambazo si nzuri kiutendaji. Mheshimiwa Waziri atuhakikishie kwamba taasisi/mashirika haya yana wafanyakazi wenye ujuzi, waadilifu au uwezo wa kwenda na kasi ya Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, *SIDO* wameacha kilio kikubwa sana kwa wakulima wa tangawizi Wilayani Same. Tangu mwaka 2012 wametengeneza mashine za kuchakata tangawizi ambayo haijafanya kazi hadi sasa, hivyo kuwatia hasara kubwa sana wakulima. *CARMATEC* wana maeneo mengi waliyopewa kazi ya kutengeneza mitambo ya *biogas* na uvunaji wa maji, lakini hawakukamilisha kazi hizo pamoja na kulipwa fedha zote. *COSTECH* walipewa kazi ya ushauri na *NIDA* na kazi yao haikutumika hata baada ya kulipwa fedha nyingi; ina maana ushauri wao haukukidhi mahitaji ya *NIDA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matumizi mabaya ya fedha za umma, katika kipindi kinachoishia Juni, 2016, kati ya mapendekezo 3,898 yaliyotolewa na *CAG,* ni mapendekezo 1,449 tu (37%) yaliyotekelezwa kikamilifu. Hata zile Wizara zilizobainika kutumia fedha vibaya zilizopitishwa kwenye bajeti, bado Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameendelea kuwaongezea fedha kwenye bajeti. Nimuombe Mheshimiwa Waziri atoe mapendekezo jinsi atakavyoweza kuweka mpango madhubuti wa kuhakikisha mapendekezo ya *CAG* yanafanyiwa kazi kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusus suala la kutozingatiwa sheria ya manunuzi na mikataba mibovu. Serikali imekuwa inapoteza fedha nyingi kutokana na Wizara na taasisi zao kutozingatia Sheria ya Manunuzi, kuingia mikataba mibovu na kushindwa kuwalipa wakandarasi kwa muda wa makubaliano. Matokeo yake Serikali inapoteza fedha nyingi zikiwemo za kulipa faini. Fedha hizo zingetumika katika kuleta maendeleo. Waziri alihakikishie Bunge jinsi Wizara yake itakavyosimamia jambo hili kuzuia upotevu wa fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo hapo juu, naamini yatasaidia katika kuboresha Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2018/2019.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii

ya kuchangia katika mpango huu wa maendeleo. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa juhudi kubwa anayochukua katika kuongoza nchi hii. Namuombea Mungu ampe uwezo na afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii ya Fedha, Naibu Waziri na watendaji wake wote kwa umakini wa kuandika na kuwasilisha Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia Mpango huu napenda kusisitiza maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kuhusu kuongeza uwezo wa kupambana na umaskini kwa wananchi. Miongoni mwa kundi kubwa la wananchi wa Tanzania ni wafanyabiashara na wakulima. Hivyo, ni vyema Serikali kuendelea kuchukua juhudi za makusudi kuwawekea mazingira mazuri ya kufanikisha shughuli zao. Serikali inapaswa kuwawekea utaratibu maalum wa kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu ili waweze kufanya biashara zao kwa utulivu na kuweza kujipatia kipato kuweza kupunguza umaskini, hasa wafanyabiashara walio wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa sekta ya uvuvi, sekta hii bado haijaonesha mafanikio katika kuwaendeleza na kuwanyanyua wavuvi wa nchi hii. Bado mpaka leo wavuvi wanahangaika kwa kukosa vifaa vya uvuvi vya kisasa. Hivyo, naiomba Serikali ichukue juhudi za makusudi kuwaendeleza wavuvi kwa kuwapatia zana za kisasa. Aidha, Serikali iunde benki ya wavuvi, ili iweze kuwakopesha wavuvi kwa kuweza kumudu kununua vifaa vya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi ya maendeleo, Serikali ina nia nzuri katika kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo, lakini miradi mingi katika nchi yetu inakosa ufanisi kwa sababu kadhaa. Moja kati ya sababu hizo ni upatikanaji wa fedha kwa wakati. Hivyo,

naiomba Serikali kupeleka pesa kwa wakati katika taasisi husika ili kuweza kwenda na wakati wa mipango kazi ya miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, pamoja na timu nzima ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuleta mapendekezo mazuri ya Mpango na pia Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2018/2019. Naomba nipendekeze kuwa katika kipaumbele cha viwanda vya kukuza uchumi na ujenzi wa msingi wa uchumi na viwanda msukumo wa kuboresha kilimo, hasa katika suala la bei na uhakika wa masoko ya mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuboresha kilimo tutaweza kuwa na malighafi ya kutosha kwa viwanda vyetu. Pamoja na msukumo wa kuanzisha kanda maalum za kiuchumi na kuimarisha *SIDO,* napendekeza katika mpango kuwepo na viwanda vidogo huko vijijini ili kuongeza thamani ya mazao, uwepo msukumo wa viwanda vya kuchakata pareto kutokana na mahitaji makubwa ya duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipaumbele cha kufungamanisha uchumi na maendeleo ya watu, kipaumbele hiki ni muhimu sana hasa ukizingatia kuwa kukua kwa uchumi wetu kuendane na hali za wananchi hasa vijijini. Katika mpango wa mwaka 2018/2019 napendekeza Serikali iweke katika bajeti ya maendeleo umaliziaji wa miradi iliyokwama kwa muda mrefu. Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya wananchi wamejitoa sana katika ujenzi wa zahanati na vituo vya afya na pia ujenzi wa madarasa pamoja na ujenzi wa kituo cha polisi cha wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya upatikanaji wa maji hairidhishi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya. Kati ya miradi tisa iliyoanzishwa mwaka 2013, ni mradi mmoja tu uliokabidhiwa wakati zaidi ya shilingi bilioni 4.2 kati ya shilingi

bilioni 5.5 ambayo ni 84% zimelipwa, lakini wananchi hawapati maji, Serikali ihakikishe miradi hii inakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo napendekeza mradi wa maji wa chanzo cha Mto Kiwira kwa matumizi ya Wilaya ya Mbeya. Pia kuwepo na kuunganisha Mamlaka ya Maji ya Jiji la Mbeya na Mamlaka ya Maji ya Mji Mdogo wa Mbalizi. Pia kuwepo kwa bajeti ya ujenzi wa mabwawa kwa wafugaji wa Kata ya Mjele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipaumbele cha ujenzi wa mazingira wezeshi, napendekeza msukumo uwepo wa kuboresha miundombinu ya barabara vijijini. Pamoja na uchumi mzuri wa Wilaya Mbeya, hali ya barabara ni changamoto kubwa. Napendekeza msukumo uelekezwe kuboresha barabara za kuunganisha mikoa, ikiwemo barabara ya Mbalizi – Makongorosi, barabara ya Mbalizi – Shigamba, barabara ya Isyonje – Kikondo – Makete – Njombe, barabara ya Mjele – Mlima Njiwa, barabara ya Kawetere – Ikukwa, barabara ya Mbalizi – Songwe – Jojo, barabara ya Ilembo – Mwala, barabara ya Ilembo Isonso na pia, *by pass* ya Mlima Nyoka (Uyole) – Songwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza reli ya *TAZARA* iboreshwe na iende sambamba na uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Bandari Kavu Inyala, Mbeya. Pamoja na uboreshaji wa reli ya *TAZARA,* pia iwekwe kwenye bajeti ujenzi wa Reli ya Uyole, Mbeya kwenda Malawi, ili kukabiliana na ushindani wa biashara ya Bandari yetu ya Dar es Salaam na bandari nyingine kama Beira, Msumbiji na zile za Afrika Kusini na hata Angola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipaumbele cha kuimarisha usimamizi na utekelezaji wa Mpango, napenda msukumo uwekwe kuboresha ufuatiliaji na utoaji taarifa za utekelezaji, ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa mfumo utakaotoa taarifa sahihi. Taarifa nyingi za miradi zimekuwa hazina uhalisia na zinapotosha, taarifa za miradi ya maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya zimekuwa zinapotoshwa. Naunga mkono hoja.

**MHE. OMARI A. KIGODA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kuipongeza Serikali kwa juhudi zake katika kuleta maendeleo katika nchi yetu, bila ya kusahau kumpa pongezi kubwa sana Rais wetu, Mheshimiwa John P. Magufuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango endelevu inahitaji kwanza kabisa kutokuwa na watu wajinga, maradhi na maskini. Lazima mipango hii iendane na kuwanyanyua watu na kuwasaidia katika utendaji wao wa kulinyanyua Taifa. Serikali ihakikishe huduma ya ukusanyaji kodi kwa kutumia mashine za kielektroniki inakuwepo nchi nzima. Hii itasaidia ukusanyaji wa haraka na kutopoteza muda wa kutoa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni lazima Serikali ihakikishe huduma za jamii kama maji, umeme na mengineyo zinapatikana kwa wingi ili muda mwingi watu tuutumie kwenye kujenga nchi yetu. Maendeleo ya nchi lazima tuwe na *manpower* ya kutosha, kwa hiyo, tukihakikisha huduma za jamii zipo itasaidia kuwa na *manpower* ya kutosha kujenga uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali lazima ihakikishe inazingatia suala la afya ya kila mwananchi inakaa sawa na inatibika kwa urahisi, ili kutokuwa na Taifa la wenye maradhi; hii itadhoofisha ukuaji wa uchumi wetu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni suala la amani. Lazima nchi iwe na amani, ili kila mtu awe huru katika kutekeleza kazi zake za kulijenga Taifa. Lazima Serikali isisitize watu kufanya kazi ili tuweze kukwamuka kutoka tulipo, twende mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *infrastructures* zetu lazima tuhakikishe zinatumika na lazima tuweke mazingira mazuri kwa watumiaji. Mfano, gesi lazima itumike kwenye viwanda vyetu ili kuwa na uzalishaji wa kutosha. Lazima barabara zetu ziwe za kupitika muda wote, hii itasaidia kwa wakulima na wafugaji hata waoa huduma kufika kwenye *point* haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu ni muhimu sana. Taifa la wajinga haliwezi kuwa na maendeleo au kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na jiografia ya nchi yetu kuna *infrastructures* ambazo ni za mkakati *especially* kiuchumi, kwa mfano, barabara ya Handeni – Mziha – Dumila na nyingine nyingi. Hizi *infrastructures* lazima tuzitengeneze ili ziweze kutumika katika mzunguko wa biashara kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna Taifa lililoendelea bila kuwahusisha wafanyabiashara wakubwa, pia na kuwahusisha katika uwekezaji. Hivyo, ni lazima Serikali iwe karibu na wafanyabiashara na kusikia matatizo yao na kujadiliana ili kuweka mambo sawa.

Mhershimiwa Mwenyekiti, miaka 30 iliyopita *South Korea* tulikuwanao *almost* sawa, lakini kwa sasa wamepiga hatua sana kimaendeleo. Walichofanya ni kuhakikisha wanaweka mazingira mazuri ya uwekezaji na Serikali ilibaki kuchukua kodi kutokana na uwekezaji huo, pia kuhakikisha hiyo kodi inatumika ipasavyo kwenye huduma za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho napenda kumshauri Waziri, hii mipango tunayopanga ni mizuri tu endapo utekelezaji wake utapewa kipaumbele na msisitizo wa kila mtu katika sekta yake lazima afanye kazi. Hakuna uchumi unaopanda kwenye Taifa la wavivu, lazima msisitizo wa uwajibikaji usemwe mara kwa mara.

**MHE. SUZANA C. MGONOKULIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Tanzania inataka iwe nchi ya viwanda, tuboreshe sekta ya kilimo kwa kuhakikisha kwamba mikopo kwa wakulima inapatikana. Tukifanya hivyo tutakuwa tumewawezesha wakulima kulima kilimo bora. Kilimo bora kinatokana na wakulima kuwa na mbegu bora na mbolea kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sera ya elimu bure, ni miaka miwili kama Taifa tumeona kuwa elimu bure inaathari kutokana na kuporomoka kwa ufaulu wa wanafunzi. Katika mpango huu uliopendekezwa na Waziri wa Fedha, je,kuna mkakati wa makusudi wa kutatua matatizo yanayoikabili sekta ya elimu? Elimu ya kutosha inatakiwa kutolewa kwa wananchi wajue kuna baadhi ya shughuli za elimu kama wananchi wanapaswa kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango huu uliopendekezwa kwa mwaka 2018/2019, hakuna sehemu iliyoonesha ukuzaji wa viwanda katika Mkoa wa Iringa ambavyo vilikuwepo katika Mkoa huo. Mkoa wa Iringa miaka ya nyuma ulikuwa na viwanda vya *COTEX, Cocacola, IMAC*, *SIDO* na *Tyre,*viwanda hivi viliwasaidia sana wananchi wa Mkoa wa Iringa na maeneo mengine ndani ya nchi yetu kupata ajira, lakini katika mpango uliopendekezwa sijaona sehemu yoyote inayoonesha kwa mwaka 2018/2019 kuhakikisha viwanda hivyo vinaimarishwa ili kupatia ajira wananchi wa Mkoa wa Iringa na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba suala hili lipewe kipaumbele.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na Malengo ya Milenia *(MDGs)* hatukuweza kufikia malengo, tulifanikiwa maeneo matatu tu na hata hivyo *UNESCO* ilitupatia tuzo katika uandikishaji wa watoto, kwa hilo napongeza japo hatukuweza kuwa na elimu bora kwa watoto wetu japo waliandikishwa kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu kwa sasa tuna *SDGs* ambayo malengo yake ni mengi zaidi ya *MDSs.* Je, katika Mpango huu Serikali imejipangaje kuhakikisha inaingiza katika Mpango huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi yoyote makini, lazima iwe na vipaumbele vichache visivyoweza kushindwa katika utekelezaji, Tanzania kwa sasa ina vipaumbele gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawezaje kuwa na maendeleo na mipango bila kilimo. Viwanda bila kilimo ni uti wa mgongo ni vema tukazingatia kilimo maana viwanda vinategemea malighafi za kilimo.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wenye dhamana ya Fedha na Mipango kwa kazi kubwa wanayoifanya ili kuhakikisha Ilani ya CCM 2015/2020 inatekelezeka. Baada ya pongezi hizi, nina maombi yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba uangalie uwezekano wa kuutengea na kuuwekea fedha Mfuko wa Taifa wa Watu Wenye Ulemavu kama ambavyo Mfuko wa Vijana unatengewa. Mheshimiwa Waziri, Mfuko wa Taifa wa Watu Wenye Ulemavu (WWU) ni muhimu sana ukatengewa fedha, hii itasaidia sana ustawi wa WWU na hasa ikizingatiwa kuwa wana mahitaji mengi ikiwemo hitaji la mitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la pili, fedha iongezwe kwenye Kasma 280400 Mafunzo kwa Watu wenye Ulemavu ambapo mwaka 2017/2018 Kasma hii ilitengewa shilingi 600,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Idara ya Watu Wenye Ulemavu haina *sub vote,* hivyo ninaomba Mheshimiwa Waziri uliangalie hili maana mchakato ulishaanza.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango juu ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2018/2019 na Mwongozo wa mMaandalizi ya Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2018/ 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mungu kwa kibali chake na rehema zake kwa kutuwezesha kukutana ndani ya Bunge lako tukiwa na afya na nguvu ya kufanya kazi. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa uteuzi wake

alioufanya hivi karibuni kwenye Baraza lile la Mawaziri na niwapongeze wote walioteuliwa na kuzidi kushirikiana vizuri huku nikiwaasa kuwa Hapa ni Kazi Tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Rais Magufuli kipekee kwa kutimiza ahadi kwa Jimbo langu la Ileje, yeye mwenyewe kwa kutujengea barabara kuu ya kutoka Mpemba hadi Isongole kwa kiwango cha lami. Barabara ya kilometa 51.8 ambayo wananchi wa Ileje wameipigia kelele kwa miaka 42 sasa. Tunaishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kutimiza ahadi zake kwa Wilaya ya Ileje. Naishukuru Serikali kwa kutujengea Hospitali kubwa ya Wilaya Itumba ambayo itafanya upasuaji mkubwa. Tunaiomba Serikali itusaidie kumalizia hospitali hii ambayo imesimama kwa zaidi ya miaka miwili sasa. Hospitali hii inategemewa na itasaidia hata Wilaya ya jirani za Mkoa wa Songwe na Mbeya Vijijini ili imaliziwe na itazuia wananchi wa Ileje kukimbilia nchi jirani ya Malawi kupata huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kusaidia kuweka miundimbinu mizuri ya maji hasa maeneo ya Isongole, Itumba, Izuba Ilulu ambapo kumekuwa na ukame wakati wa kiangazi na kusababisha upungufu mkubwa wa maji wakati Mto Songwe uko hapo jirani kabisa. Hii imerudisha imani ya wananchi kwa Serikali kwa kiasi kikubwa sana na kuinua ari yao. Tunahamasisha Serikali kuhamasisha mipango yote ya maji kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *TRA* walikuwa na mpango wa kujenga kituo kidogo cha forodha kwenye mpaka wa Tanzania na Malawi kwenye Mto Songwe. Eneo limeshapimwa na *TRA* wamejenga ofisi ndogo ya forodha lakini bado haitoshelezi. Mpaka wa Tanzania hauna ofisi ya Uhamiaji, Polisi, Kilimo, Jeshi la Wananchi na Idara nyingine muhimu za Kituo cha Forodha Mpakani. Tunaiomba Wizara itusaidie kituo hiki kijengwe kwa kwa sababu kinapunguza msongamano wa Tunduma, kwa njia ya Ileje inapendelewa na wenye magari makubwa kwa sababu hupitia Chitipa

upande wa Malawi kutokea Isongole Ileje kuja Mpemba ni tambarare zaidi kuliko ile ya Kasumulo Kyela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia itawezesha kudhibiti mpaka huu ambao umekuwa na matukio ya wakimbizi wa Kisomalia na wengine kuutumia. Kwa hali hiyo huwezi jua athari gani nyingine zinaweza kutokea bila kuwa na kituo cha forodha sehemu muhimu hiyo ya mpaka. Aidha, hicho kituo kitasidia sana pindi mradi wa Bonde la Mto Songwe kati ya Malawi na Tanzania utakapoanza. Vyote hivi vitachangia kwa kiasi kikubwa kuchangamsha uchumi wa Ileje na Wilaya za jirani ambazo kwa muda mrefu zimedumaa kwa kukosa miundombinu ya kisasa na taasisi muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kumekuwa na mwelekeo Wizara ya Mambo ya Ndani wana mpango wa kujenga Chuo cha Uhamiaji cha Ulende katika Wilaya ya Ileje na eneo tayari limeainishwa, hii pia ingesaidia sana kujenga uwezo wa Maafisa Uhamiaji wa Tanzania lakini hata wale wa nchi za *SADC* na hii itasaidia kuinua uchumi wa Jeshi la Tanzania kwa ujumla. Hii ni miradi ya kitaifa naomba Serikali iangalie jinsi ya kutusaidia kwa kuingiza mipango yake ya kipindi hiki ili Ileje nayo ipate maendeleo ya haraka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ileje ni kati ya Wilaya inayozalisha mazao ya kilimo kwa wingi sana hususani mahindi, ulezi alizeti, mpunga, kahawa, pareto, hiliki, tangawizi, ndizi, viazi mviringo, viazi vitamu, soya, maharagwe, karanga, matunda ya aina mbalimbali pamoja na mazao ya misitu ikiwa ni pamoja na mbao, nyuki na kadhalika. Zaidi ya hayo Ileje ina uwezo wa kuzalisha maziwa kwa wingi, mifugo midogo midogo, viungo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na haya yote Ileje inakabiliwa na tatizo kubwa la upungufu wa maghala, masoko, Maafisa Ugani na kwa kiasi kikubwa mitaji kwa sababu maeneo yote ya Ileje hayajapimwa na tumehusisha upungufu wa wataalam wa kupima maeneo haya. Tunaomba Serikali iweke bajeti na nguvu ya ziada na ya upendeleo kwa maeneo ya pembezoni hasa Ileje na hasa

kwa sababu tumejaliwa kuwa na hali ya hewa nzuri sana, udongo mzuri, mvua nyingi na za kutosha ni rahisi kwa kilimo na ufugaji huwainua na kupanua uzalishaji sana kwa mazao yote hayo na huwaondolea wananchi kwenye umaskini na ukosefu wa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijikite katika mpango na nianze kwa kuwapongeza sana Serikali kwa kuwashirikisha wadau katika mchakato mzima wa kutayarisha mpango na mwongozo huu, ni jambo la kupongezwa kwa sababu limekuwa shirikishi zaidi. Lakini tunaiomba Serikali iyazingatie maoni haya na kuyazingatia katika Mpango ili uwe na tija zaidi. Maoni mengi ya wadau yanaonesha uzoefu wao kwenye soko na utekelezaji ambao umezidi ule ambao watumishi wa Serikali ambao wana ofisi tu au ni wa wananchi wanaotumiwa na masuala mbalimbali kwa hiyo, siyo ya kupuuzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali imepokea na kuorodhesha maeneo waliyopata ushauri ninaomba Serikali itupatie masharti ya jinsi wanapanga utekelezaji na fedha itakayotumia, maoni yote yaliyo ukurasa wa tano wa Mpango huu wa 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti,ni kweli uchumi wetu umekua vizuri kwa muda mrefu lakini bado kwa kiasi kikubwa tuna utegemezi mkubwa kwa wafadhili wa fedha za nje ambazo haziji zote kwa wakati. Tupate sasa wakati wa kupunguza zaidi utegemezi huu na vilevile kutumia sekta binafsi zaidi kutengeneza miradi ili kupunguza utegemezi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mfumuko wa bei kuendelea kuwa mdogo tumeona kuwa umepanda kidogo kutokana na bei za chakula kupanda na bei zinapanda kwa sababu utaratibu wa soko la mazao nchini haujawa vizuri kitu kinchosababisha wakulima kukosa mapato stahiki na wateja pia wanaathirika na kuwapa faida kubwa walanguzi. Lakini kama haitoshi zao la mahindi limekuwa yatima nchini, liliachiwa na wakulima kuhangaika wenyewe wazalishe mazao mengine kama korosho, pamba na kadhalika

kunachangiwa kwa kupatiwa pembejeo, madawa na kadhalika.

Je, ni kwa nini Serikali inaacha mazao haya yanayolisha nchi nzima na kuwawezesha wananchi kunufaika kwa biashara ya mazao yao? Serikali ije na mustakabali wa kuwasaidia wakulima wa mazao ya nafaka na jamii za kunde na ya mbegu za mafuta ili ziwe na tija na yachangie Pato la Taifa na kuwaodolea umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Deni la Taifa kuonesha liko himilivu, lakini tukiendelea hivi litatupeleka pabaya hususani kama hatutaongeza mauzo ya kuuzwa nje *(exports)* ili yabadilishe *balance of trade* yetu Tanzania. Nchi nyingi zenye deni kubwa vilevile ni nchi za viwanda zenye uchumi mkubwa, kwa hiyo malipo ya madeni hayo hayaathiri sana uendeshwaji wa uchumi. Lakini kwa Tanzania deni lilikua sana dhidi ya ukuaji wa uchumi kwa maana Pato la Taifa tutafikia hatari. Tujitahidi kuboresha na kuinua viwanda, kuanzisha viwanda vingi, huongeza masharti ya uwekezaji, kupunguza viwango vya kodi ili tupate ufanisi na mwisho wa madeni yote ya ndani na ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kuwa pato la ndani halitoshi hutokana na ukusanyaji mdogo wa mapato ya ndani, uzembe na hata rushwa. Vilevile sekta isiyo rasmi imesahauliwa katika suala nzima la makusanyo ya kodi. Sekta hii ni kubwa na ina wajasiriamali wa aina mbalimbali wadogo, wa kati na wanazalisha bidhaa na huduma za kutosha na kulipa kodi nyingi. Serikali ina mpango wa kurasimisha shughuli hizi, hili ni jambo la msingi na kwa hakika zimechelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali sasa hivi iweke utaratibu mzuri na ishirikishe. Aidha, Serikali ishirikishe taasisi zake zinasimamia vizuri sekta hii na kuwapatia huduma zao za kifedha na mafunzo ya kuwawezesha kuinua shughuli zao. Hii iendane na kuwapatia maeneo ya kufanyia shughuli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza sana Serikali kwa kuanza kutengeneza miradi ya maendeleo kwa mwaka 2016/2017 pamoja na kugharamia ujenzi wa awamu ya kwanza wa reli ya kati kwa *standard gauge* kutoka Dar es Salaam kwenda Morogoro, pamoja na miradi mingine, miradi hii mikubwa itakayoleta mageuzi makubwa ya kiuchumi, Serikali ianze kutayarisha watumishi wa kuhudumia reli hii mapema kwa kuwapa mafunzo stahiki ili imalizike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya msingi inayopanuliwa iendane na ujenzi wa madarasa ya kutosha, vyuo vya kutosha, maji na vyumba vya walimu na maabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya viwanda ni muhimu sana na tuipongeze Serikali kwa kuwezesha viwanda hivi kuanza uzalishaji na kudumisha mahusiano mazuri nao. Tunaomba mvisaidie hivi viwanda kupata umeme wa gesi wa uhakika na kuhakikisha hawapati ushindani usio wa haki na bidhaa kwa mfano, mali zinazoingizwa na *Good One* wa China amekuwa yeye mwenyewe akiagiza na kuuza jumla na rejareja lakini huwahujumu wateja wake hao hao kwa yeye kuweka bei ndogo kwenye bidhaa zake na kufanya kushindwa kuuza. Huu ni mchezo mchafu, *TFC* walifuatilie hili kwa bidhaa zote zinazoingizwa na ambazo zina sababisha bidhaa za viwanda visishindwe kuuza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali itenge pesa za kujenga vituo vya afya Wilayani, aidha, zahanati nyingi zilizojengwa kwa nguvu za wananchi sasa zimaliziwe kwa awamu hadi na kuweka vifaa na watumishi wa kutosha zimalizike zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapongeza juhudi za kuboresha huduma ya maji nchini. Tunaishauri Serikali itoe kipaumbele kwenye uvunaji maji ya mvua katika maeneo yenye tatizo la umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania bado tunalalamikiwa kwa urasimu mkubwa katika kuhudumia wawekezaji na bado tunachukua muda mrefu, hutoa

maamuzi na tunakuwa waoga kuamua. Hii inapunguza kasi ya kufanya biashara Tanzania.Jina la Tanzania sio zuri nje ya nchi, mwisho Serikali inatuhumiwa kuwa haizingatii mikataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza Serikali kwa kuboresha huduma za afya katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, lakini kuna haja ya kuhalalisha kuwa hospitali zote za Wilaya, Kata, Mitaa zinapata huduma muhimu za kutosha na vifaa na watumishi ambao wanahitajika sana kwenye maeneo yetu nchi nzima. Pesa ya kutosha hupewa kwa ajili ya huduma za afya nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kwa kuhitimisha nataka kuiomba Serikali itufanyie kuboresha maendeleo ya kilimo cha kisasa, miundombinu ya vijiji na mitaa. Wakati huo huo Serikali itoe kipaumbele katika kupima maeneo ya vijijini ili kurasimisha ardhi na kuwawezesha wazalishaji kukopa. Kilimo hakionekani kuwa kweli ni uti wa mgongo na kilete tija kubwa kwa ajili ya viwanda, ajira na mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serika ije Bungeni na mkakati wa kuanza kutekeleza miradi ya kielelezo na maeneo yale ya *SEZ* na *EPZ* ambayo yamekaa muda mrefu ilhali ni miradi muhimu kwa kuviwezesha kuanza viwanda kwa uhakika zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho tunaiomba Serikali itafakari kwa kina na kuzingatia maoni ya Wabunge kwenye Mpango wa 2018/2019.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niane na sekta ya uvuvi.

Katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2017/2018 kuhusu rasilimali za uvuvi, Serikali ilitenga shilingi bilioni 2.2, na shilingi milioni 400 tu kama fedha za ndani kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya uvuvi pekee. Fedha hii ni ndogo sana ukilinganisha na matokeo tunayoyatarajia katika sekta ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli usiopingika kwamba Serikali hii ya Awamu ya Tano inataka kuwekeza kidogo huku ikitarajia matokeo makubwa sana. Sekta ya uvuvi ni sekta nyeti ambayo inachangia katika uchumi wa Taifa na pato la mtu mmoja mmoja katika maeneo mengi ya nchi yaliyozungukwa na maji. Jambo la kushangaza jamii za wavuvi zimekuwa ni jamii zinazoishi maisha duni sana pamoja na ugumu na changamoto nyingi wanazopitia wavuvi ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa zana bora na za kisasa katika kufanya uvuvi wenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi wamekuwa wakitozwa kodi nyingi huku miundombinu ikibaki vilevile. Wavuvi wa Tanzania hususani wa Mkoa wa Mara wamekuwa wakinyanyasika kwenye kulipa tozo nyingi, hawana uhakika wa mikopo na pia usalama wa kutosha wawapo katika shughuli zao usiku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi kama Norway imekua sana kiuchumi kwa kuwekeza katika sekta ya uvuvi pekee. Leo hii katika nchi za Ulaya, Norway ni nchi inayoongoza kwa kuwa na *GDP* kubwa ambapo sehemu kuwa ya Pato la Taifa hutokana na uvuvi tofauti na hapa nchini ambapo jamii ya wavuvi ndio jamii maskini wa kutupwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usafiri wa anga, uwanja wa ndege wa Musoma, katika mpango huu wa maendeleo 2017/2018 hakuna mahali panapoonesha mkakati maalum wa ukarabati wa uwanja wa ndege wa Musoma. Ni dhahiri uwanja huu ni muhimu sana katika kukuza sekta ya utalii kwa Kanda ya Serengeti. Uwanja wa Ndege wa Musoma ni wa muhimu sana katika kuchochea ukuaji wa uchumi wa Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na sababu za kiuchumi uwanja wa ndege wa Musoma ni muhimu katika historia ya ukombozi wa nchi yetu. Uwanja huu umebeba historia ya Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Hivyo ni muhimu kwa wageni wanaokuja nchini

kutembelea makazi ya Hayati Baba wa Taifa ambaye aliipigania ukombozi wa nchi hii kwa gharama kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ni vema sasa Serikali ione umuhimu wa kuuweka uwanja huu katika vipaumbele vyake ikiwa ni pamoja na kuutengea fedha za kutosha na kukamilisha ukarabati kwa wakati kama vile ilivyofanya kwenye uwanja wa ndege wa Chato. Pamoja na hilo, uwanja huu utakuwa kichocheo kikubwa cha uchumi kwani hata shughuli za uchimbaji madini zinazofanyika Mkoani Mara zitaimarika zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naamini Mkoa wa Mara una wasafiri au watumiaji wengi wa ndege wanaofanya biashra katika maeneo mbalimbali ya ndani na nje ya nchi ikiwemo nchi jirani ya Kenya. Hivyo Serikali itueleze ni lini itakamilisha uboreshaji wa uwanja huu ili wananchi hawa waweze kunufaika. Naomba kuwasilisha.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta ya nishati, Mpango unaonesha mpaka mwaka 2020 uzalishaji wa umeme ufikie zaidi ya Mw 5000 *Installed Capacity,* kwa sasa ni Mw 1358 na mradi wa *Stieglers Gorge* utazalisha Mw 2100. Je, Mw 1542 itatokana na mradi upi ili kufikia lengo la Mw 5000 mpaka ifikapo mwaka 2020?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango haujaainisha kama itashirikisha sekta binafsi au itatumia mradi upi kufikia lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali katika mradi wa *Stieglers Gorge* itumie teknolojia ya kisasa ya *electricity generation by recycling of water* ili kuepusha kusuasua kwa uzalishaji wa umeme kutokana na upungufu wa kina cha maji kwenye vyanzo vya maji. Mfano wa teknolojia iliyotumika kwenye *The Grand Ethiopian Renaissance Dam.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa namba 14 umeonesha *projection* ya *population growth*. Tanzania katika miaka michache ijayo itakuwa na idadi kubwa ya watu. Je,

tumejiandaa katika mipango yetu kuhakikisha kuwa ongezeko hili la watu sio tegemezi na lisiwe mzigo wa Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wa Mtanzania. Je, Serikali imeandaa mikakati gani ya kuimarisha mazingira ya *Agro Business Tanzania?* Kwa mfano, kuna vyombo kama Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ambayo ni chombo cha kusaidia wakulima wanapata soko la uhakika wa mazao yao, lakini Bodi hii haijawezeshwa kibajeti kutimiza malengo. Mfano, mwingine ni Benki ya Maendeleo ya Kilimo ambayo inachangamoto ya mtaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iweke katika mipango yake namna ya kuwezesha vyombo vilivyo vya kuendeleza kilimo Tanzania. Lakini Serikali iweke mipango ya makusudi ya kuwahakikishia wakulima soko la mazao yao ili kilimo kiweze kuleta tija. Pia itoe kibali kwa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko kupata shilingi bilioni 8.9 *loan* kutoka *NSSF* na kibali cha kupata mkopo wa bilioni 6 kutoka *Azania Bank* ili Bodi ifanye kazi zake kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefikia wapi katika kuleta Muswada wa sheria itakayoanzisha *Price Stabilazation Fund*, mfuko utakaoweza kuwa suluhisho la kumlinda mkulima pale bei za mazao zinapoanguka, kwa mfano mbaazi mwaka huu?

**MHE. ZAINABU M. AMIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Philip Isdor Mpango (Mbunge) kwa kuwasilisha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2018/2019 na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu na maoni yangu katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2018/2019utakuwa katika sehemu tatu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali iweke kipaumbele katika viwanda hususani kujenga, kufufua viwanda vyetu mfano, katika Mkoa wa Morogoro kuna viwanda kama vile Canvas, Polyster, Ceramic, Magunia, Tannaries (Kiwanda cha Ngozi), Moro Shoe, Moproco. Vyote hivi vipo katika Manispaa ya Morogoro, viwanda hivi vingine vinafanyakazi na vingine wawekezaji hawaviendelezi. Hivyo Serikali isimamie na kuwapa muda wawekezaji hao kuviendeleza na wakishindwa virudishwe kwa Serikali ili wapewe wawekezaji wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda hivi vikifanyakazi kama miaka ya 1980 na 1990 vitaleta ajira kwa Watanzania pia kuongeza Pato la Taifa la Tanzania, kulipa kodi ya bidhaa zinazozalishwa kutokana na ujenzi wa reli itakayojengwa kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro (treni ya mwendokasi itaongeza chachu ya ajira ya wananchi wa Dar es Salaam, Mkoa wa Pwani na Morogoro ambao watapata ajira katika viwanda hivyo vilivyopo Mkoa wa Morogoro).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kodi, niipongeze Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* kwa kukusanya kodi kwa wafanyakazi hususani katika Miji Mikuu mfano Dar es Salaam. Nashauri katika kipaumbele kimojawapo Serikali iandae utaratibu maalum ambao utamwezesha mfanyabiashara alipe kodi kwa wakati na afurahie kuchangia Pato la Taifa na siyo Serikali iwe adui kwa mlipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iboreshe mazingira ya mwananchi wakati wa kuanza biashara. Kuna tatizo katika utaratibu uliopo, nashauri katika Mpango wa Maendeleo 2018/2019 Serikali impe muda angalau miezi mitatu *(grace period)* mwananchi anayeanzisha biashara na baada ya hapo ifanye makadirio kwa malipo ya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa mfanyabiashara anakadiriwa malipo ya kulipa kwa mwaka kabla ya kuanza biashara na sehemu kama vile Kariakoo makadiro ni makubwa mno ambayo si chini ya milioni mbili kwa mwaka, na hii hupelekea wafanyabiashara kushindwa kulipa kodi na

hatimaye kufunga biashara. Hivyo maoni yangu Serikali ipitie tena utaratibu huu kupunguza makadirio ili mwananchi aweze kumudu kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri faini wanazotozwa wafanyabiashara ambao wanakutwa na makosa, mfano ya kutotoa risiti za *EFD* ni kubwa mno shilingi milioni tatu kulinganisha na bidhaa aliyouza na hii hupelekea mwananchi kushindwa kulipa faini na hatimaye kufunga biashara zao. Pia nashauri wafanyabiashara wadogo wadogo maarufu kama wamachinga hususani waliopo katikati ya Jiji la Dar es Salaam (Kariakoo) Serikali iwasajili ili waweze kuwa na mchango kwa Pato la Taifa kwa kulipa kodi na kwenda sambamba na kauli mbiu ya Rais wetu Mheshimiwa John Pombe Magufuli ya ukiuza toa risiti na ukinunua dai risiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya afya Serikali imefanya jitihada kubwa katika kutatua matatizo mbalimbali yakiwemo kutoa madawa, vifaa tiba, ujenzi wa zahanati na vituo vya afya. Maoni yangu Hospitali ya Taifa Muhimbili ni Hospitali ya Rufaa Tanzania, wakati tunaelekea katika Mpango wa Maendeleo wa Bajeti wa mwaka 2018/2019 Serikali ijenge eneo ambalo litasaidia wananchi wanaowasindikiza wagonjwa wao kutoka katika mikoa mbalimbali Tanzania ambao hawana ndugu au jamaa Jijini Dar es Salaam, waweze kupata sehemu za kufikia baada ya kumkabidhi mgojwa wodini. Maana kuna baadhi ya wagonjwa wanahitaji huduma za karibu kutoka kwa ndugu zao ambazo wahudumu wakati mwingine ni vigumu kuzifanya. Wakati mwingine wagonjwa wanaopewa rufaa kuja Muhimbili ni watoto zaidi ya miaka 5 – 15 ambao wanahitaji huduma ya karibu ya mzazi au mlezi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naunga mkono hoja ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2018/ 2019.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mahindi ni zao la chakula na uzalishaji wake umepanda

kutokana na mwamko wa wakulima kutokana na hamasa kubwa iliyotolewa na Serikali. Pamoja na yote hayo ukulima wa mahindi leo hii ni kama adhabu kwani hakuna soko la mahindi, bei yake ni ya chini, gunia moja ni kati ya shilingi 25,000 mpaka shilingi 30,000. Je, kwa bei hiyo mkulima atamudu kununua pembejeo, mbolea, mbegu, dawa na gharama nyingine za kuendesha kilimo?

Mheshimimwa Mwenyekiti, mkulima ataendeshaje shughuli nyingine za maisha huku tukijua kuwa zao la mahindi kwa mkulima ndiyo zao la chakula na biashara. Akiugua anategemea auze mahindi, watoto kwenda shule auze mahindi, kujenga nyumba auze mahindi na kulipa michango auze mahindi. Hivyo, unapofungia mahindi yasipelekwe nje huoni kuwa ni kuwatesa wakulima wakati Serikali hainunui mahindi? Hivi Serikali inataka wakulima warudi kwenye jembe la mkono au kilimo kwa ajili ya familia tu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kilimo hakuna viwanda. Wafanyakazi wa viwandani wanahitaji kula, viwanda vinahitaji malighafi inayotokana na kilimo. Hata bidhaa itakayozalishwa viwandani lazima soko la kwanza liwe wananchi wenyewe. Je, watanunuaje bidhaa kama hawana fedha kwa sababu Serikali imewafanya wawe maskini kwa kutonunua mazao yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, itakuwa ni vizuri wananchi wote wanaolima wahamie kulima korosho? Wakulima waache kulima mzao ya chakula wote wahamie migodini kuchimba madini? Wananchi wa Tanzania wataweza kununua chakula nje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Kilimo akumbuke maneno yafuatayo ya Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli, alisema:-

1. Mkulima asinyanyaswe.

2. Mkulima asipangiwe bei ya mazao yake hukumsaidia kulima.

3. Hata kama utanunua debe moja la mahindi kwa ng'ombe watatu ni sawa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais huyu anajua shida ya wakulima cha ajabu Waziri wake anakwenda kinyume na bosi wake. Kwa hali hiyo viongozi tumuelewe Mheshimiwa Rais wetu, tusimchonganishe na wananchi (wakulima).

Mheshimiwa Mwenyekiti, zuio la kuuza nje lina tafsiri kama ifuatavyo:-

(i) Unapomzuia mkulima asiuze mazao yake (mahindi) nje wakati na wewe hununui maana yake ni kumpangia bei wakati hukumsaidia kulima.

(ii) Unaposema wafanyabiashara wakanunue mahindi na kupeleka mikoa isiyo na chakula, je, huyo mfanyabiashara umempatia fedha za kwenda kununua hayo mahindi kiasi kwamba uwe na uhuru wa kumpangia bei ya kwenda kununua hayo mahindi? Je, hao wafanyabiashara utawatafutia soko zuri la kurudisha gharama zao ili wapate faida?

(iii) Unaposema kuuza chakula nje kwa maana ya mahindi/mchele mpaka wa-*process* wauze unga na mchele. Je, wakulima hao wameandaliwa kuwa na uwezo huo kwa sasa?

(iv) Unaposema wakulima hao kuuza nje wa-*process* wauze unga/mchele, je, wakulima wetu wamefikia kiwango hicho? Je, ni kila sehemu kwa sasa kumefikiwa na umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimwambie Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ni uungwana sana ukiaminiwa na Rais tenda haki kwa watu wake na ukiona ngoma ni nzito siyo vibaya kuachia ngazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu afya, nashauri kuwe na mpango wa kumalizia maboma ya majengo ya zahanati

na vituo vya afya ambavyo tayari wananchi wametoa nguvu kujenga maboma hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango haujaonesha kununua magari ya wagonjwa kwa vituo vya afya ambavyo bado. Mfano, Kituo cha Afya Milepa na Laela katika Jimbo la Kwela - Sumbawanga Vijijini havina magari ya kubebea wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umeme, Mpango ueleze juhudi za makusudi kuhakikisha kila kijiji/kitongoji kinapata umeme. Mfano, Jimbo la Kwela lipo nyuma halijapata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa barabara, naishukuru Serikali kwa kuanza ujenzi wa Daraja la Mto Momba. Naomba baada ya daraja kukamilika ianze ujenzi wa barabara ya Kasansa - Kilyamatundu - Kamsamba - Mlowo kwa kiwango cha lami.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Waziri Mpango pamoja na timu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapozungumzia mapinduzi ya viwanda pia hutoacha kuzungumzia mapinduzi ya kilimo. Niishauri Serikali yangu ipeleke wataalam wa kutosha katika sekta nzima ya kilimo kama Maafisa Ugani pamoja na Maafisa Maendeleo ya Jamii washirikiane kuhakikisha kuwa wanatoa elimu yenye tija kwa wakulima wetu pamoja na Serikali kupeleka pembejeo na mitaji kwa walengwa ambao ni wakulima kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote haya ni kutaka kuboresha kilimo chetu ili kuwezesha malighafi nyingi zitoke kwenye kilimo ambazo zitatumika katika viwanda vyetu kuliko kutegemea malighafi kutoka nje. Pia katika viwanda vyetu Serikali ihakikishe inasimamia viwanda vyetu vizalishe bidhaa bora zenye viwango kuhakikisha tunashindana na ubora wa masoko ya ndani na nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ndiyo njia kuu pekee ya kiuchumi. Kwa hiyo, niishauri Serikali yangu Tukufu ipeleke fedha za kutosha na kuhakikisha barabara zinaunganisha Mikoa hadi Mikoa na Wilaya hadi Wilaya. Pamoja na barabara hizi muhimu ambazo ndiyo zinazotoa malighafi kutoka vijijini, Serikali ipeleke pesa za kutosha na kuwa na usimamiaji wa karibu kwa kuhakikisha zinapatikana kwa mwaka mzima kuliko ilivyo sasa hasa barabara za Jimbo la Lushoto zimeharibika sana. Kwa hiyo, niiombe Serikali katika Mpango wake huu iangalie kwa jicho la huruma barabara za Lushoto ili wakulima wetu mazao yao yasiozee shambani kama ilivyokuwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila afya hakutakuwa na maendeleo katika sekta zote hapa nchini. Wananchi wengi wameitikia wito wa kujitolea kujenga zahanati pamoja na vituo vya afya, lakini Serikali haipeleki mafungu kwa ajili ya kumalizia majengo hayo. Niishauri Serikali yangu ipeleke pesa za kutosha ili majengo yale yaweze kukamilika na Watanzania waweze kupata afya njema na kuweza kulitumikia Taifa lao. Hii iende sambamba na kupeleka vifaa vyote vya afya ili kupunguza mlundikano mkubwa katika hospitali zetu za Mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ndiyo kila kitu katika maisha ya binadamu. Kwa hiyo, niiombe Serikali katika Mpango wake huu wa mwaka 2018/2019 ihakikishe inamalizia maabara zote ambazo zimeanza kujengwa bila kumaliziwa pamoja na kuongeza vyumba vya madarasa, kujenga vyoo pamoja na kujenga nyumba za walimu na elimu hii iendane na kujenga vyuo vya *VETA* kila Wilaya. Wilaya ya Lushoto tokea mkoloni hakujawahi kujengwa Chuo cha *VETA*. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Mpango katika awamu hii naomba utenge pesa za kujenga Chuo cha *VETA* katika Wilaya ya Lushoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia mazingira tuwe tunahakikisha tunapanda miti nchi nzima pamoja na kusimamia sheria kikamilifu ili wananchi wetu wawe wanatunza vyanzo vyetu vya maji na Serikali ihakikishe inawawezesha wananchi kwa kuwapatia miche ili wapande

katika mashamba yao. Kwa mfano, katika Jimbo la Lushoto kuna misitu imeungua moto lakini kuna kikundi cha vijana kinaitwa *Friends of Usambara* mpaka sasa kina miche zaidi ya milioni 10 na wao wenyewe wameamua kupanda miti katika maeneo yote ya misitu yaliyoungua. Kwa hiyo, niishauri Serikali iweze kusaidia vikundi kama hivi ambavyo vipo hapa nchini na vikundi hivi ikisimamiwa vizuri tutarudisha uoto wetu wa asili uliopotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyoanzishwa *TARURA,* niishauri Serikali ije na mpango wa kuanzisha pia wa Wakala wa Maji Vijijini na Serikali ipeleke kwa wakati umeme vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 *(The Public Finance Act, 2001 No.4)* inaitaka Serikali kuleta Bungeni bajeti ya nyongeza kwa ajili ya kupata idhini ya Bunge ikiwa fedha za awali hazikutosha. Kwa sasa kuna baadhi ya miradi ya maendeleo inatekelezwa nje ya bajeti na hatujaona Serikali ikiomba bajeti ya nyongeza, mfano, ujenzi wa mabweni ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ujenzi wa barabara za juu Dar es Salaam, ni baadhi tu. Kitendo cha Serikali kuamua kufanya matumizi bila kupata idhini ya Bunge ni uvunjaji wa Katiba na sheria na kitendo hicho kinaweza kuruhusu mianya ya rushwa na ubadhirifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mikopo ya elimu ya juu, katika mwaka wa fedha 2016/2017 wanafunzi waliopata mikopo walikuwa 20,183 na wanafunzi takribani 27,053 walikosa mikopo. Mheshimiwa Rais katika kampeni za mwaka 2015 alisema yeye atakuwa muarobaini wa mikopo ya elimu ya juu. Utolewaji wa mikopo umekuwa na ubaguzi na usumbufu mkubwa, ni vyema Serikali katika Mpango wake iweke *commitment* ya kuandaa mfumo bora wa utoaji mikopo ili kuondokana na tatizo hili. Vilevile kumekuwa na tatizo au hakuna mfumo mzuri wa urejeshaji mikopo kwani sheria iliyopo inawaumiza sana waliopo katika ajira kukatwa

asilimia kubwa kulingana na kipato wanachopata na kushindwa kuhimili maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haionyeshi uwezo katika kuziwezesha sekta binafsi kukua ili ziweze kuipunguzia Serikali mzigo wa walio wengi kukosa ajira. Wafanyabiashara walio wengi wamefunga biashara zao au kupunguza wafanyakazi kutokana na kushindwa kumudu gharama za uendeshaji, kushuka kwa mapato kwa baadhi ya makampuni, mfano, viwanda vya vinywaji, makampuni ya kitalii, nyumba za starehe zikiwemo baa na hoteli. Mfumo huu unaangamiza kabisa sekta binafsi. Sekta binafsi ndiyo inayochangia mapato ya Serikali kupitia kodi inayokusanywa kwa bidhaa na waajiriwa. Vilevile kumekuwa na tabia ya kuwatishia wafanyabiashara kufunga makampuni kiholela, hii inaongeza umaskini kwa Watanzania walio wengi. Hivyo, nashauri Mpango huu uzingatie na uweke kipaumbele katika kuwezesha sekta binafsi kufanya kazi bila bughudha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa viwanda, kama Tanzania ya viwanda ni uhalisia na siyo ndoto basi suala hili lisingekuwa ni la matamko kwani hivi karibuni Waziri wa TAMISEMI amenukuliwa na vyombo vya habari akieleza kuwa kila mkoa kujenga viwanda 100 ambapo hadi Desemba, 2018 katika Mikoa yote Tanzania Bara inatakiwa kuwa na viwanda 2,600. Kama miaka yote iliyopita imeshindikana kufufua tu viwanda vilivyokuwepo hii leo ya mwaka mmoja itawezekana? Kwa Mkoa wangu wa Iringa tu kulikuwa na viwanda vifuatavyo:-

1. Kiwanda cha Vifaa vya Nyumbani kama masufuria kiliitwa *IMAC;*

2. Kiwanda cha Nyuzi na Nguo *(COTEX);*

3. TANCUT Almasi;

4. Kiwanda cha Magurudumu ya Magari *(VACULUG);*

5. Kiwanda cha Tumbaku;

6. Kiwanda cha Coca cola; na

7. *SIDO*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyote hivyo havipo tena. Maelekezo hayo ya viwanda 100 yanashangaza kwa sababu kama mikopo kwa sekta binafsi imepungua na kama Serikali haifanyi biashara hivyo viwanda vitajengwa na nani? Serikali inabidi ijipambanue ili kujua mfumo upi inaufuata kama ni uchumi wa kijamaa au uchumi wa kibepari au soko huria ili ijikite madhubuti katika mfumo itakaoamua kuufuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ndicho kinachotoa ajira kwa Watanzania zaidi ya asilimia 70. Katika Mpango huu bado sekta hii inaendelea kupuuzwa na matokeo yake ni kudorora kwa uchumi na hiyo Tanzania ya viwanda inaendelea kuwa ndoto. Kuna changamoto kwenye kilimo kwani wakulima hawapati pembejeo kwa wakati, kilimo cha umwagiliaji hakitiliwi mkazo, Maafisa Ugani hawako wa kutosha, baadhi ya mabenki kutokopesha wakulima kwa madai kwamba mikopo katika sekta ya kilimo huwa haina uhakika wa kurudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango huu Serikali inatakiwa kubuni utaratibu maalum wa kuziwezesha benki za biashara kuweza kutoa mikopo hiyo. Wanawake na vijana wakiwezeshwa hasa katika mikopo ya kilimo na ufugaji ukosefu wa ajira utapungua.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango wangu kwa kuzungumza nina mawazo katika kuimarisha sekta ya sukari kutokana na *potential* ya soko la ndani na nje. Mfano sisi tunaagiza sukari yenye thamani dola za Kimarekani milioni 60.9 (shilingi bilioni 123 za Kitanzania), majirani zetu kama Angola ambao ni *member* wa *SADC* wanaagiza sukari kwa thamani ya dola za Kimarekani milioni 161.1, Ethiopia dola za Kimarekani milioni 188, haya ni masoko wazi lakini ili tuyafaidi. Pamoja na mradi wa Mkulazi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, tufikirie kuwezesha wawekezaji wa ndani kupitia benki za *TIB* na ile ya kilimo *TAB*

ambayo mpaka sasa ina *around* shilingi bilioni 164 lakini imekopesha shilingi bilioni 3.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwekeza kiwanda cha kuzalisha tani 150,000 inahitaji wastani wa dola za Kimarekani milioni 80 bila kujenga *facilities* nyingine. Pamoja na mashamba utahitaji jumla ya dola za Kimarekani milioni 150, hapo tayari una miundombinu ya nishati na barabara. Sasa kumbe tutumie mfumo wa *small scale growers* ambapo tunakuwa na *factory* nyingi maeneo mbalimbali kwa kushirikiana na Halmashauri na sekta binafsi. Maeneo *potential* ya kuzalisha sukari ni pamoja na Bagamoyo tani 120,000; Mkulazi tani 200,000; Ruipa tani 60,000*;* Rufiji tani 60,000*;* Kasulu tani 30,000 na Mkongo – Mara tani 30,000*,* jumla tani 500,000*.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida ya kutumia *small scale sugar plants* ni kama ifuatavyo:-

(i) Inahitaji eneo dogo kama *five acres.*

(ii) Inahitaji kama shamba la miwa la ekari 3,000 ili kulisha kiwanda.

(iii) Inapunguza gharama za kusafirisha miwa kwenda kiwandani mfano leo hii pale Kilombero kuna miwa inasafirishwa umbali hadi wa kilometa 60 lakini ikiwa ndani ya shamba la eka 3,000 huwezi kuwa na gharama kubwa ya kusafirisha.

(iv) Inachukua wastani wa miezi kumi kujenga kiwanda cha *small scale.*

(v) Inahitaji mwaka mmoja kuwaendeleza wakulima wadogo *(small scale farms).*

(vi) Ina *promotes* ushiriki wa *small holder farmers.*

(vii) Ni rahisi kutoa *extension service* na pia mwekezaji hahitaji kugombania ardhi maana yeye atasaidia *small holder*

kwa mbegu na pia huduma nyingine muhimu kuwezesha kupata miwa yenye *content* kubwa ya sukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muundo huu umewasaidia sana Brazil ambao wanazalisha 20% ya sukari (tani milioni 36) na wanahodhi 40% ya soko la dunia. Hivyo, *potential* ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee Benki ya Kilimo. Nimeona juzi hapa benki ikiwa imepata fedha zaidi. Hata hivyo, kuna matatizo makubwa kwenye hii benki kuanzia Mtendaji Mkuu mpaka Bodi. Mfano, hivi *Zanzibar State Trading Corporation (ZSTC)* waliomba mkopo wa shilingi bilioni 10 ili wanunue karafuu, Bodi ikapitisha lakini kwa uzembe wa Mtendaji Mkuu mkopo ukacheleweshwa, msimu ukapita baadaye *ZSTC* wakaukataa mkopo. Tujiulize *with a capital of over 164 billion, how come* wametoa mkopo wa *less than five billion? And this is a bank* na *main core/function of the bank* ni kukopesha. Mliangalie hili jambo ili benki hii iwe nyenzo kuelekea uchumi wa viwnada. Ahsante.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na kauli mbiu ya Serikali ya viwanda ni vyema tukaboresha Benki ya Kilimo na kuifikisha mikoani ili wakulima waweze kukopesheka ili waweze kujikomboa kimaisha na kufikia malengo ya viwanda katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu soko la uhakika la mazao, kutokana na nchi yetu kuwa na idadi kubwa ya wananchi ambao ni wakulima wamejikita kwenye kilimo cha mazao ya chakula na mazao ya biashara ambayo yamekosa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta binafsi, Serikali inapaswa kushirikisha sekta hii katika taratibu za kukuza uchumi katika nchi yetu ili waweze kuwa mfano na wengine waweze kuwekeza katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ya maliasili na utalii, kulingana na umuhimu wa sekta hii ya utalii ni muhimu ikatazamwa kwa umakini mkubwa kwani tukiwekeza kwa

kufanya tafiti za kutosha tutaweza kupata fedha nyingi za kigeni kwa kutengeneza mazingira rafiki kwa watalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya kilimo ipewe kipaumbele katika shughuli zote za maendeleo kwa kuwawezesha wakulima kwa kuwapa pembejeo, mtaji na elimu ya kuachana na kilimo cha mazoea badala yake kiwe cha kisasa. Kuhusu kilimo cha umwagiliaji, Serikali ijielekeze kwenye kilimo cha umwagiliaji ili kuelekea kwenye nchi ya viwanda kuepuka kilimo cha msimu ambacho hakitabiriki na kinaweza kisifikie malengo ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa sekta ya madini, kulingana na umuhimu wa viwanda ni vyema Serikali ikawekeza kwenye utafiti ili wanavyuo wanapomaliza masomo yao waweze kusaidia Taifa la Tanzania kwa upande wa madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Deni la Taifa, ni vyema kama Taifa tukawa na utaratibu wa kukopa mikopo ambayo haiwezi kuwatesa Watanzania wote. Tutaweza kuepuka kero hiyo kwa kukopa kwa wazabuni wa ndani ambayo haitakuwa na kero kubwa.

**MH. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze uwasilishaji wa Kamati ya Bunge na Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali kuwaangalia kwa jicho la huruma wajasiriamali wadogo kama wasindikaji ambao wanakutana na pingamizi kubwa na kukatishwa tamaa na Taasisi za Serikali za Udhibiti. Mfano, *TFDA* imekuwa chanzo cha wajasiriamali kukata tamaa kwani *TFDA* wanatoza fedha nyingi sana kwa kila *product/* bidhaa inayotengenezwa. Pia suala la *TFDA* kutoza kwa dola imekuwa kikwazo kikubwa na inarudisha nyuma zoezi zima la wajasiriamali kukua. *TFDA* inatoza dola 2.5 mpaka 500 kwa bidhaa ambayo mtengenezaji anaiuza kwa shilingi za Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iangalie jinsi ya kupunguza urasimu kwenye usajili wa biashara kwani urasimu ni mkubwa unapelekea watu wengi kukata tamaa kwa mfano wawekezaji toka nje wanalalamikia sana kuhusu usajili hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali juu ya kodi kwa wafanyabiashara wanaoanza biashara kutozwa kodi kabla ya biashara kuanza. Sheria ya mlipa kodi inatozwa kwa kuangalia pato la biashara na si mtaji hivyo inasababisha watu wengi kushindwa biashara kwani hawana *grace period* ya biashara kama wageni wanavyopewa fursa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kuwa na vipaumbele kwenye mipango yake kwani Serikali ikiwa na vipaumbele vichache vinavyotekelezeka itasaidia kuwezesha nchi kuondokana na utegemezi au kuongeza Pato la Taifa kuliko ilivyo sasa ambapo vipaumbele ni vingi kiasi kwamba utekelezaji unashindikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali katika Mpango wake wa viwanda iimarishe kilimo ambako malighafi zitatoka. Serikali iboreshe tafiti za kilimo na watoe elimu ya kilimo ili wananchi wajue kilimo cha kisasa chenye tija na si kilimo cha mlo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kuangalia hili suala la masoko kwa mazao, soko la ndani na la nje. Mpaka sasa wananchi wamekata tamaa ya kilimo baada ya Serikali kushindwa kununua mazao yao pia sheria ya kukataza wakulima kujitafutia masoko. Wakulima wengi wamekata mitaji baada ya kulima na kukosa masoko na mazao yao kuishia kuharibika. Pembejeo nazo ni tatizo, hazifiki kwa wakati hivyo kupishana na msimu wa kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali kuweka viwanda vya kuchakata bidhaa zitokanazo na mifugo ikiwa ni pamoja na ngozi, maziwa, nyama kwani Tanzania ina mifugo mingi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano na nafasi za Wabunge zimeshafungwa sasa tunarudi kwenye majibu ya Serikali. Tunaanza na Mheshimiwa Nyongo ajiandae Mheshimiwa Nditiye, ajiandae Mheshimiwa *Engineer* Kamwelwe.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi kwa upande wa Serikali basi tuanze kutoa maelezo kwa upande huu.

Kwanza kabisa nipende kushukuru kwamba Waheshimiwa Wabunge wengi wametoa mawazo mengi tofauti katika kuchangia huu mpango wa mwaka. Mawazo ni mengi na nashukuru mawazo mengi ni mazuri lakini na mimi kwa kujikita kwa upande wa madini kulikuwa kuna mawazo machache kwa Wabunge ambayo waliyatoa hasa walijikita katika upande huu wa madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kabla sijajibu hoja hizo awali ya yote nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya. Tumeona anafanya mambo mengi ambayo kwa kweli yalikuwa hayana majibu, lakini kwa uwezo wake Mheshimiwa Rais na uzalendo wake ameonesha dhahiri kwamba ana nia thabiti na ya dhati kuhakikisha kwamba analinda rasilimali ya nchi yetu, anahakikisha kwamba rasilimali ya nchi yetu inakuwa na tija kwa uchumi wa nchi yetu. Kwa hilo Mheshimiwa Rais tunampongeza sana kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuanzisha hii Wizara mpya ya Madini. Wizara hii ilikuwa imeungana na Wizara ya Nishati na Madini na ukitazama ni kwamba tunatambua kwamba madini ni sekta nyeti, ni sekta ambayo ina mchango mkubwa katika uchumi wa nchi yetu. Hivyo Mheshimiwa Rais aliniteua mimi na Mheshimiwa Angellah Kairuki tuweze kuongoza Wizara hii lakini ukitazama kwa kina ni kwamba Mheshimiwa Rais alitaka tija katika Wizara hii ya Madini. Wizara hii imeundwa kwa maana ya kwamba tuongeze *efficiency* ya kusimamia rasilimali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua mchango wa uchumi katika nchi yetu rasilimali ya madini ilikuwa inachangia kiwango kidogo sana, asilimia 3.7 lakini sasa hivi kwa juhudi zake Mheshimiwa Rais ni kwamba sekta ya madini inachangia zaidi ya asilimia 4.3 katika uchumi wa nchi yetu. Hivyo basi mimi na mwenzangu tuna kazi kubwa kwa kushirikiana na wataalam wa Wizara ya Madini kuhakikisha kwamba tunaongeza tija kupitia hii sekta ya madini kuhakikisha kwamba uchumi wetu unaimarika na tunakwenda kuimarisha uchumi kwa maana ya kwamba tunakwenda kupandisha kiwango hicho kilichopo cha asilimia 4.3 na kwenda mbele zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na tumefanya mabadiliko yake ambayo ni ya mwaka 2017. Mabaadiliko haya ni makubwa lakini yalitazama sana katika sehemu nne ambazo ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kwanza ilikuwa ni kuua ile *Tanzania Mineral Auditing Agency (TMAA)* na jambo la pili lilikuwa ni kuunda Tume ya Madini ambayo mpaka sasa kama Wizara tupo katika kufanya *restructuring* kwa maana ya kuitengeneza hii Tume na kuianzisha ili sasa Tume hii iweze kusimamia sekta ya madini inavyostahili, kwa maana ya kutoa leseni, kusimamia ku-*regulate* sheria na kanuni za masuala ya madini ili kusudi madini yetu yaweze kuongeza tija katika uchumi wa nchi yetu. Kwa hiyo, kwa muda mfupi ujao, nadhani hadi kufikia mwisho wa mwaka huu Tume hiyo itakuwa tayari na itakuwa imeanza kazi kuhakikisha kwamba inasimamia vizuri sekta hii ya madini na tuweze kupata tija kutokana na madini ambayo tunachimba nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ya sheria hii ilikuwa ni sehemu ya kuongeza kodi ya *royalty (*mrabaha), kutoka asilimia nne kwenda asilimia sita na kutoka asilimia tano kwenda asilimia sita kwenye madini ya vito na madini ya *metallic.* Vilevile kuongeza gharama au kuongeza kodi ya *clearance* ambayo ni asilimia moja. Mchakato huu hata kabla ya kuanzisha Tume hiyo, umeshaanza, sasa hivi

wachimbaji wanalipa *royalty* asilimia sita. Hii ni hatua kubwa, ni hatua nzuri ambayo itatuongezea kipato katika mrabaha na Serikali itaweza kuneemeka zaidi na madini haya tofauti na ilivyokuwa kipindi cha mwanzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndiyo mambo ya mwanzo, naweza kusema ni utangulizi kwa ujumla wake. Ninapenda kusema na niwaeleze Watanzania kwamba, tunakwenda kudhibiti utoroshaji wa madini kwa kuunda Tume hii na marekebisho ya sheria. Tunakwenda kuhakikisha kwamba, madini yetu tena hayatoroshwi, hayapiti njia za panya, hayapiti njia zisizo sahihi, tunataka kwamba wachimbaji wote wapitie utaratibu unaostahili ili waweze kulipa kodi zote kwa *TRA* na vilevile waweze kulipa mrabaha ili Serikali iweze kupata kipato chake ambacho kinastahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushahidi umeonesha Mheshimiwa Rais, tarehe 20 Septemba, 2017 alipokuwa Mererani, alitoa amri ya kujenga ukuta unaozuia yale maeneo yote ya machimbo ya *Tanzanite.* Ujenzi huo umeanza toka tarehe Sita mwezi huu na ujenzi huo unakwenda kwa kasi ya hali ya juu. Jeshi letu la JKT liko *site* linafanya kazi ya *construction* na kwa hali iliyopo sasahivi ni kwamba, kuna wanajeshi pale wa kutoka JKT zaidi ya 2,000 na wanafanya kazi hiyo na wataifanya kazi hiyo kwa mkataba unavyosema, watafanya kazi ndani ya miezi sita na fedha za ujenzi wa ukuta huo wamekwishapewa asilimia 80. Kwa hiyo, tuna hakika kwamba ukuta ule utajengwa na tutadhibiti utoroshaji wa madini kutoka eneo la Mererani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Mheshimiwa Rais alitoa amri ya kwamba, tujenge mnada ambao utakuwa ni Mererani ambao mnada huu utatumika kwa watu wanaokuja kununua madini ya Tanzanite katika Mnada wa Mererani. Hapa tunavyozungumza pale Mererani tumeshapata eneo la *EPZA* ambalo shilingi bilioni 2.2 imetolewa kwa ajili ya ujenzi wa haraka wa mnada ule, ukishakamilika ujenzi ule kwa muda mfupi ujao, basi mnada ule utafunguliwa, madini ya Tanzanite, maonesho ya madini, wanunuzi watakuja pale

watanunua na watalipa mrabaha, watalipa ili tuweze kupata kipato chetu kama kinavyostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika michango mbalimbali kuhusiana na utoroshaji wa madini hata sheria inasema, sasa hivi tuna wataalam wazuri, wathaminishaji wa madini yetu. Ukiangalia kwenye upande wa Almasi tuna wataalam wazuri, mfano mzuri ni juzi tu hawa *Wiliamson Diamond Limited (WDL)* waliweza kuzalisha Almasi. Almasi ile katika kutolewa kuisafirisha Serikali kwa juhudi zake ilikamata na kuangalia, kulinganisha uthaminishaji wa mwanzo na wa pili, tukakuta thamani ya Almasi zile ni kubwa, Serikali ikazuia uuzaji wa zile Almasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *WDL* waliendelea kuzalisha. Walizalisha tena *carat* 39,000 na zikathaminishwa kwa kiasi cha shilingi bilioni nane na wataalam wetu, lakini kupeleka Almasi ile kwenye soko la Almasi, soko la mnada la Antwerp, kwa mara ya kwanza tumeweza kuuza Almasi yetu kwa njia ya mnada kwa dola za Marekani bilioni 10. Hii ni hatua kubwa ambayo Serikali imechukua na ni ya kumpa moyo Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya. Kwa kweli hiyo ni hatua kubwa na Mheshimiwa Mwenyekiti na wewe ni shahidi unalielewa hili. Kwa kweli, utoroshaji wa Almasi ulikuwa ni wa hali ya juu, lakini kwa namna tunavyokwenda tunakwenda kudhibiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa yako katika ule mzigo wa pili uliokwenda kuuzwa kwa dola milioni 10, ndani ya almasi zile ilikuwepo almasi adimu ambayo inapatikana Tanzania ambayo tunasema inaitwa *pink diamond,* iliuzwa kwa dola milioni mbili, kipande kimoja tu chenye *carat* tano. Kwa hiyo, tunaweza tukaona kwamba, kumbe tulikuwa na *pink diamonds* nyingi ambazo zinakwenda bila kuwa *recorded* katika zile takwimu ambazo zilikuwa zinaandikwa, kwa hiyo, hiyo ni hatua kubwa tumeweza kufikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunaendelea na hatua za ku-*control* utoroshaji wa madini. Juzi tumekamata kilo nne za dhahabu katika Bandari ya Zanzibar, tumezikamata

dhahabu ambazo zina thamani ya milioni 500. Tunaendelea kuimarisha ulinzi mipakani kuhakikisha kwamba utoroshaji wa dhahabu unasimamishwa, lakini wakati huo huo Serikali ina juhudi ya kuanzisha minada mitano mikubwa ambayo itakuwa inauza dhahabu. Tutauza dhahabu kwa njia ya wazi ili watu waje wanunue dhahabu na waweze kulipa ushuru, waweze kulipa na mrabaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile minada yetu hii tunatakiwa tuitengenezee miundombinu mizuri kwa maana ya usalama, miundombinu ya umeme, miundombinu ya maji, miundombinu ya usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mjadala uliokuwa unaendelea watu wamepiga sana kelele kuhusu kutengeneza Uwanja wa Ndege Chato. Kule Chato tunahitaji usafirishaji wa madini yetu, tunahitaji kusafirisha watu, tunahitaji kusafirisha vifaa, uwanja wa ndege wa Chato ni muhimu sana kujenga pale Chato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda pale Bulyanhulu wana uwanja wa ndege. Wale mabwana wamejenga uwanja wao wa ndege wa kuweza kusafirisha bidhaa zao, Kwa nini Serikali tusiwe na uwanja wetu? Kwa nini Serikali tusiweke uwanja wa kisasa wa kuweza kusafirisha bidhaa zetu za madini kupitia uwanja wa Chato? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wameongelea kuhusu umbali wa kutoka Mwanza. Kutoka Mwanza hadi Geita ni kilometa 185, kutoka Geita kwenda Chato ni zaidi ya kilometa 120. Kwa hiyo ni kilometa 120 na hizo 180 ni zaidi ya kilometa 300 kutoka uwanja wa ndege wa Mwanza, hapa katikati usafirishaji wa dhahabu ni hatari sana kusafirisha dhahabu umbali wa zaidi ya kilometa 300.

Kwa hiyo, uwanja wa Chato ni muhimu kuuweka pale na hii ni kwa manufaa ya Watanzania wote na wala sio kwa manufaa ya watu wachache kama wenzetu walivyokuwa wakieleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nditiye, ajiandae Mheshimiwa Injinia Kamwelwe.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa jitihada zake mbalimbali za kuisogeza nchi yetu katika uchumi wa kati. Nampongeza vilevile Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Mpango, kwa mpango mzuri sana aliouleta, ambao ni mpango endelevu kwa ajili ya Serikali, unaolenga Mpango wa Serikali wa miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii vilevile kuwashukuru wachangiaji mbalimbali Waheshimiwa Wabunge waliochangia Mpango huu kwa nia njema kabisa, lakini niwashukuru kipekee wale waliochangia kwenye sekta ya ujenzi, uchukuzi na mawasiliano.

Mheshimwa Mwenyekiti, kipekee kabisa napenda niongelee masuala makuu manne, nitaongelea masuala ya reli, nitaongelea masuala ya barabara, nitaongelea masuala ya bandari na mwisho nitagusia kidogo masuala ya viwanja vya ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango mkubwa sana wa ujenzi wa reli mpya kwa kiwango cha *standard gauge,* kila Mbunge anajua na kila mwananchi anafahamu. Serikali ya Awamu ya Tano inatarajia kujenga jumla ya kilometa 4,886 ambazo kiujumla kabisa zitajumuisha kanda kuu tatu, tutakuwa na Ukanda wa Kati ambao utajumuisha mikoa ya Dar es Salaam, Isaka, Mwanza ambayo ni kilometa 1,219 lakini vilevile tutakuwa na Ukanda

wa Kaskazini ambao tutakuwa na reli ya kutoka Tanga, itapita Arusha mpaka Musoma, hizo ni kilometa 1,233 na vilevile tutakuwa na Ukanda wa Kusini ambao ni wa kilometa 1,092 ambao utatoka Mtwara – Mbamba Bay na matawi yake ambayo ni ya Liganga na Mchuchuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia na reli ya kati, tumeshaanza ujenzi wa kiwango cha *standard gauge* kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro, kilometa 300 ambazo zitajumlisha njia ya reli ya kawaida pamoja na *trunks* zake na *sliding,* mkandarasi mpaka sasahivi yuko *site* anaendelea na kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekwishapata mkandarasi vilevile kwa ajili ya kipande cha Morogoro mpaka Makutupora kilometa 422 sasa hivi yuko kwenye *mobilization,* wakati wowote ule ataanza kazi, sehemu nyingine zote zinaendelea na utaratibu wa upembuzi yakinifu na taratibu nyingine kwa ajili ya ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya gharama itakayotumika kwa ajili ya mradi huu wa *standard gauge* kwa nchi yetu itakuwa ni dola za Kimarekani bilioni 3.17. Tunategemea itakapokwisha itakuwa na uwezo wa kwenda *speed* ya kilometa 160 kwa saa, vilevile itabeba tani milioni 17 kwa mwaka. Hiyo ni miradi kwa upande wa reli ambayo inaendelea na tumeona jitihada za Serikali katika kuhakikisha kwamba hiyo reli inajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa bandari tulikuwa na wachangiaji kadhaa ambao walizungumzia sana masuala ya bandari. Serikali imekuwa na mpango mzuri sana wa kuboresha bandari yetu kwanza ya Dar es Salaam kwa geti namba moja mpaka geti namba saba, ambapo moja ya shughuli zitakazofanyika itakuwa ni kuongeza kina cha bandari kwa mita 15 *deep sea,* halafu kuna sehemu ya meli kugeuzia na yenyewe inapanuliwa kwa kiwango kizuri kabisa cha kimataifa, vilevile tunaongeza sehemu ya *dragging and channel.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Bandari ya Dar es Salaam itaenda kuboreshwa kwa kipindi kifupi kinachokuja kuhakikisha kwamba inaweza kuhudumia meli nyingi kwa wakati mmoja kwa kiwango cha kimataifa na gharama zitakazohusika katika mradi huo ni shilingi za Kitanzania bilioni 335.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuna uboreshaji wa Bandari ya Mtwara ambapo zimetengwa jumla ya shilingi za Kitanzania bilioni 186. Tunatengeneza gati mpya pale kwa ajili ya kufungua lango la Kusini kusafirisha na kupokea mizigo. Tunajua jinsi ambavyo kuna mabadiliko makubwa sana katika Ukanda wetu wa Kusini, kuna viwanda vinaanzishwa vikubwa, tunategemea tuweze kupata mizigo ya kutosha kwa ajili ya kuhudumia bandari ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Mamlaka ya Bandari Tanzania inaendelea kulipa fidia kwa wananchi kwa ajili ya ujenzi wa bandari mpya ya Bagamoyo baada ya malipo kukamilika tunategemea kwamba ardhi itakayokuwa imepatikana sasa atapewa mwekezaji ambaye tunaendelea na mawasiliano naye kwa ajili ya kujenga bandari hiyo ambayo itasaidia sana katika kufungua lango upande wa Mashariki wa nchi yetu. Ni matumaini yetu kwamba, wananchi ambao wako maeneo ya Bagamoyo ambayo yako karibu na sehemu tutakakojenga bandari watatoa ushirikiano wa hali ya juu kwa Serikali kuhakikisha kwamba tunapata eneo hilo kwa ajili ya kujenga bandari mpya pale Bagamoyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuna suala la viwanja vya ndege. Ni kweli kwamba Serikali imenunua jumla ya ndege sita, tunazo *Bombadier Q400* ziko tatu ambazo zina uwezo wa kubeba abiria 76 na ndege mbili tayari ziko hapa nchini na moja itakuja hivi karibuni. Tunayo ndege ya *Q Series* au *Q300* ambayo inabeba abiria 150 mpaka 176 na yenyewe iko kwenye hatua za mwisho kabla haijaja nchini na tumekwishafanya malipo ya mwanzo kwa ajili ya kupata *Boeing 787* ambayo itakuwa na uwezo wa kubeba abiria 262. Ndege hizo zote ni kwa ajili ya kurahisisha huduma ya

usafiri kwa njia ya anga ili nchi yetu iweze kupata maendeleo yanayotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali imeendelea kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya upanuzi wa viwanja mbalimbali hapa nchini. Tuna viwanja 11 ambavyo tayari matengenezo yameshaanza kwa ajili ya kuvipanua, kupanua *run ways,* kuna sehemu kwa ajili ya *apron,* kwa ajili ya sehemu za kugeuzia ndege na ku-*park,* lakini vilevile tumeendelea kujenga majengo ya abiria kwa ajili ya kuhudumia abiria wanaofika kwenye viwanja hivyo husika vya ndege. Kwa kutaja tu, kuna uwanja wa ndege wa Kigoma tumeshatangaza *tender* kwa ajili ya kutafuta mkandarasi wa kupanua uwanja huo, kuna uwanja wa ndege wa Sumbawanga tumeshatangaza *tender* vilevile, kuna viwanja vingine mbalimbali kama Mbeya, Tabora na uwanja wa ndege wa Geita. Kwa hiyo, kuna maendeleo makubwa ambayo Serikali inayafanya kwa ajili ya kuhakikisha kwamba viwanja vyetu vinakuwa vya ubora wa kisasa kabisa kwa ajili ya kuhudumia abiria mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongelea kwa haraka tu upande wa barabara. Waheshimiwa Wabunge wote wanaelewa wazi kwamba kuna miradi mikubwa tunaendelea nayo ya ujenzi wa barabara. Kuna barabara ya *TAZARA flyovers* inaendelea, mkandarasi yuko pale na tunategemea muda sio mrefu barabara itakuwa iko tayari kwa ajili ya matumizi, vilevile kuna *Ubungo Interchange* ambayo tayari maandalizi ya ujenzi yameshaanza, mkandarasi yuko kwenye *site* kwa ajili ya kufanya *mobilization* na shughuli mbalimbali za kuhakikisha kwamba ujenzi unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali imeendelea na mpango wa kuhakikisha kwamba kila Mkoa katika nchi yetu ya Tanzania unaunganishwa kwa kiwango cha lami. Sehemu zile chache zilizobakia ambazo bado hazijapata mkandarasi tunaendelea kutangaza tenda ili mkandarasi apatikane kwa ajili ya kuweza kuunganisha Mikoa yetu kwa kiwango cha lami, lakini vilevile tunaunganisha Wilaya zetu

ndani ya Mikoa mbalimbali kwa kiwango cha lami na hatua kadhaa mbalimbali zimeshaendelea kutekelezwa. Tunashukuru sana kwa michango ya Waheshimiwa Wabunge na tunawaahidi tutaendelea kuhakikisha kwamba tunayachukua mawazo yao na kuyafanyia kazi kwa kadri itakavyowezekana, ili nchi yetu iweze kuwa na mtandao wa barabara nchi nzima ambao unapitika mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuwapongeza vilevile Waheshimiwa Wabunge ambao wametuletea michango kwa njia mbalimbali na kwa sekta yetu ya uchukuzi, mawasiliano na ujenzi tunawaahidi kwamba, tutafanya nao kazi kwa karibu sana, lakini tukiwakumbusha kwamba ujenzi au uinuaji wa kiwango cha barabara unategemea kwanza vikao ndani ya Halmashauri husika, baada ya hapo inekwenda kwenye *RCC,* baada ya hapo ndiyo inakuja kwenye bajeti kuu na kutengewa pesa kwa ajili ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo naomba kuunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Injinia Kamwelwe na Mheshimiwa Dkt. Tizeba na Mheshimiwa Dkt. Kalemani.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kunipa pumzi. Pili nimshukuru Mheshimiwa Rais, ameniamini miezi 23 katika nafasi ya Naibu Waziri, lakini baadae ameniamini zaidi na kunikabidhi nafasi ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji. Ninamshukuru sana na ahadi yangu kwake na ahadi kwa wananchi wa Tanzania ni kwamba nitawatumikia kuhakikisha wanapata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeze sana Waziri wa Fedha, ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, kwa kuleta mpango mzuri huu ambao hauna maneno mengi, lakini ukiuangalia unatupeleka moja kwa moja kwenye

uchumi wa kati ili tuhakikishe kwamba, wananchi wetu wanakuwa na maisha bora. Niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu ndani ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji na michango hii yote kwetu ni dira, tutaifanyia kazi, tutashirikiana na ninyi na tunaomba muendelee kutu-*support* ili tuweze kutekeleza majukumu yaliyo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninayo michango ya kiujumla kwenye Wizara yangu ya Maji na Umwagiliaji na nianze na tatizo ambalo tumekuwanalo nab ado tunalo sasa hivi kuhusiana na utoaji wa huduma ya maji vijijini na mijini, hasa kupitia katika mamlaka. Tunazo mamlaka za aina tatu, tuna mamlaka ya daraja la tatu, mamlaka daraja la pili na mamlaka daraja la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, daraja la kwanza wanajihudumia kwa asilimia 100, ikiwa ni kulipa mishahara, kununua madawa na kulipa gharama za umeme. Madaraja ya pili na daraja la tatu ni kwamba madaraja haya inabidi yasaidiwe hasa katika kulipa bili za umeme. Daraja la pili linasaidiwa kwa asilimia 50, daraja la tatu linasaidiwa kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko changamoto katika mamlaka hizi, zipo mamlaka ambazo zipo chini ya Wizara ya Maji na ambazo zipo chini ya Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tulishakaa na Serikali tukayaainisha medeni na tukakubaliana kwamba Serikali sasa hivi inaendelea kutafuta fedha ili iweze kulipa madeni yote ya nyuma. Tumejipanga kuhakikisha kwamba hatuendelei kuzalisha deni jingine na ndio maana tumekuja na mfumo wa mita za LUKU upande wa maji ili tukishaiweka mwananchi unalipia ndio uweze kupata huduma ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu katika hili, Waheshimiwa Wabunge na Serikali kwa ujumla ni kwamba sasa tunajadili mapendekezo ya maendeleo ya mwaka ujao

wa fedha pamoja na mwongozo wa bajeti, Serikali tuhakikishe watu wote wanatenga bajeti kwa ajili ya kuzihudumia hizi mamlaka za daraja la tatu na daraja la pili ili mwaka ujao wa fedha tena isitokee kwamba mtu anakatiwa umeme kwa sababu hajalipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Nzega sasa hivi wamekatiwa na maeneo mengine pia lakini kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Nishati kwamba tutakaa tuhakikishe kwamba wananchi hawa wanapata huduma ya maji. Changamoto ninayoipata ni kwamba umeme ukikatika, maji yakikosekana hatuangalii kwamba ni umeme linarudi kwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe sana hasa Serikali tuhakikishe kila mtu kwenye Taasisi yake mwaka ujao wa fedha atenge bajeti kwa ajili ya kulipia gharama hizo za umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kutekeleza azma ya kuhakikisha wananchi wa Tanzania wanapata maji safi na salama, bajeti ya mwaka 2006/2007 tulianzisha programu ya maendeleo ya sekta ya maji. Katika programu hiyo tulipanga kutekeleza miradi 1,810, hadi sasa kupitia progamu hiyo ya awamu ya kwanza ambayo ilikamilika mwezi Juni mwaka 2017, tumefanikiwa kutekeleza miradi 1,423, miradi iliyobaki ni miradi 378 lakini tunaendelea na utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya utekelezaji wa miradi hiyo, tumetengeneza vituo 117,000 vya kuchotea maji, kama vituo vyote vingetoa maji, sasa hivi tungekuwa na asilimia 78 ya upatikanaji wa maji safi na salama katika maeneo ya vijiji. Bahati mbaya sana kutokana na changamoto mbalimbali, asilimia 35 ya hivi vituo havitoi maji na matokeo yake sasa huduma ya maji inayopatikana kwa sasa ni asilimia 63.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia bajeti ya mwaka huu wa fedha tulionao 2017/2018 Waheshimiwa Wabunge vile vitabu mlivyopewa kwenye bajeti za Halmashauri tumeweka

kifungu cha fedha kwa ajili ya Halmashauri kuhakikisha kwamba wanarejesha huduma kwa kukafuta vyanzo vingine. Tumeweka *incentives* kwamba ukirejesha huduma ya kituo kutoa maji, unapata *sterling pound* 50 na ukiweka kituo kipya unapata *sterling pound* 1,500. Fedha mnazo zimeainishwa kwenye bajeti, kwa hiyo tujitahidi kuhakikisha kwamba tunarejesha hiyo huduma ambayo tumeweka vituo lakini vile vituo havitoi maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ambayo imejitokeza mpaka hivyo vituo vikakosa kutoa maji hadi sasa tumebaini kuna changamoto za aina tatu. Kwanza ni wananchi kushindwa kuendesha miradi hasa miradi ambayo unakuta kwamba mradi umewekwa katika kijiji wakaweka jenereta ambayo inatumia *diesel,* wananchi wanafikia mahali wanashindwa kumudu gharama ya kununua mafuta na matokeo yake ni kwamba mradi ule upo lakini hautoi maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekutana na mradi wa namna hiyo wakati wa ziara zangu nikiwa Manispaa ya Mji wa Singida nikakuta kuna mradi una vituo vya kuchotea maji zaidi ya 19, maji yapo lakini wamesitisha huduma kwa sababu mashine iliyowekwa ya kusukuma maji inatumia *diesel* na hawana uwezo wa kununua hiyo *diesel,* sasa hivi tumeelekeza kwamba miradi yote ambayo inatumia jenereta za *diesel* tuhakikishe kwamba tunaweka *solar* na ndio maana tuna bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishangaa Manispaa hiyo bajeti ya mwaka 2016/2017 walikuwa na shilingi bilioni mbili lakini hawakutumia hata senti tano na bado walishindwa kununua umeme wa kutumia nguvu ya jua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ni mabadiliko ya tabianchi na sisi wananchi kulima kwenye vyanzo vya maji, matokeo yake vyanzo vimekauka na miradi tuliyotekeleza tukiwa tunatarajia kwamba chanzo kitakuwa mahali fulani, maji hakuna na matokeo yake sasa maji hayatoki katika hiyo miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya tatu ni pamoja na usanifu mbaya, tumekutana na usanifu mbaya. Wataalam wanakwenda kusanifi kipindi cha mvua, kwa hiyo, kwa vyovyote maeneo yote unakuta yana maji, baada ya kiangazi lile eneo ulilobaini linakuwa halina maji. Kwa hiyo, sasa hivi tunasimamia kuhakikisha usanifu unafanyika wakati wa kiangazi ili chanzo kikipatikana kinakuwa na uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tumeanza awamu ya pili ambayo itakamilika mwaka 2020. Katika awamu hiyo, tunatarajia kutumia zaidi ya dola bilioni 3.3 na tunalenga kutengeneza miradi ya maji vijijini 4,015 na hadi sasa tayari tumeshasaini miradi 150 na tunaendelea vizuri kabisa. Hii ni miradi itakayotekelezwa katika vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna miradi zaidi ya 33 ambayo tunatarajia tuitekeleze miradi ambayo ni mikubwa. Miradi hii ni pamoja na mradi wa ujenzi wa bwawa la Kidunda, tuna mradi wa maji wa Mtwara Mikindani, tuna mradi wa usambazaji wa maji kutoka visiwa vya Kimbiji na Mpera na tuna miradi ya maji 17 katika miji 17 ambayo itafadhiliwa na mkopo nafuu kutoka Serikali ya India. Fedha hii imeshapatikana, taratibu za kukamilisha kusaini *financial agreement* ziko mbioni na wakati wowote ikishasainiwa basi tutaendelea na utekelezaji wa miradi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna mradi mkubwa wa maji utakaopeleka Wilaya zote za Simiyu, huu ni mradi mkubwa utakaotumia zaidi ya dola bilioni 300 na *tender* tumeshatangaza tayari. Kwa hiyo, tunasimamia kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao mradi tunaendelea na usanifu wa kutoa maji Mto Malagarasi kupeleka Tabora na kama tutaufanikisha mradi huu na maji yakawa mengi, tuna malengo ya kupanua huduma hii ili iweze kusambaa na mikoa mingine kama tulivyofanya maji ya kutoka Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mradi wa maji wa uondoaji wa majitaka katika Mji wa Dodoma nao pia tunaendelea nao kutafuta fedha. Pia tuna mradi wa maji kupeleka Mji wa Kisarawe na juzi meagiza ikifika mwezi wa tano mkataba wake uwe umeshasainiwa ili wananchi wa Kisarawe waweze kupata huduma ya majisafi na salama. Pia Kisarawe sasa hivi kuna eneo ambalo viwanda vinaendelea kujengwa na tayari tuna kiwanda cha *cement* pale kinafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mradi wa maji kwa ajili ya Mji wa Kilolo. Tuna mradi wa maji wa *HTM* nao pia taratibu zinaendelea...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Tizeba, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Kalemani.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote na mimi nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini kusimamia sekta ya kilimo hapa nchini. Pia niwashukuru sana viongozi wetu wakuu wa Serikali, Mheshimiwa Makamu wa Rais na Waziri Mkuu kwa uongozi wao wanaonipa ili kutekeleza majukumu yangu sawasawa. Pia nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuniletea Msaidizi katika shughuli Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa naamini kwamba tutafanya kazi vizuri kwa matarajio ya waliotuteua na wananchi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mpango na Mheshimiwa Dkt. Kijaji kwa kuleta huu mpango ambao kwa kweli unatoa dira ya namna uchumi wa pamoja unavyoweza kwenda na tukafikia hilo lengo letu la kuwa na uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niombe kutumia nafasi hii kuishukuru sana Kamati ya Kilimo, Mifugo, Maji na Uvuvi

kwa sababu wamekuwa msaada mkubwa katika kutekeleza majukumu yetu. Wametushauri na tumesikiliza ushauri wao, wametuelekeza na tumetekeleza maelekezo yao. Pia niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia kwa namna moja au nyingine kuhusu mambo ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kamati yetu, ratiba ya Bunge iliyokuwa imetolewa ilikuwa tuanze kuwasilisha taarifa za Wizara tarehe 30 mwezi uliopita, lakini kwa unyeti wa jambo la mahindi, Kamati ilituita mapema zaidi tarehe 25 ili tujadili suala la mahindi kwa udharura. Wapo wananchi wana mahindi, hawawezi kuyauza kwa sababu ya bei kushuka na kwa hivyo wanashindwa kuingia katika *cycle* nyingine ya kilimo kwa sababu hawana fedha kwa ajili ya pembejeo na maandalizi ya mashamba yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kutokana na mjadala katika Kamati, ndipo Serikali tulisikia na tukachukua pia hatua za kidharura tukaelekeza Wakala wetu wa Mazao *(NFRA)* waanze tena kwenda kununua katika maeneo yenye uzalishaji mkubwa, tukajipiga piga pesa ikapatikana ya kuanzia na tunaendelea ku-*mobilize funds* ili waendelee kununua katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi wapo wameanza manunuzi katika Mikoa ya Njombe na Ruvuma lakini pesa tena tulikuwa tunazungumza na Waziri wa Fedha nyingine imepatikana sasa wataanza pia kununua katika Mkoa wa Rukwa na baadae wataingia katika Mkoa wa Songwe. Kwa hiyo, hizi ni hatua ambazo tulizichukua kwa udharura ule ili kuhakikisha kwamba angalau fedha inaanza kupatikana kwa wananchi waweze kuingia katika kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya tathmini tumebaini pia kwamba mahindi yaliyopo kwa wananchi ni mengi sana na watu kwenye maeneo haya wasipopata soko la uhakika wengine hiyo fedha ambayo inatolewa na Serikali kupitia Wakala wake inaweza isiwafikie kabisa. Kwa hiyo, Serikali imeamua kwamba itawaruhusu wafanyabiashara

waweze kupeleka mazao nje ya nchi, hasa mahindi ili kutengeneza soko na kuchangamsha bei kwa wafanyabiashara na wakulima wa zao hili la mahindi hapa nchini. Tunaomba tu kwamba viongozi wote tushirikiane kuhakikisha kwamba taratibu za kawaida za uondoshaji wa mazao nje ya nchi zinafuatwa ili kulinda mipaka yetu na kulinda usalama wa chakula hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kuwaagiza Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kote nchini kuacha mara moja tabia ya kuzuia mazao kutoka katika mikoa yao kwenda mikoa mingine au kutoka katika wilaya zao kwenda wilaya zingine. Tanzania ni moja na tungependa bidhaa ziweze kusafiri kutoka sehemu moja ya nchi kwenda sehemu nyingine ya nchi bila vikwazo vyovyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru pia Wabunge wote wanaotoka maeneo yanayolima tumbaku kwa jinsi ambavyo wameshughulikia suala la ukosefu wa soko la zao hili kwa umakini na kuguswa sana. Serikali ilikwishaliona hili tatizo mapema la kwamba tumbaku imezalishwa zaidi ya mikataba iliyokuwepo na wanunuzi wetu wa kawaida wa hapa ndani, kwa hivyo tulianza mchakato wa kutafuta wanunuzi wa hii tumbaku ya ziada walioko ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada kubwa zimefanyika na mpaka hapa tunapozungumza sasa zipo kampuni za ndani ya hapa ya nchi walio tayari kununua hiyo tumbaku. Zipo kampuni pia ambazo zimeonyesha mwelekeo kutoka nje ya nchi ambao pia wapo tayari kununua hii tumbaku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie pia nafasi hii kuiagiza Bodi ya Tumbaku ifanye mazungumzo na makampuni yote yaliyo tayari kununua tumbaku hii ya ziada, ifikapo kesho mchana wawe wamekwishanipa taarifa ya kampuni gani inaunua wapi kiasi gani ili hii tumbaku iliyopo kwa wananchi isiendelee kuharibika kwa kutunzwa vibaya hasa ukizingatia kwamba sasa hivi tupo kwenye msimu wa

mvua na inaweza kunyeshewa na kupoteza ubora wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutarajie tu kwamba zoezi hili litakwenda vizuri, wanunuzi watapatikana wataichukua hii tumbaku nasi tutajipanga vizuri sasa kuhakikisha kwamba tunapanua wigo wa soko hili la tumbaku kwa kuingiza wanunuzi wengi zaidi wa tumbaku kuliko tulionao hivi sasa. Kwa hiyo, mazungumzo yanaendelea na nchi mbalimbali ambazo zina *interest* ya kununua tumbaku yetu na *Inshallah* Mungu akitujaalia tutapata wanunuzi wengi zaidi katika msimu ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti ilizungumzia suala la upatikanaji wa pembejeo kwa wakati. Ni kweli hili limekuwa tatizo kwa wakulima wetu hapa nchini kwa miaka mingi. Pembejeo inafika mahali na hasa pale tulipokuwa na mfumo wa ruzuku, pembejeo ya ruzuku inafika kwenye eneo msimu umekwisha mbolea na mbegu ndio zinafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, sasa hivi tunafanya mpango hapa nchini kupitia wizara yetu ambapo tutahakikisha kwamba mbolea inakuwepo maeneo yote wakati wote. Hili tunalifanya kupitia huu utaratibu wa uagizaji wambolea kwa pamoja, mbolea itakuwa inaendelea kuagizwa bila kujali msimu wa kilimo ili kuhakikisha kwamba ipo madukani muda wote na mwananchi akiihitaji anakwenda ananunua anafanya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo la kuamini kwamba kilimo ama pembejeo zinahitajika wakati wa mvua peke yake sio sahihi, kwa sababu wapo pia wananchi ambao wanafanya kilimo cha umwagiliaji, kwa hiyo, wao hawasubiri msimu ule mvua, wanaendelea na kilimo chao muda wote. Kwa hiyo, sasa tumeanzisha huu utaratibu ambao utakuwa unatuhakikisha kwamba madukani iko mbolea na inayohimilika kwa maana ya bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la bei limekuwa ni tatizo au changamoto kwa wakulima wetu kwamba wengi

wamekuwa hawawezi kumudu bei ya mbolea hizi. Sasa tulichokifanya tumeanzisha huo utaratibu ambao unatuhakikishia kushuka kwa bei ya hizi mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tena kutumia fursa hii kuwakumbusha wadau wote wahakikishe kwamba bei elekezi kwa aina mbili za mbolea tulizoanza nazo katika mfumo huu yaani mbolea ya kupandia *DAP* na mbolea ya kukuzia *Urea* bei elekezi zinazingatiwa kwenye maeneo yote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwatahadharishe wafanyabiashara ambao hawataki uaminifu, wanaoendelea kuuza bei elekezi katika maduka ya jumla ya Mikoani na Wilayani kwamba jambo hilo ni kuvunja sheria, kwa sababu wao katika maduka ya jumla wanatakiwa wauze kwa bei chini ya bei elekezi ili bei elekezi imfikie mwananchi kijijini ambaye ananunua mbolea na kwenda shambani. Bei elekezi siyo katika maduka ya jumla isipokuwa bei elekezi ni ya wakulima anayenunua na kwenda shambani. Kwa hivyo, viongozi wote wa mikoa simamieni hili jambo, viongozi wote wa wilaya wasimamie hili jambo ili wananchi waweze kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo limezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge na tumeona ni vema na sisi tulitolee maoni ni kuhusu uboreshaji wa lililokuwa Shirika letu la Usagaji la Taifa *(National Milling Corporation).* Niseme tu kwamba sasa hivi iliyokuwa *NMC* iko chini ya Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko na bodi hii imekwishaanza kazi. Ilianzishwa mwaka 2009 lakini utekelezaji wa majukumu yake umeanza mwaka 2013 na sasa hivi wanasaga na kununua mahindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasaga mahindi katika kinu cha Iringa na katika msimu huu mwanzo walikwisha nunua tani 2,300 za mahindi lakini sasa hivi wamepata pesa, mkopo kutoka Shirika letu la Hifadhi ya Taifa *(NSSF)* shilingi bilioni 8.9 na tumewaelekeza kwamba waendelee na ununuzi wa mahindi katika maeneo haya ambayo yana uzalishaji

mkubwa ili kuondoa hiyo *stress* ya bei katika soko la mahindi. Pia wanafanya jitihada za ku-*possess* mali zao zote ambazo wamepewa kwa mujibu wa sheria ili waweze sasa kufanya biashara kama ambavyo inatarajiwa kutoka kwa wananchi na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisigongewe kengele ya pili, naomba nikome hapo. Nisisitize tu kwamba ni ruhusa sasa kusafirisha mahindi kwenda nje ya nchi na taratibu tu za kawaida zifuatwe, pia ifikapo kesho mchana suala la tumbaku ya ziada liwe limekwishapata suluhu kwa maana ya kwamba mnunuzi gani ananunua kiasi gani, wapi niwe nimekwishafahamishwa ili keshokutwa kama ni ununuzi kuanza uanze mara moja bila kuchelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kalemani, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, ajiandae Mheshimiwa Profesa Ndalichako na ajiandae pia Mheshimiwa Mpina.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lubeleje, taarifa unampa nani? Haya, kwa vile najua mahindi yanamsumbua kila mtu sema.

## T A A R I F A

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ninachangia Hoja ya Waziri wa Fedha na Mipango, nilizungumzia sana tatizo la ukame, watu ambao wana njaa na chakula kimejaa kwenye ma-*godown.* Sasa Waziri wa Kilimo hakugusia hilo ni lini wataanza kugawa chakula cha msaada? Watu wanateseka na njaa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, na ninaomba nimjibu Mzee wangu, Mheshimiwa Lubeleje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa tulizalisha kwa utoshelevu wa asilimia 123. Kama ulivyosikia katika maelezo yangu sasa hivi yapo maeneo yenye ziada nchini, kule bei ziko chini, wananchi wanalalamika hawana pa kuuza mahindi kiasi kwamba tumefikia turuhusu watu kupeleka mahindi nje ya nchi. Lakini yapo maeneo na kwa tathmini yetu, mikoa kama 11 itakuwa na utoshelevu wa chini ya kiwango na kwa hiyo tunaendelea kuwaomba wafanyabiashara nchini wachukue mahindi kule ambapo yapo ya ziada wapeleke kwenye maeneo haya ambayo hayana utoshelevu wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nitumie tu tena nafasi hii labda kulisemea hili, kwamba wafanyabiashara nchini na wakala zetu za Serikali wanaonunua watachukua mahindi maeneo haya yenye ziada na kwenda kuyauza kwenye maeneo ambayo yana upungufu ikiwamo pia Jimbo lake la Mpwapwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kalemani, atafuatia Mheshimiwa Dkt. Kigwangala halafu Profesa Ndalichako.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri kamili wa Nishati, Wizara ambayo ni mpya. Ninapenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote, hata mimi kuwa Waziri wa Nishati nadhani ni kwa sababu ya mikono ya Waheshimiwa Wabunge hawa, kwa jinsi ambavyo tumeshirikiana sana awamu iliyopita katika masuala yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa juhudi ambazo mlikuwa mnatupa na ushirikiano wenu, tunaamini sasa tutashirikiana zaidi katika safari inayofuata. Hongereni sana Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano, Wizara yetu mpya ya Nishati inayo vipaumbele ambavyo ni vya msingi sana katika kujenga uchumi wa viwanda. Tunatambua kama Serikali kwamba uchumi ni nishati, viwanda ni nishati na maendeleo ni nishati, bila nishati hakuna maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya vipaumbele ambavyo kwa kweli vimezungumzwa vizuri sana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango ambavyo ninapenda kurejea kwenye michango ni pamoja na miradi mikubwa ya kuzalisha umeme. Hivi sasa tuna mkakati mkubwa wa kuzalisha umeme wa kujitosheleza kujenga uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa umeme tulionao unatosha kwa mazingira ya sasa, lakini hauwezi kutosheleza kwa mwendo kasi wa kujenga uchumi tunaokwenda nao. Kwa hiyo, juhudi kubwa tumezielekeza katika kuzalisha umeme ili sasa utumike vizuri kwenye kujenga uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mkubwa wa kuzalisha umeme tulionao kwa sasa ni Mradi wa Kinyerezi Namba Moja na Kinyerezi Namba Mbili. Mradi huu tuna matarajio utakamilika *soon,* mwezi Agosti, 2018 miradi miwili itakamilika na kutuingizia sasa jumla ya megawati 425. Huu ni umeme mkubwa, kama utaingia kwenye Gridi ya Taifa utachangia sana kwenye kujenga uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuishukuru sana Serikali kupitia kwa Mheshimiwa Rais na Serikali yetu kwa kupitisha uamuzi wa kujenga umeme wa maji kupitia *Stiegler's Gorge* ya Mto Rufiji. Huu ni umeme mkubwa ambao utatuzalishia megawati 2100. Taratibu za kuanza kuujenga mrdai huu zimeshaanza, hivi sasa tumeshatangaza *tender* na waombaji zaidi ya 80 wamejitokeza, kesho tunaanza kufungua sasa kuanza kufanya *evaluation.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matayarisho ya ujenzi wa

mradi huu yatakamilika mwezi Disemba mwaka huu na mwezi Januari tunaanza kuujenga. Kwa hiyo, kufikia mwaka 2020 tutaingiza kwenye Gridi ya Taifa megawati nyingine 2100. Tujipongeze sana kwa mradi huu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ulichelewa kidogo kwa sababu kubwa mbili; ya kwanza, kulikuwa na masuala ya mazingira, katika awamu hii sio kwamba tunapuuza mambo ya mazingira, tutaenda nayo lakini huku tukiharakisha ujenzi wake. Jambo la pili, mradi huu huko nyuma uliwekwa chini ya *RUBADA,* kazi ya *RUBADA* kimsingi haikuwa kuzalisha umeme, ilikuwa ni ku-*reserve* mambo ya mazingira na vyanzo vya maji lakini baada ya Serikali kuamua kwamba mradi huu upelekwe kwenye Wizara inayoshughulika na masuala ya nishati, Serikali tumeuchukua na ndiyo maana tutaharakisha ujenzi wake. Kwa hiyo, niwape uhakika wananchi na Waheshimiwa Wabunge kwamba mradi huu utajengwa kuanzia Januari, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele chetu cha pili, pamoja na mambo mengine, ni ukamilishaji wa ujenzi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima, Uganda kuja Tanga, Tanzania. Kama mnavyokumbuka, niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge, mwezi Septemba 2017 mlipitisha mkataba wa nchi mbili ili uanze kutekelezwa. Tunawashukuru sana kwa sababu baada ya hapo ujenzi umeshaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu kama ambavyo nimeeleza ni mradi mkubwa. Hapa nchini kwetu utahusisha Mikoa minane ambapo utapita katika Mikoa ya Geita, Tabora, Shinyanga, Singida, Dodoma, Manyara na hatimaye Tanga. Kama ambavyo nimekuwa nikieleza mara zote, mradi huu, nasema utakuwa na *impact* kubwa kwa sababu unapita katika Wilaya nyingi sana, unapita katika Wilaya 24 katika Mikoa niliyoitaja, kadhalika unapita katika vijiji 134 na unapita katika vitongoji 210. Sasa unaweza ukaona manufaa yake itakavyokuwa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kokote mradi utakapopita utakuwa na fursa kubwa sana za kiuchumi kwa Watanzania

na wawekezaji wengine. Kwa hiyo, mradi huu ujenzi wake unaanza pia mwezi Januari utakapokamilika ndani ya miaka mitatu, fursa kubwa sana za kiuchumi zitakuwa zimeongezeka katika nchi yetu. Kwa hiyo, nilitaka kutoa taarifa kwamba haya ni maendeleo mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na juzi tuikuwa Uganda, tumekamilisha uwekaji wa bomba na kwa upande wetu tulishakamilisha, sasa kazi inayofanyika ni kukamilisha majadiliao kati ya Serikali na wawekezaji. Hatua inayofuata ni kuingia mkataba wa ubia na ujenzi kuanza mara moja; huo ulikuwa ni mradi wa pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa tatu ni Mradi wa Uchakataji Gesi *(LMG),* huu ni mradi muhimu sana kama ambavyo mnausikia. Upo uvumi kwamba inawezekana mradi huu haupo, niseme kwa niaba ya Serikali; msimamo wa Serikali wa kujenga mradi huu uko palepale. Sasa kinachofanyika, pamoja na mambo mengine, tumeshapata eneo, tumeshafanya tathmini ya wale watakaoathirika na kutakiwa kufidiwa, lakini kazi inayofanyika sasa ni kukamilisha majadiliano ya uwekezaji, hatua inayofuata ni kuingia makubaliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nyingine iliyokamilika ni kupata eneo ambalo kinu kitajengwa kwa ajili ya kuchakata hiyo gesi. Kwa hiyo, hatua zinakwenda vizuri, na kesho nitakutana na wadau wote watakaojenga mradi ule kama *Oil4All, Big Shell* na makampuni mengine ili taratibu za kuanza kujenga zianze mara moja. Kwa hiyo, ule uvumi wa kwamba mradi huu umetelekezwa, Serikali iko makini sana na mradi huu na lazima utekelezwe kwa nguvu zote. Kama Waziri wa Wizara hii pamoja na Naibu wangu, tutausimamia mradi huu kwa makini sana mpaka utakapokamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya gesi viwandani. Kama mnavyojua imechukua muda mrefu sana, hasa viwanda vya mbolea na vingine vya mkakati kupewa gesi, ninapenda kutoa taarifa kwenye kikao chako kwamba wiki mbili zilizopita tumekamilisha makubaliano kati ya Serikali

na Ferrostaal, sasa wako tayari kuja kuwekeza wamekubaliana na bei ya Serikali. Walichoomba ni kupata unafuu wa masuala machache ya kodi. Sasa tumeshaanza kukamilisha makubaliano nao, tunachofanya ni kupitia maombi yao ili baada ya kukamilika waanze kuwekeza. Kwa hiyo, maeneo ya Kilwa Masoko kutajengwa kiwanda kikubwa cha mbolea chini ya ujenzi wa Ferrostaal kuanzia sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mtwara bado tunaendelea kuzungumza na *HELM* na wenyewe wanaonesha nia ya kukubaliana na Serikali ili sasa nao waingie katika utaratibu wa kujenga. Kwa hiyo, viwanda vya kimkakati vitaanza kujengwa sasa kwa sababu tunakwenda kwa kukubaliana pamoja.

Mradi mwingine ni wa usambazaji umeme vijijini wa *REA.* Tunaposema ujenzi wa viwanda, havijengwi mjini peke yake. Serikali imedhamiria viwanda vianze kujengwa kuanzia vijijini na hakuna njia ya kujenga viwanda vijijini kama hujawapelekea wananchi umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wetu uko palepale, kama ambavyo tumeeleza, majibu mengi yametolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini mimi nifafanue kwa urefu zaidi. Kwamba mradi huu kama ambavyo tumekuwa tukisema tumeanza kuutekeleza. Na nitoe rai na tamko kwa wakandarasi wote, tunataka ifikapo tarehe 20 mwezi huu, wakandarasi wote wa *REA* wawe wamesharipoti katika maeneo yao na mkandarasi yeyote abaye atakuwa hajafika kwenye eneo lake na kuanza kazi ifikapo tarehe 20 mwezi huu atakumbwa na kimbunga kikali kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kusema kwamba Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano kuwapelekea umeme wananchi kwa ajili ya kujenga uchumi tunakwenda nao vizuri. Vijiji vyote 7,873 vitapatiwa umeme katika awamu hii ya kwanza tunaanza na vijiji 3,359 lakini baadaye tunamalizia na vijiji 4,320, vyote vitapelekewa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo ya mitambo ya maji ambayo tumedhamiria kuyapelekea umeme ili kurahisisha shughuli zao. Kule Karatu tayari vile visima walivyokuwa wameomba tumewapelekea umeme na tunataka kupeleka visima vya maji maeneo ya Mara na mikoa mingine. Lakini maeneo yote ambayo kutakuwa na mitambo ya maji niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge mtupatie orodha ya maeneo hayo ili tuanze kuyapelekea umeme mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu na mradi wa kusambaza gesi majumbani. Huu mradi ulikuwa unafanyiwa tathmini, tathmini imekamilika, hivi karibuni tutatoa tenda kwa ajili ya kuanza ujenzi. Kadhalika tumezungumza na wadau mbalimbali wanaounga mkono juhudi kwa ajili ya kujenga viwanda hivi. Tutaanza na Mkoa wa Dar es Salaam ili kupunguza matumizi ya mkaa. Tutaanza kusambaza Dar es Salaam kwa kaya 3,000 na baadaye tutahamia Mtwara na Lindi na baadaye tutakwenda katika Mikoa ya Dodoma, Morogoro, Singida na hatimaye katika mikoa yote ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itoshe tu kusema naunga mkono hoja, Wizara ya Nishati itapambana kwa niaba ya Serikali kuhakikisha kwamba uchumi wa viwanda unajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Dkt. Kigwangalla na Mheshimiwa Profesa Ndalichako ajiandae.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii na mimi nichangie kwenye hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango. Kwanza, nianze kwa kuiunga mkono hoja hii, lakini pili kwa kumpongeza yeye mwenyewe binafasi na Naibu wake kwa kuleta mpango huu mzuri ambao unatoa dira ya namna

ambavyo Serikali itatekeleza majukumu yake kwenye mwaka unaokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, naomba nitoe ufafanuzi kwenye maeneo machache ambayo yamegusa sekta ya maliasili na utalii kwa ujumla wake. Lakini kabla ya kufanya hivyo, nitumie nafasi hii kuwashukuru viongozi wetu wa juu wa Serikali kwa miongozo mbalimbali na maagizo ambayo wamekuwa wakitupa toka wametupa dhamana ya kusimamia sekta hii. Mimi naomba niwape uhakika tu wao pamoja na wananchi wa nchi yetu kwamba sintowaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo nimeona limejitokeza kwa kiasi kikubwa na ambalo ninaomba nianze kwa kulitolea ufafanuzi kabla sijafika mbali ni suala la kwamba Waziri mpya wa Maliasili na Utalii ameanza kazi kwa kufukua makaburi. Naomba niseme tu kwamba mimi siyo mashuhuri sana kwa ufukuaji wa makaburi, lakini ukiwa Waziri halafu ukawekwa kwenye Wizara ambayo wiki ya kwanza tu hata kabla hujaanza kazi kila mtu anasema umekalia kuti kavu, ni lazima kabla hujaanza kufanya kazi uliyopewa uanze kwanza kwa kusafisha nyumba yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, tumeanza kazi ya *hygiene* kwenye Wizara hii na kazi hii haitakoma mpaka pale ambapo mitandao yote ya watu ambao wako ndani ya Wizara hii wanashiriki kwenye vitendo vya ujangili, wanashiriki kwenye hujuma na wamekuwa wakitajwatajwa kwenye kashfa mbalimbali za rushwa, tutashughulika nao kwanza. Tukimaliza kuing'oa hii mitandao sasa tutaanza kazi kubwa na pana na ya maana zaidi kwa nchi yetu ya kuendelea kuongeza idadi ya watalii, lakini pia kuongeza idadi ya vivutio, pia kuendelea na kazi ya uhifadhi wa rasilimali hii adimu tuliyonayo kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutafanya hivyo kwa kuwekeza kwenye kanda nyingine kama Kanda ya Kusini kwa maana ya *diversification* ambapo kwa sasa tutaelekeza nguvu zetu huko ili kuifungua *corridor* ya Kusini kiutalii. Serikali

imepata fedha, shilingi bilioni takribani juu kidogo ya 300 kwa ajili ya kutekeleza mradi mkubwa wa kuifungua Kanda ya Kusini kiutalii na ninaomba hapa nitambue mchango mkubwa wa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango na timu yake, kwa kazi kubwa waliyofanya ya kuandika andiko la mradi huu na hatimaye kufanikisha zoezi la kupata fedha hizi zaidi ya bilioni 300 kwa ajili ya kufungua *corridor* mpya ya Kusini kitalii na ninaona kwa kweli yuko *busy* kutekeleza mpango wake ule uliopita na sisi tunamshukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla hatujafika kuanza kutekeleza hii mipango yote mizuri, nilisema ni lazima tuanze kusafisha. Katika kusafisha naomba niseme sikusudii kufukua makaburi ya Mawaziri wazuri waliopita hapo wakapata ajali mbalimbali za kisiasa kama akina Mheshimiwa Maige, Mheshimiwa Kagasheki na Mheshimiwa Maghembe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nianze kwa kuzungumzia Waziri mmoja ambaye wenzetu hawa wa Upinzani walimsema sana alipokuwa Waziri wa Maliasili na Utalii na huyu si mwingine ni Mheshimiwa Lazaro Nyalandu. Ninataka niseme tu kwamba rafiki yangu, Mheshimiwa Nassari alizungumza kwa mwembewe nyingi sana hapa Bungeni kwamba kama Dkt. Slaa...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, *order!* Hebu vumilieni.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, aende kwenye Mpango.

**MWENYEKITI:** Mimi ndiye niliyekalia Kiti, ninaye-*control*, siyo wewe. Wewe Mheshimiwa Haonga kaa kimya. Huwezi kujibizana na Kiti, kama msemaji atakosea mimi ndiye nitakayemrekebisha siyo wewe. Kaa kimya, itapendeza ukitulia. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Unajua ukiwa unaishi kwenye nyumba ya vioo, usianzishe vita ya mawe, kuna wengine kwa wale mliokuja wapya humu Bungeni mnatakiwa mjifunze mazingira ya humu ndani, kuna watu wanaguswa na kuna watu hawaguswi. Mimi ni katika watu wasioguswa na huwa sipendi mambo ya kipuuzi kabisa hata siku moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu amesema nimeanza kazi kwa kuanza kufukua makaburi sasa sitaki kuwakumbusha yaliyotokea huko nyuma lakini naomba tu niwape uhakika kwamba mimi huwa sichezewi chezewi. Mtu aliyesema nimeanza kazi hii kwa kufukua makaburi na mimi nasema leo nafukua moja na ninaanza kufukua hilo moja kwa maelezo yaliyotolewa na Wabunge hawa wa Upinzani kwenye Bunge lililopita. Walisema Mheshimiwa Lazaro Nyalandu kazi yake ni kustarehe kwenye mahoteli ya kitalii, kazi yake ni kutembea nchi za mbali huko Marekani wapi na warembo, wakasema alitembea aliendа Marekani na Aunty Ezekiel.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakasema Ndugu Lazaro Nyalandu anatumia helikopta za wawaekezaji kwa shughuli zake binafsi za kisiasa na Mheshimiwa Nassari alisema kwamba kama yeye kama Dkt. Slaa angeshinda Urais mwaka 2015 na akampa yeye Uwaziri wa Mambo ya Ndani kwa siku moja tu, angeanza kwa kushughulika na Mawaziri wa hovyo kama Mheshimiwa Lazaro Nyalandu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo ninaeleza kwamba kwa nini Mheshimiwa Nassari alikuwa sahihi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Nassari alikuwa sahihi kwa sababu wakati Waziri Nyalandu akistarehe kwenye Hoteli ya Serena pale Dar es Salaam akitumia helikopta ya mwekezaji wa *TGTS,* mezani kwake.......

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nimewaona wawili upande huu ambao mnasema nje ya utaratibu wa Kibunge na utaratibu wa Kibunge kama unahoja unasimama na *you have to catch the Speaker's eyes,* nikikuona nikuruhusu kama sikuruhusu unakaa, unapendeza kwa kukaa na kama mtu anataka kuharibu kipindi hiki cha mchana, nawaambieni na mapema tuanze kuharibiana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba kuna sauti mbili za Wabunge wanawake nimeshaziona na nimeshazi-*mark*, si vizuri kutajana majina lakini ikibidi tutasema. Kwa hiyo, naomba kama mchangiaji mnamuona mimi hapa ndio *referee* mimi siyo kocha. Kama mlivyotulia hivyo hivyo tulieni inapendeza. Mheshimiwa Waziri endelea.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nilichokuwa nataka kusema ni tu kwamba wakati Mheshimiwa Nyalandu Nyalandu akivinjari kwenye Hoteli ya Serena ambapo alikuwa akifanyia kazi zake za Waziri wa Maliasili na Utalii kwenye hoteli ile na akapewa chumba akawa anaishi pale kwa muda wote ule, mezani kwake kulikuwa kuna *GN* yaani tamko la Serikali kuhusiana na kitu kinachoitwa *concession fees* kwenye mahoteli ambayo yako ndani ya mbuga ya Serengeti.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu Utaratibu.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja iliyopo mezani kwako ni kujadili Mpango wa Maendeleo uliowasilishwa na Waziri wa Fedha...

**MBUNGE FULANI:** Kaa wewe.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** ...na katika Bunge lako hili leo ni siku ya sita tunajadili. Kwa hiyo, tunamuomba

Mheshimiwa Waziri ajibu hoja zilizotolewa na Wabunge zilizoelekezwa kwenye Wizara yake. Haya anayotuambia ya Mheshimiwa Nassari humu ndani hatuyajui na kama alivyosema hatujayajadili na wala hayajajadiliwa kwenye Bunge la Kumi na Moja hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ajibu hoja, tunajadili suala kubwa na suala nyeti hapa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bobali unayo Kanuni hapo? Sasa nenda kasome Kanuni ya 68(10). Mheshimiwa Waziri endelea kwenye hoja yako. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Bobali mimi mzoefu humu ndani, wewe unadhani mimi najibu hoja, mimi sijibu hoja mimi nachangia, mwenye hoja yuko pale Waziri wa Fedha na Mipango. *(Makofi)*

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Uzoefu maana yake nini?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Muwe mnajifunza nishasema mimi huwa sichezewi chezewi.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Wewe unamtisha nani wewe bwana!

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Kwa sababu najua Kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kuchangia, ninachokisema ni kwamba wakati Mheshimiwa Nyalandu akifanya yote hayo kulikuwa kuna mambo makubwa mawili ambayo napenda tu kuyatolea mfano hapa.

Moja; mezani kwake kama Waziri wa Maliasili na Utalii kulikuwa kuna *concession fees* ambayo ilikuwa imependekezwa na *TANAPA* na gazeti likatengenezwa likisubiri *signature* ya Waziri ili Serikali ianze ku-*charge concession fees* kwenye mahoteli ya kitalii. Hilo lingeongeza

mapato na kwa mwaka huo wa 2014 tungeweza kukusanya bilioni 16 lakini Waziri yule hakusaini hiyo *GN* mpaka anaondoka madarakani, maana yake Mheshimiwa Nyalandu aliikosesha Serikali mapato ya takribani bilioni 32, hilo ni moja na ni jambo ambalo watu wa mahoteli walipinga na baada ya watu wa mahoteli kupinga, Serikali ikashitakiwa Mahakamani, Serikali ikapata ushindi mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, Waziri alikuwa hana lolote lile la kuamua kwa sababu kuna amri ya Mahakama kwamba Serikali iko sahihi na i-*charge concession fees,* lakini Waziri yule hakusaini kwa miaka miwili mpaka anatoka madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo kama haya ukiniambia nafukua makaburi mniache tu niendelee kufukua lazima nifukue kwa sababu bila kuweka mambo sawa, bila kujua kwa nini Mheshimiwa Nyalandu hakusaini, bila kujua Mheshimiwa Nyalandu alikuwa anashirikiana na akina nani na je, alikuwa anashirikiana nao wapo ama wameondoka? Huwezi kufanya kazi yako vizuri. Ndiyo maana hata Mawaziri watakaowekwa pale wataendelea kutolewa tu, wataendelea kukalia kuti kavu tu, sasa mimi siko tayari kukalia kuti kavu, hata nikikaa miezi mitatu nitakuwa nimeinyoosha hii sekta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili napenda kuzungumzia mahusiano ya kutatanisha aliyokuwa nayo Waziri wa Maliasili na Utalii Ndugu Nyalandu na wawekezaji wa taasisi maarufu inajulikana kama *Friedkin Family Foundation* ni billionea kutoka nchi ya Marekani ambayo ilikuwa ina Makampuni yanayofanya kazi mbalimbali za utalii hapa na bado yapo mpaka sasa. Moja inaitwa *Mwiba Holdings,* nyingine inaitwa *Winged to Winrose* na nyingine inaitwa *Tanzania Game Trackers Safaris.* Kampuni zote hizi, Kampuni ya *TGTS* ilipewa vitalu zaidi ya vitano ambazo ingepaswa kupewa kwa mujibu wa sheria maana yake ni kwmba hapo kuna mazingira ya kutatanisha, kuna mambo hayako sawa na bado Kampuni hii ipo na inafanya kazi

kwenye sekta hii, ukisema nisifufue makaburi utakuwa unanionea, ni lazima nijue kwa nini waliopewa vitalu zaidi ya vitano? Kwa nini wanaendelea kuwinda?

Kampuni ya *Mwiba Holdings* ina tuhuma za ujangili kwamba Kampuni inawinda, inafaya kazi za utalii lakini imekamatwa na nyara za Serikali na hizi Kampuni zote zinamilikiwa na mtu mmoja anaiywa Tom Friedkin ambaye ni rafiki wa Ndugu Nyalandu na Waziri huyu kama nilivyosema huko nyuma alikuwa akifanya kampeni za Urais kipindi kile tulijaribu na sisi kuomba ridhaa ya Chama kugombea Urais, alikuwa akifanya kampeni zake, akizunguka na helkopta ambayo inamilikiwa na Kampuni ya huyu Ndugu Tom Friedkin. Sasa katika mazingira kama hayo, Waziri wa Maliasili na Utalii, *GN* ya kusaini kuhusu kudai *concession fee* iko mezani kwao hausaini na unaka kwenye hoteli...

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kumpa taarifa Mheshimiwa Waziri kwamba yote hayo kama alifanya Waziri Nyalandu miaka yote hiyo, kwa muda wote huo ilipaswa awe ameshachukuliwa hatua kwa maana ya kupelekwa mahakamani kwa muda mrefu na wasingeweza kusubiri kuona amehama chama amehamia chama kingine ndiyo wanakuja na maneno mepesi mepesi, siasa nyepesi ambazo haziwezi kujenga Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni taarifa tu kwamba yoye aliyo...

**MWENYEKITI:** Ahsante ameshakuelewa, Mheshimiwa Kigwangalla.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, zama zinabadilika na uongozi pia unabadilika. Kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii sasa hivi kuna Waziri

ambaye anaweza kumchukulia hatua Ndugu Nyalandu, kwa hivyo kama ndiyo kilio chako Ndugu Haonga mimi nitaagiza hapa TAKUKURU pamoja na Jeshi la Polisi wayasikilize haya ninayosema, wachukue *Hansard,* wakafanye uchunguzi ili waweze kumchukulia hatua Ndugu Nyalandu wala hilo halisumbui. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ndiyo kiu yako na wewe kama mwananchi na kama Mbunge kwamba kwa nini Nyalandu hajafika mahakamani, mahakama bado zipo na jinai haiishi muda, jinai hata miaka 100 ipo tu, kwa hiyo vyombo vinavyohusika vichukue hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo Ndugu Nyalandu alikuwa akitumia helicopter za Kampuni za huyu Ndugu Tom Friedkin kufanya kampeni zake za Urais lakini pia kufanya kampeni zake za ubunge Jimboni. Katika mazingira kama hayo, dada yangu Devotha Minja ukisema nisifukue makaburi utakuwa unanionea bure tu. Mniache nifukue haya makaburi, tuweke sawa nchi, tumsaidie Mheshimiwa Rais ndiyo kazi tuliyopewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, vitalu vya uwindaji kabla ya Ndugu Nyalandu vilikuwa vikitolewa kwa makampuni mbalimbali na muda wa kuwinda ulikuwa ni katika kipindi cha miezi mitatu tu, kati ya Julai mpaka Oktoba ili kuwapa nafasi wale wanyama kupumua na pia kuzaliana, lakini...

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,ninakushukuru kwa kunipa nafasi.

Napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Wziri anayechangia, nafikiri anaeleza kitu kizuri sana na mimi ninamshauri kwa kuwa ameingia kwenye Wizara hiyo,

tunaomba atupe taarifa za Mheshimiwa Maige, za Mzee aliyeondolewa pia wote kwa pamoja na Mheshimiwa Maghembe atupatie ili tuweze kulisaidia taifa letu kusonga mbele. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Hiyo ni katika taarifa ambazo silazimiki kuzijibu kwa sababu haina maana yoyote.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea na mchango wangu, Ndugu Nyalandu alivyopewa tu kiti cha Waziri wa Maliasili na Utalii alichokifanya bila huruma yoyote ile, bila uzalendo wowote ule alianzisha mchakato wa kubadilisha...

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ndalichako ajiandae Mheshimiwa Mpina.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii nami nichangie hoja ambayo iko mezani kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuanza kwa kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuniamini na kuniteua tena niendelee kutumikia katika sekta hii ya elimu. Nimhakikishie Mheshimiwa Rais na Watanzania kwa ujumla kwamba nitafanya kazi yangu kwa uadilifu na kamwe sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuanza mchango wangu kwa hoja iliyoko mbele yetu ambayo ni Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2018/2019 pamoja na Mwongozo wa Bajeti kwa kuanza kusema kwamba ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja hii kwa sababu imeandaliwa vizuri na imeangalia maeneo ambayo ni muhimu katika kusukuma maendeleo kwa Taifa letu. Napenda kumpongeza kwa dhati Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Philip Mpango na Naibu wake kwa kazi nzuri ambayo wameifanya katika kuandaa hoja hizi pamoja na watendaji wote katika Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza Mpango huu, Wizara yangu inayo mchango muhimu kwa sababu elimu ndiyo nguzo muhimu katika kuleta maendeleo ya Taifa letu. Kama ambavyo tunafahamu, Mpango wetu wa maendeleo umejikita katika kujenga uchumi wa viwanda na ili tuweze kujenga uchumi wa viwanda ni lazima kuangalia kwa umakini ujuzi wa Watanzania ambao ndiyo nguzo kuu ya maendeleo katika Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu katika kuhakikisha kwamba tunaweka mchango unaotakiwa katika kukuza ujuzi nchini, tumeweza kufanya mambo mbalimbali, Waheshimiwa Wabunge wamekuwa katika michango yao wanaulizia na kuonesha wasiwasi wao kama kweli hii Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba kunakuwa na ujuzi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme katika mpango wetu tumeonyesha kwamba ili tuweze kwenda na kasi inayotakiwa tunatakiwa tuwe na asilimia 55 ya Watanzania wenye ujuzi wa chini, asilimia 33 ya ujuzi wa kati na asilimia 12 ya ujuzi wa juu.

Kwa hiyo, Serikali inao Mpango Mkakati wa Kukuza Ujuzi *(National Skills Development Strategy)* ambao katika kutekeleza mpango huo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu kuna mpango ambao tunazo dola milioni 120 ambazo ni sawa na fedha za Kitanzania bilioni 250 ambazo zinalenga kukuza ujuzi

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zitawezesha kuimarisha mafunzo ya ufundi stadi kwa kuimarisha

miundombinu katika taasisi zetu zinazotoa mafunzo ya ufundi stadi hususan *VETA*, *Arusha Technical, Dar es Salaam Institute of Technology* pamoja na taasisi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia huu mpango wa elimu na ujuzi kwa kazi zenye tija *(education and skills for productive jobs)* umejikita katika kuangalia maeneo ambayo ni ya kipaumbele katika mpango wetu wa maendeleo ambao ni pamoja na sekta ya kilimo, utalii, usafirishaji, ujenzi, nishati pamoja na TEHAMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna mojawapo ya kupata fedha hizi ambazo nimezisema bilioni 250 ambazo Serikali tayari inazo kwa ajili ya kutekeleza mradi huu itakuwa ni pamoja na kuandika maandiko ambayo ni shindani. Kwa hiyo, nitumie fursa hii kuwataka Waheshimiwa Wabunge tushirikiane katika kuhakikisha kwamba fedha hizi ambazo tunategemea kutangaza kwa mara ya kwanza maombi kwa ajili ya kupaya ufadhili *(skills development fund)* mwishoni mwa mwezi huu tushirikiane kuhamasisha taasisi za ufundi zilizoko katika maeneo yetu kwa sababu fedha zitakuwa zinatolewa katika mfumo wa ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ningependa kuchangia ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelizungumza katika michango yao ni suala la utoaji wa elimu bure na suala la changamoto zilizopo katika utoaji elimu.

Kwanza niseme kwamba suala la utaoji wa elimu bure katika Nchi hii limekua na mafanikio makubwa sana. Kila mwezi Serikali inatoa kiasi cha shilingi bilioni 20.8 kwa ajili ya elimu bure na mojawapo ya vigezo ambavyo tunaweza tukavitumia kusema kwamba kumekuwa na mafanikio makubwa, ukiangalia takwimu za wanafunzi ambao wanafanya mtihani wa kidato cha pili ambao wameanza leo hii wameongezeka kutoka wanafunzi 435,075 mwaka 2016 hadi kufukia wanafunzi 521,855 ambalo ni ongezeko la wanafunzi 87,730.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mpango wa elimu bure ulianza kutekelezwa mwaka 2016, hii ina maana kwamba, wale wazazi ambao walikuwa wanashindwa kuwapeleka watoto wao sekondari kwa sababu ya ada, Serikali imefungulia na ndiyo maana leo hii tunaona hata idadi ya watahiniwa wanaofanya mtihani wa kidato cha pili imeongezeka sana. Niwahakikishie Watanzania kwamba, Serikali imejipanga vizuri katika kuimarisha miundombinu katika ngazi zote za elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na changamoto za ongezeko la wanafunzi tumekwishajenga madarasa 1,409 tumeshajenga matundu ya vyoo 3,394 lakini vilevile tumeongeza mabweni kwa ajili ya kuhakikisha kwamba watoto wa kike wanaotoka umbali mrefu wanaweza kusoma katika mazingira ambayo ni tulivu zaidi kwa hiyo, tumejenga mabweni 261.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kutambua kwamba mazingira ni muhimu kwa wananfunzi kujifunza vizuri tunafanya ukarabati wa shule zetu kongwe na mpaka sasa tumekwishaanza ukarabati katika shule 42 kati ya shule kongwe 88 katika nchi hii, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba shule zote kongwe nchini zitafanyiwa ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumeboresha miundombinu katika vyuo vyetu vya ualimu na tunaendelea kufanya hivi. Sasa hivi ninavyozungumza Vyuo vya Ualimu vya Kitangali, Mpuguso, Ndala na Shinyanga miundiombinu yake inaimarishwa kwa kiwango kikubwa, majengo ya kisasa yanajengwa, hii yote ni katika kutekeleza mpango wa Serikali ambao unalenga kufungamanisha maendeleo na rasilimali watu, ili kufanya hivyo lazima tuhakikishe kwamba tunayo rasilimali iliyobobea katika ujuzi katika kutekeleza mpango wetu wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo Wizara imekuwa ikifanya katika kutekeleza mpango huu ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na msingi ulio imara. Kwa

sababu tunafahamu kwamba nyumba bora inajengwa katika msingi ulio imara, Serikali imekuwa ikiweka kipaumbele katika elimu ya awali kuhakikisha kwamba vijana wanapata utayari wa kuanza elimu ya msingi, tumeendelea kutekeleza Programu ya Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu ili kuwajengea vijana wetu msingi mzuri wa kuweza kupata maarifa wanapokuwa wanaanza darasa la kwaza, la tatu hadi la nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanya hivyo tumekuwa tukitoa mafunzo kwa walimu wa darasa la kwanza, la pili, walimu wa darasa la tatu na la nne pamoja na walimu ambao wanafundisha wananfunzi wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum ambapo tumewanunulia vifaa vya kujifunzia vyenye thamani ya shilingi bilioni 3.6 lakini pia Serikali inaendelea kuimarisha ufundishaji wa sayansi kwa sababu tukipata Wanasayansi wazuri ndiyo chachu muhimu ya kuweza kupata wataalam ambao wanahitajika katika fani mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea pia kuhakikisha kwamba tunakwenda sambamba na utoaji wa elimu ya juu kwa kuimarisha miundominu katika elimu ya juu. Ninapende kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba pamoja na taarifa ya Serikali ambayo niliisoma hapa Bungeni tarehe Tisa pia Bodi ya Mikopo imeendelea kutoa mikopo na wananfunzi zaidi ya 1,775 wamepangiwa mikopo na hivyo kufanya sasa jumla ya wananfunzi ambao wameshapangiwa mikopo kufikia 31,353.

Mheshsimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kwa Wanafunzi ambao hawajapata mikopo lakini wanaona bado wana uhitaji, dirisha la kukata rufaa limefunguliwa leo na litafungwa tarehe 19 Novemba, 2017. Niwaombe na niwaelekeze wanafunzi wote ambao hawajapata mikopo lakini wanaona wana uhitaji mkubwa, watumie fursa hiyo

kukata rufaa na Serikali inaendelea kujiridhisha kama Je, kweli wanafunzi wale waliopangiwa mikopo ndiyo wale ambao wana uhitaji ukilinganisha na wale ambao hawajapata ili kuhakikisha kwamba dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba mikopo ya elimu ya juu inatolewa kwa wanafunzi tu wenye uhitaji kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa inazingatiwa, kwa sababu hiyo tayari nimeagiza Bodi ya Wakurugenzi ya Bodi ya mikopo kupitia jina moja baada ya lingine ili kujiridhisha kwamba je, wale waliopangiwa mikopo ndiyo wenye uhitaji kuliko wale ambao hawajapangiwa, lakini pia kupitia majina yote ya wanafunzi ambao hawajapata mikopo ili kujiridhisha kama kweli hawana vigezo kwa mujibu wa vigezo mbavyo vimewekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie kama nilivyosema, wanafunzi wa elimu ya juu kwamba Serikali inatekeleza sera ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wenye uhitaji tu na hapo Waheshimiwa Wabunge tuelewane kwamba sera yetu ya elimu ya juu ni sera ya uchangiaji. Hatujafikia mahali ambapo Serikali inatoa mikopo kwa wanafunzi wote na ndiyo maana hata Sheria ya Bodi ya Mikopo imeainisha wazi kwamba mikopo itatolewa kwa wanafunzi wenye uhitaji, kazi ya Wizara yangu ni kusimamia na kuhakikisha kwamba wale ambao wanapangiwa mikopo ni wale tu wenye uhitaji na siyo vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kushukuru kwa nafasi na kama nilivyosema tangu mwanzo wakati naanza ninaunga mkono hoja hii na ningeomba Wabunge wote tuiunge mkono kwa sababu ni Mpango ambao ni mzuri sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina.

**TAARIFA**

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na tunashukuru kwa michango ambayo inaendelea kutolewa na Mawaziri wanafanya kazi nzuri, lakini wakati ambapo tulipokuwa tukichangia Mpango huu wa Maendeleo tulikuwa tunazungumzia *issues specific* kwa upande mwingine wa Jamhuri ya Muungano, lakini kadri ya michango inavyoendelea kutolewa naona hakuna *aspect* yoyote. Kwa mfano, eneo la utalii na vilevile eneo la elimu ya juu.

Kwa hiyo, Mheshimiwa naomba kutoa hiyo taarifa kwamba hata Mawaziri nao wanaowajibu wa kujibu hoja zile ambazo tulikuwa tumezitoa na *specific* kwa ajili ya upande mwingine wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, hoja hizo atakuja kuzijibu Waziri mwenyewe mtoa hoja Waziri wa Fedha zote. Tunaendelea na Mheshimiwa Mpina.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi hii. Na mimi ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kunipa dhamana hii ya kuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi na kumuahidi kabisa kwamba nitaitumikia nafasi hii na kuwahakikishia Watanzania wenzangu kwamba nitawatumikia kupitia nafasi hii kwa nguvu zangu zote na kipaji chote nilichopewa na Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni Mapendekezo ya Mpango wetu wa Maendeleo. Waheshimiwa Wabunge wetu wamezungumza mambo mengi sana, lakini ninachotaka kusema kwa sababu haya ni mapendekezo ya mpango, zile *inputs* zao walizozisema tumezichukua ili sasa tuje na Mpango wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa hatujibu sana kihivyo kwa sababu tumepewa ushauri na Waheshimiwa Wabunge ili tukaandae Mpango wenyewe. Hata katika mapitio hapa nimeona kwenye Wizara yangu na wamependekeza mambo

mengi, wamezungumzia suala la bandari ya uvuvi, meli ya uvuvi, umuhimu wa kuwa na viwanda vya kuchakata samaki, umuhimu wa kuwa na viwanda vya nyama, umuhimu wa kuwa na viwanda vya maziwa, haya yote ni *inputs* wametupa ili tukaandae Mpango wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kabisa kwamba kwa moyo mmoja, michango yote ambayo imehusu sekta yangu nimeichukua ili kwenda kutengeneza Mpango wenyewe ambao ndiyo baadae muda utakapofika tutauwasilisha hapa Bungeni na hapo ndipo mtakapoona kwamba tumefanya kufikia wapi zile *inputs* ambazo ninyi mmetuwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo na kwa sababu muda unakuwa hautoshi sana nitoe ufafanuzi wa baadhi ya mambo machache.

Moja, limezungumza sana suala hili la uchomaji wa vifaranga vya kuku 6,400 ambavyo vilikuwa vinasafirishwa kuingia nchini mwetu kutoka Kenya. Tukajaribiwa kulaumiwa sana kama Wizara na kama nchi wakati mwingine kwa kitendo hicho tulichokifanya. Jambo moja tu niseme, hapa tuko Mawaziri pamoja na Wizara yangu tumeapishwa kusimamia sheria na tunatekeleza kwa misingi ya sheria iliyowekwa katika kutekeleza majukumu yetu na kwamba hatuwezi kufanya vinginevyo kwa sababu tukifanya vinginevyo Bunge hili litatuuliza kwa nini tumefanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria yetu ya Magonjwa ya Wanyama Namba 17 ya mwaka 2003 inatoa utaratibu wa namna ya kuingiza kuku pamoja na mazao yake ndani ya nchi. Vilevile kuna mazuio ambayo yalitolewa kulingana na jambo hili. Tarehe 29 Oktoba, 2017 tulipowakamata hao vifaranga, tuliwachoma moto kwa sababu kubwa kwamba tulikuwa na zuio ambalo tulishaliweka toka tarehe 7 Juni, 2006 kwamba kutokana na tishio la ugonjwa wa mafua ya ndege lililokuwepo duniani tulilazimika kuzuia uingizaji wa kuku pamoja na mazao yake na tukawa tumezuia mtu yeyote kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu ndugu aliyeingiza hawa vifaranga kwanza aliingiza kinyume cha utaratibu bila kibali chochote ilikuwa ni *illegal importation*, pili, alitaka kuingiza wale kuku wakiwa hawajakaguliwa. Kwa namna yoyote ile kuingia ndani ya nchi ambako kungesababisha kero kubwa. Kwa mfano, kuku wale wangekuwa wana ugonjwa huo wa mafua ya ndege maana yake tungeua ndege wetu wote walioko hapa nchini, vilevile mafua haya ya ndege yanambukizwa mpaka kwa binadamu tungeweza kuua binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuzungumza kwa urahisi jambo la vifaranga hivi kuwateketeza ukawa unazungumza tu kiurahisi kwamba unajua, sijui mambo gani! Ni lazima tuchukue hatua hizi kali kwanza kwa yule aliyefanya hivyo kuhakikisha kwamba hakuna mtu mwingine ambae atafanya jambo kama hilo, mtaji wake tumeuteketeza maana yake kama ana njia zingine ambazo alikuwa anatumia kuingiza vifaranga nchini hawezi kurudia tena, Watanznaia watuelewe kwamba tunasimamia maslahi ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuku wakifa, biashara Tanzania imekufa ya kuku, Watanzania watakufa kwa mafua ya ndege na kama Watanzania watakufa kwa mafua ya ndege kutokana na uzembe wa Wizara yangu na wale askari au watu waliokuwa wanafanya *inspection* kama wasingewachoma kuku siku ile, ningewafukuza kazi wote siku hiyo. *(Makofi)*

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENTEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Waziri kutokana na kifungu cha 68(8), Mheshimiwa anasema

kwamba waliogopa kwamba wale kuku walikuwa na ugonjwa wa mafua ya ndege, lakini taarifa waliyoitoa muda wote walisema kwamba hawakupima. Hii ni aibu kubwa sana kwa Serikali kufanya mambo kama yale yaliyofanyika kuchoma vifaranga vya watu bila kupima. Tulifikiri hata kama ni Serikali inatekeleza sheria ilipaswa pia Serikali...

**MWENYEKITI:** Ahsante amekusikia. Mheshimiwa Waziri endelea.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema kwamba Bunge hili ndilo ambalo linatunga sheria. Utekelezaji wa sheria hauwezi ukafanyika kama Mheshimiwa Mbunge anavyopendekeza. Sheria ya Magonjwa ya Mifugo, Magonjwa ya Wanyama Na. 17 ya mwaka 2013, Kifungu cha 8(2) kinasema "ni kukamata na kuteketeza" na siyo anavyozungumza yeye. Tumekamata na tunateketeza na tunapelaka salamu Afrika na duniani kwamba lazima wanapotaka kufanya hivyo waangalie sheria za nchi yetu zinasema nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili tunafanya *operation* ya mifugo kutoka nje ya nchi. Ni takribani asilimia 30 ya malisho ya nchi hii yanalishwa na mifugo ya kutoka nje, napo tunalalamikiwa, tumekatana ng'ombe, tumekamata, tumetaifisha na tumepiga mnada. Napenda niwambie watu ambao wanatetea mambo haya, kuna jambo moja tu wanalotaka kufanya...

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa ya mwisho hiyo.

**TAARIFA**

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wadau wa haki za wanyama kwa kweli tumesikitishwa sana na kitendo kile. Sasa kama vifaranga wamechomwa, kwa nini...

**MWENYEKITI:** Kaa chini huna taarifa! *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafanya *operation* ya kuondoa mifugo kutoka nje ya nchi ambao wameingia nchini kinyume cha sheria. Hili pia limelalamikiwa na wakati mwingine wanaolalamika ni watunga sheria za nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa sheria hiyo niliyoitaja Sheria ya Magonjwa ya Mifugo Namba 17 ya mwaka 2013 imeonesha utaratibu wa kuingiza mifugo ndani ya nchi kutoka nchi nyingine. Ukieda kinyume na huo utaratibu umevunja sheria. Sheria hiyo pia inakataza kuingiza mifugo kwa ajili ya malisho. Watanzania wetu sasa ukiruhusu mifugo ile kuingia hapa nchini madhara yake ni nini? Madhara yake unaweza kuleta ugonjwa wa kutoka nchi jirani kuingia hapa nchini. Kwa hiyo, tumekamata ng'ombe wale 1,325 wa kutoka Kenya na sasa hivi tunashikilia ng'ombe wengine zaidi ya 10,000 kutoka Rwanda na Uganda ambao tutawapiga mnada hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafanya hivyo kwa sababu gani, moja, kuhakikisha kwamba tunalinda mifugo ya Watanzania isipate magonjwa, mbili, tunalinda Watanzania wasipate magonjwa kupitia mifugo hiyo,tatu; tunalinda pia malisho ya Tanzania, Tanzania haiwezi ikawa malisho ya nchi za kutoka nje, nne, tunahakikisha kwamba migogoro ya wakulima na wafugaji inayochochewa na mifugo ya kutoka nje inakwisha, tano, kuhakikisha kwamba tunalinda mazingira pamoja na vyanzo vyetu vya maji ambavyo vinaharibiwa na makundi makubwa haya ya mifugo. *(Makofi)*

Kwa hiyo basi, watu wanaojaribu kuhusisha…

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MWENYEKITI:** Nilishasema hakuna taarifa tena kaa chini.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hawajachoma...

**MWENYEKITI:** Nimesema kaa chini.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** ... mahusiano yetu na Kenya pamoja na nchi zingine za jirani wanatakiwa wazingatie mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna ushirika wa uhalifu. Watu wanaoingiza mifugo kutoka nje ya nchi ni wahalifu kwa sababu wamevunja sheria na wale wanaozungumza hivyo ni kwa sababu Waziri wa Mifugo ametangaza. Je, ni Watanzania wangapi wamekamatwa Kenya leo wako *lockup*, wapo wamefungwa kwa kuvunja sheria nani anajua idadi? Nani anajua Watanzania ambao wako Uganda kwa kuvunja sheria leo wako mahabusu, leo wamefungwa nani anajua kuwa Rwanda, Burundi. Hivyo hivyo, mhalifu akija hapa hawezi kutetewa kwa sababu ya ushirika, ushirika wetu siyo wa uhalifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashirikiano yetu yanayoendelea katika nchi za Afrika Mashariki ni mazuri mno, *ecellent.* Mahusiano tuliyonayo na Kenya ni mazuri mno kwa sababu mashirikiano yetu ni ya kisheria, mashirikiano na Uganda yapo kwa sababu ni ya kisheria. Kukamatwa kwa ng'ombe hawa ni wavunja sheria haiwezi kuhusishwa na ushirika wetu, wanashauriwa wahusika kufuata sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri nilipotangaza *operation* hii ya siku saba, Waziri wa Mambo ya Nje alichukua hatua ya kuzijulisha nchi zote kwamba wawaambie watu wao kuondosha mifugo Tanzania kulingana na sheria yao. Ng'ombe wengi waliondolewa, sasa hivi nimesema tuna ng'ombe 10,000 tunawashikilia ambao tutawapiga mnada hivi karibuni lakini mifugo mingi imeondolewa, wale ambao wamekaidi ukweli tutapiga mnada ng'ombe zao bila huruma, *operation* inaendelea na tunaendelea kuwashauri ambao hatujawakata waondoe mifugo yao kwa hiari yao. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, orodha ya majibu ya Mawaziri nane tumekamilisha, tutakuwa na orodha jioni, ataanza Mheshimiwa Mwakyembe, atafuata Mheshimiwa Ummy na ataendelea Mheshimiwa Mwijage.

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae, Katibu.

**NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI- KATIBU WA BUNGE:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**
**KAMATI YA MIPANGO**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae.

Waheshimiwa Wabunge, kama tunavyokumbuka kwamba katika uchangiaji wetu wa hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango ya kujadili Mpango wa Maendeleo ya Taifa, tulishamaliza upande wetu sasa tunaendelea na uchangiaji bado, lakini upande wa Serikali.

Kwa hiyo, tutakuwa na wachangiaji kadhaa halafu baada ya muda siyo mrefu tutamuita Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Fedha ambao kwa pamoja watakuwa na saa moja ili kuhitimisha zoezi letu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa jinsi hiyo nitaanza na mchangiaji wa kwanza ambaye ni Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe atafuatiwa na Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Waziri wa Afya.

Mheshimiwa Mwakyembe tafadhali.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naomba nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini kumsaidia kuongoza Wizara hii ya Habari, Utamaduni na Michezo na vilevile kwa kumteua Mbunge kijana, mchapakazi na mwanamichezo hodari Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza kunisaidia kuongoza hii Wizara.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii na ninampongeza sana Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji kwa kazi nzuri wanayoifanya ya weledi mkubwa na katika Wizara hii nyeti katika maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze kwenye baadhi tu ya michango iliyogusia Wizara yangu ambayo inahitaji ufafanuzi wa kina kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na madai ya Mbunge wa Mbeya Mjini, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, kwamba Mkurugenzi wa Idara ya Habari ambaye vilevile ni Msemaji wa Serikali alitumia kifungu cha 54(1) cha Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari kulifungia Gazeti la Tanzania Daima, kitu ambacho anasema kwamba siyo sahihi, alichotakiwa kufanya si kulifungia gazeti, lakini kuwawajibisha waandishi waliohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madai haya ya Mheshimiwa Mbilinyi yanagusia utekelezaji mzima wa sheria hii mpya, hivyo nafikiri kuna umuhimu sana wa kutoa uchambuzi wa kina kidogo kuhusu sheria hii na hapa tulipofika ili tusiendelee kuwachanganya wanaotusikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbushane kidogo tu kuwa Sheria hii ya Huduma za Vyombo vya Habari tuliipitisha wenyewe hapa Bungeni tarehe 5 Novemba, 2016 na tarehe 16 Novemba, 2016 Mheshimiwa Rais akaridhia hii sheria na tarehe 31 Desemba sheria hii ikaanza kutumika rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kurahisisha na kuwezesha utekelezaji wa sheria hii uende vizuri zaidi ikabidi tutengeneze Kanuni na kanuni zenyewe pia zikawa tayari na tarehe 3 Februari, 2017 zikaanza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nielezee hili wanisikilize vizuri hata wadau katika masuala ya habari vizuri kwa makini kwamba chini ya sheria hii na kanuni zake kuna vyombo vikuu vinne vya kusimamia uendeshaji na maendeleo ya vyombo vya habari hapa nchini ambavyo vinatakiwa viundwe. Kwanza ni *Independent Media Council of Tanzania* ambalo ni Baraza Huru la Habari ambalo linaundwa na wanahabari wenyewe, lakini ni wanahabari ambao ni *accredited* walishapata ithibati. Chombo cha pili kilichotakiwa kuundwa hapa ni Bodi ya Ithibati yenyewe *(Accreditation Board).* Kwa sababu tulishakubaliana kwamba Uandishi wa Habari sio kitu cha kubahatisha tena ni taaluma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama zilivyo taaluma zingine lazima kiwepo chombo kinachofuatilia *training* ya uandishi, weledi wao na nani atambuliwe kuwa mwandishi wa habari ndiyo maana tuna chombo hicho kinaitwa chombo cha ithibati *(Accreditation Board)*. Tatu ni Kamati ya Kimahakama ya malalamiko ambayo kazi yake kubwa ni kusikiliza malalamiko ya wananchi kama kuna upotofu wa maadili, kama mtu ameonewa na hicho chombo kitakuwa na mamlaka kama ya Mahakama, ndiyo maana ukiona

hujaridhika unakwenda Mahakama Kuu kudai kwamba haki yako kwa kweli imefinywa, pengine hukusikilizwa vizuri ama kuna uvunjifu wa hizi kanuni tunaita *principles of natural justice.* Kwa hiyo, hicho chombo ni *Quasi Judicial Board,* ni *almost* kama Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chombo cha nne ni Mfuko wa Habari ambao kazi yake kubwa ni kuandaa waandishi wa habari vizuri zaidi waweze kupata weledi katika kazi na vilevile kufanya utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasema hayo yote kwamba dhamira ya sheria hii ilikuwa nzuri sana, kuwa vyombo hivi vinne vikifanya kazi vizuri kwa kushirikiana, sio tu vyenyewe vilevile na Serikali na kwa kuzingatia maadili na sheria za nchi, basi tasnia ya habari ingeweza kujiendesha wenyewe kwa kweli bila mtu yeyote kuvisogelea Vyombo vya Habari, hilo ndilo lilikuwa lengo la sheria.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kuna swali limekuwa linaulizwa mpaka kwenye Kamati kwamba, vyombo hivyo ulivyovitaja mbona havijaanza kufanya kazi mpaka leo? Ndiyo ni kwa sababu kubwa mbili, sababu kwanza tumeanzisha usajili mpya wa majarida na magazeti yote, tatizo moja ni kwamba hatujapata ushirikiano mzuri kutoka kwa wadau wenyewe, tumeahirisha zaidi ya mara tatu *deadline* ya usajili. Mwisho tumekuja kusajili tarehe 31 Oktoba ambazo ni wiki mbili tulizopita na ni robo tu ya majarida na magazeti yaliyoandikishwa. Tumefungua milango wanaweza kuendelea kujiandikisha. Kwa hiyo, hatuwezi kupata idadi ndogo ya wadau hao tukaanzisha vyombo hivi muhimu kesho utaambiwa Serikali imelazimisha hivyo vitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili tukumbuke kwamba kuna uwepo wa kipindi cha mpito *(transition period)* katika hii sheria, yote ilitokana na hoja za Wabunge hapa. Wabunge wanasema hatuwezi kuwawajibisha waandishi wa habari kwa sababu kazi ya uandishi wa habari ni kazi nzito ya kutafsiri mtu amesema nini, anakaa kwenye chumba cha habari, unahitaji elimu *at least basic education* ambayo tukubaliane

hapa. Ndiyo maana wote tukasema tunaiga na nchi zingine kama Uganda ambapo lazima uwe na *degree* mbili, tukasema lakini hapa angalau uwe na Diploma au Shahada ya Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge mkasema tuwape miaka mitano tusiwe *unfair* kawa hawa watu tukatoa miaka mitano, wenzetu wajipange vizuri waingie ili waweze kuwa *accredited* kama waandishi wa habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake ni kwamba utekelezaji mzima wa uanzishwaji wa vyombo hivi vinne unachelewa mpaka pale wadau wenyewe haitokuwa Serikali, wadau wenyewe walisema pale *to speed up,* tuko tayari hata tukaanzisha kesho *Media Council* na wale waandishi wenye shahada na wenye diploma wanatosha hao waliopo, tukifanya hivyo kama Serikali itakuwa na mgogoro mkubwa. Kwa hiyo, tunasubiri wadau wenyewe watuambie muda umefika tuitekeleze hiyo sheria sasa tuepukane na *transitional period,* hiyo hatuwezi kuamua kama Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana namjibu Mheshimiwa Mbilinyi kwamba Mkurugenzi wa Habari hajawahi hata siku moja kulifungia gazeti lolote kwa chini ya sheria hii mpya na wala hajawahi kutumia hicho kifungu cha 54. Kifungu cha 54 kinatoa ufafanuzi tu wa kosa la kuchapisha habari za uongo na kuitia jamii katika hofu. Madaraka anayoyazungumzia Mheshimiwa Mbilinyi ni madaraka ya Waziri nilitaka nilieleze hili. Pamoja na sheria hii kuunda vyombo vinne ambavyo vitaweza kabisa kuleta pengine nidhamu kama kweli Watanzania tutaamua kutumia vyombo hivi kuheshimu kanuni na maadili ya nchi, kuna kitu kinaitwa *residual powers of the government,* hizo *residual powers* hatujanyanganywa na hii sheria ningeshangaa sana tungenyanywa na hii sheria. Duniani kote Serikali lazima iwe na *residual powers* kuhakikisha kwamba inalinda haki za watu wake na pili inalinda usalama wa nchi hizo lazima tuwe nazo, hata kama kuna vyombo vingine

vinafanya hiyo kazi. Sasa hayo madaraka yamo katika sheria mpya katika kifungu cha 59 ndiyo ambayo Waziri anatumia. Ukiona *trend* ya gazeti toka siku ya kwanza unaionya, siku ya pili unaionya, siku ya tatu unamwambia bwana eeh, unaleta uchochezi mara ya sita unaonya unasema aah, pengine ukapumzike miezi mitatu utafakari vizuri, ndiyo hicho tunachofanya ili kulinda mstakabali wa nchi yetu hii.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo hatuyafanyi Tanzania tu iko dunia nzima na tunafanya kwa kuzingatia matakwa ya Mkataba wa Kimataifa tulioingia Watanzania *International Covenant on Civil Political Rights* ya mwaka 1966, sisi ni *signatories* dunia yote ni *signatories* na kila nchi imechukua hayo maudhui yako kwenye Ibara ya 19 ya huu mkataba na sisi tumechukua tumeingiza kwenye Katiba yetu Ibara ya 18 na Ibara ya 30 kwamba hata kama una haki, hata kama una uhuru, uhuru huo lazima uwe na mipaka kwa ajili ya maslahi ya nchi. Mipaka lazima iwepo na hata hii sheria imeingizwa katika kifungu cha 59 kwamba pamoja na kuwaachia mjiendeshe yanapokuja maslahi ya Taifa, inapokuja kulinda usalama wa nchi, lazima Serikali iwe na sauti hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kitu kimoja Mheshimiwa Saada Mkuya naye aliongelea kuhusu ujenzi wa mazingira wezeshi ya michezo kuitangaza nchi kimataifa. Nampongeza sana Mheshimiwa Saada Mkuya kwa kuja na hilo wazo, ni wazo zuri sana. Sasa hivi tunamalizia utengenezaji wa rasimu ya Sera ya Michezo ya Taifa mpya, imefika mbali sana, nina uhakika ndani ya miezi sita tutakuwa sera mpya ya michezo hapa Tanzania. Hata kabla hiyo sera haijakamilika tumeshaanza kutekeleza, kuhakikisha kwamba tunatumia michezo kuitangaza nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu mapema tumeweza kuleta timu ambayo iko kwenye *Premier League* ya Uingereza iitwayo Everton, kuja kucheza kwenye uwanja wetu wa kisasa hapa kitendo hicho tu peke yake kimeweza kuinyanyua Tanzania katika macho ya ulimwengu na ndiyo maana tukaweza kupata hata ufadhili wa kutengeneza

kiwanja chetu upya na nitakabidhiwa nafikiri tarehe 24 na mwenzangu Naibu Waziri kikiwa na nyasi ambazo zitakaa kwa zaidi ya miaka kumi bila kutusumbua tena ama kupata ugojwa wa moyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo asubuhi nimeingia kutoka Arusha baada ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuniruhusu kwenda kufunga michezo ya *golf*. Naomba nimshukuru tena Mheshimiwa Dkt. Mpango na mwenzake Mheshimiwa Dkt. Ashatu kwa kutoa pesa kuelekeza kwenye mahitaji ya barabara, hii barabara kwenda Arusha imekamilika. Hii *shortcut* kwenda Arusha nimetoka Arusha saa 11 asubuhi nimewahi kipindi asubuhi, hayo ndiyo maendeleo Mheshimiwa Mpango hongera sana, Mheshimiwa Kijaji hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikwenda Arusha kufunga mashindano ya *golf* ambayo yamevutia wacheza *golf* wa kimataifa wa mataifa 250. Nampongeza sana mwekezaji wa Arusha ambaye amejenga kiwanja cha *golf* ni Mholanzi Mtanzania wamejenga kiwanja cha *golf* cha kisasa kupita vyote katika Afrika ya Mashariki na Kati. Wamekuja wageni wengi na ndiyo maana tumekubaliana na Mheshimiwa Waziri wa Utalii hapa tufanye kazi kwa karibu sana kwa sababu michezo sasa hivi na utalii vinaenda pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wote duniani michezo ya *golf* inachezwa na matajiri, kwa hiyo, ukivisogeza karibu na mbuga za wanyama unapata watu wazito kweli. Nimepishana tu juzi na mcheza sinema mashughuli wa Marekani Harrison Ford amekaa hapo akicheza *golf* wiki nzima, siyo yeye tu wengi wanakuja. Ndiyo maana naomba nitoe wito kwa viongozi wenzangu hasa huku kwenye Wilaya kama kulikuwa na kiwanja cha *golf* zamani naomba msivigeuza kuwa magulio, maana kulikuwa na imani kwamba hii michezo ya *golf* siyo yetu, hapana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijana aliyeshinda *golf tournament* ya kimataifa ya Arusha jana ni kijana wa Kitanzania kwa jina la Victor Joseph na ni mwanafunzi, mtoto

wa kawaida tu. Unajua hawa vijana ambao hawajawahi kucheza *golf* Mungu amewapa kipaji cha ajabu, anapiga tu mara moja anaingia moja kwa moja kwenye shimo utafikiri Tiger Woods! Tiger Woods wapo wengi, naomba ndugu zangu tutenge maeneo kwa ajili ya kujenga viwanja vya kisasa vitatusaidia. Ukinipa tu eneo nitatafuta Wawekezaji kama ambavyo tumefanya upande wa Arusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema naunga mkono hoja hii kwa nguvu kweli. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Nakushukuru sana kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, mmemsikia Waziri? Chezeni *golf,* tatizo hapa Dodoma uwanja wa *golf* hamna! Tulikuwa tuwe na mashindano ya Afrika Mashariki ya Mabunge yote lakini inabidi yahame kwa sababu tu Dodoma hatuna uwanja wa *golf*. Kwa hiyo, hoja yake bado iko pale pale, *golf* ndiyo mchezo wa watu wa aina yenu*.* Ahsante sana Mheshimiwa Mwakyembe. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, nimkaribishe Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Mheshimiwa Ummy Mwalimu, tafadhali.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, kwa kuniamini kusimamia sekta hii ya afya na maendeleo ya jamii, nimhakikishie Mheshimiwa Rais nitashirikiana na Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndungulile, Naibu Waziri ili kuhakikisha Watanzania wanakuwa na afya njema na hivyo kuweza kushiriki katika kujiletea maendeleo yao na maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Mpango na Naibu Waziri kwa kazi nzuri

wanayofanya katika eneo hili la uchumi na fedha lakini hasa kwa kuleta mapendekezo ya mpango wa maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa maoni na ushauri walioutoa hasa katika kuboresha upatikanaji wa huduma za afya nchini, ikiwemo kujenga jamii ya Watanzania inayojali na kuheshimu haki, ustawi na maendeleo ya wanawake, wazee na watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge lakini nitajikita sana kwa Dada yangu Mheshimiwa Susan Kiwanga. Niliposikiliza mchango wake nikasema hivi huyu amesoma huu mpango au amesoma hajauelewa? Kwa sababu anasema kwamba mipango yetu haizingatii mahitaji halisi ya Watanzania. Unasema hivi huyu anazungumzia Watanzania gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Mheshimiwa Dkt. Mpango ataeleza uhusiano mkubwa sana kati ya ujenzi wa uchumi wa viwanda na maendeleo ya watu, ikiwemo kuboresha afya, ikiwemo elimu, ikiwemo vijana na kila kitu. Lakini nataka ni-*summarize* kwa kitu kimoja, maendeleo ya watu, maendeleo ya jamii, msingi wake mkubwa ni maendeleo ya kiuchumi. Dkt. Mpango na timu yako songeni mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua Tanzania ya viwanda ndani ya huu mpango ni halisi. Maana nimesoma hotuba yao wanasema Tanzania ya viwanda uhalisia au ndoto? Ni uhalisia! Tunasonga mbele wame-*panic* ndiyo maana sasa wanatafuta sababu zisizo na maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ndiyo maana nasema amesoma? Ukiangalia ukurasa wa 51, Mheshimiwa Mpango na timu yake wanasema kufunganisha maendeleo ya viwanda na maendeleo ya watu, sasa niache nimuoneshe kwenye sekta ya afya, wananchi wa Mlimba wanataka nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mlimba hawataki bora huduma, wanataka huduma bora za afya. Mheshimiwa Mpango katika kitabu hiki anasema kwamba kuboresha upatikanaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba. Huu ndiyo Mpango! Sasa namshangaa Mheshimiwa Susan Kiwanga, kabla ya Serikali ya Awamu ya Tano haijaingia madarakani Ifakara walikuwa na fedha za dawa shilingi milioni 19 tu, mwaka jana tumewapa shilingi milioni 120 za dawa, mwaka huu tunawapa shilingi milioni 164, halafu anasema Mpango huu haujazingatia mahitaji ya wananchi. Najiuliza, Dkt. Mpango mimi naunga mkono hoja kwa sababu najua hata huko Mlimba, Ifakara tutaongeza fedha zaidi ya hizi ambazo umeweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili unajiuliza anasema siyo vipaumbele vya Watanzania. Unajiuliza, Watanzania wanataka nini? Watanzania wanataka wote tutibiwe Muhimbili siyo nje ya nchi. Mheshimiwa Dkt. Mpango anatuonesha hapa kwamba ataboresha huduma za matibabu ya kibingwa. Ndiyo maana nimesema ni kuchanganyikiwa, wanaona tunasonga mbele. Nitoe mfano, Watanzania tutatibiwa Muhimbili, nataka kutoa mfano Hospitali ya Taifa ya Muhimbili pale *ICU* tumeongeza vitanda vya wagonjwa mahututi kutoka 21 mwaka 2015 hadi vitanda 75. Tumeongeza vyumba vya upasuaji Muhimbili kutoka vyumba 13 hadi vyumba 20. Watu walikuwa wanasubiri miaka miwili kufanyiwa upasuaji. Sasa hivi watu wanasubiri miezi minne na tunategemea kushusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upasuaji wa watoto, Muhimbili walikuwa wanafanya upasuaji wa watoto 15 kwa wiki, sasa hivi wanawafanyia watoto 50 kwa wiki. Mheshimiwa Dkt. Mpango anasema haya ni mapendekezo, nataka kuboresha huduma za matibabu ya kibingwa. Sasa unasema mpango huu haujazingatia mahitaji halisi ya wanananchi. Unajiuliza hivi huyu kweli anazungumza anachokijua kweli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutoa mfano mwingine. Watanzania wanataka nini kama nilivyosema?

Watanzania wanataka wote wapate huduma za matibabu ya kibingwa. Tumeanza, kuna wazazi wana watoto wana matatizo ya kutosikia, Muhimbili leo wamepandikiza vifaa vya kusikia *cochlear implants,* Mtanzania gani wa kawaida ataweza kutumia shilingi milioni 80 mpaka shilingi milioni 100 kwenda China? Lakini Muhimbili watapata Watanzania wote!

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari njema, wasiwe wanasema tu, habari njema ni kwamba kabla ya tarehe 30 Desemba, tunaanza upandikizaji wa figo. Watanzania wanataka kuona huduma za matibabu ya kibingwa wote wanapata na siyo wenye fedha, huduma hizi zitapatikana nchini, Dkt. Mpango hongera sana nakuunga mkono kwa mpango huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nani alikuwa anafahamu upasuaji lazima watu wapelekwe India? *Jakaya Kikwete Cardiac Institute* ilikuwa inapasua mgonjwa mmoja kwa siku, leo wagonjwa watatu kwa siku. Watanzania wote wanapata huduma hizi. Haya mambo ni kuanzia mwaka 2016 mpaka leo ndani ya miaka miwili mambo makubwa sana yamefanyika katika kuboresha sekta ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa nasema hivi huyu anasoma nini? Watanzania wengi wanapata matatizo ya saratani. Zamani unaenda pale *Ocean Road,* wana vitanda 40 tu kwa ajili ya huduma ya saratani ya maji *(chemotherapy)* leo kuna vitanda 100, wagonjwa 100 wanatibiwa kwa wakati mmoja. Mheshimiwa Dkt. Mpango nashukuru kwamba tunaenda kununua kifaa kinaitwa *PET scan* kwa ajili ya tiba ya uchunguzi na uchunguzi wa matibabu ya saratani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nashangaa hivi huyu, lakini ninamshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Bobali ametoa mchango mzuri, jamani wagonjwa wengi wa saratani wanaongezeka. Mna mpango gani wa kuongeza elimu? Huu ndiyo mchango ambao ninauona una lengo la kujenga. Siyo mchango wa kusema hakuna

vipaumbele. Kaka yangu Bobali nakushukuru sana. Nataka kukuhakikishia tutaendelea kutoa elimu juu ya wananchi kujikinga na saratani na tulichokifanya sasa hivi, tumeongeza pia vituo vya kuwezesha hasa wanawake kwa sababu saratani kubwa inayoongoza ni saratani ya mlango wa kizazi kwa asilimia 34 na saratani ya matiti asilimia 12. Kwa hiyo, Serikali ya Awamu ya Tano imeongeza vituo vya kuwezesha wananchi kupima kutoka 343 hadi 443, haya ndiyo wanayotaka Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie jambo la mwisho, anazungumzia afya ya mama na mtoto wananchi wanakufa, tunajua. Lakini hivi ukijenga tu majengo ndiyo watu watapona? Sisi tumejikita kwenye kuboresha kwanza huduma. Tumesema kama kweli hiki ni kituo cha afya tunakitaka kiwe kituo cha afya na ndiyo maana kupitia Awamu ya Tano, wakati Mheshimiwa Dkt. Magufuli hajaingia madarakani, vituo vya afya 500 vya Serikali ni 109 tu vinavyotoa huduma za uzazi za dharura ikiwemo upasuaji. Mwaka wa pili wa Magufuli tunaongeza vituo 170 na Waheshimiwa Wabunge mmepata barua. Hii ndiyo tunataka, lakini kwa nini wanawake wanakufa? Kwa sababu pia wanavuja damu, wana upungufu wa damu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Mpango anatuambia anataka kuongeza upatikanaji wa dawa na chanjo. Sasa hivi chanjo, dawa za uzazi salama *(Oxytoxin)* kwa ajili ya kuzuia mwanamke kuvuja damu *magnesium sulphate* kwa ajili ya kuzuia kifafa cha mimba na *phehol* kwa ajili ya kuongeza damu zinatolewa bure! Hii ndiyo wananchi wa Mlimba wanataka. Najua Mheshimiwa Jafo ataongelea ujenzi wa zahanati na vituo vya afya, lakini sisi tumejikita hizo huduma zilizokuwepo ziwe ni huduma bora siyo bora huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, anasema siyo vipaumbele vya wananchi. Labda Dada yangu Mheshimiwa Susan Kiwanga wewe na familia mna hela, lakini Watanzania nikikutwa *HIV positive* nianze dawa mara moja. Tumeanza Sera ya *Test and Treat.* Mtanzania yeyote atakayepima na

kukutwa na maambukizi ya virusi vya UKIMWI anapata dawa siku hiyo hiyo tunamwanzishia, halafu anasema Mpango huu haujazingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namaliza la mwisho, Mheshimiwa Susan Kiwanga; *TB* kabla Mheshimiwa Magufuli hajaingia madarakani kulikuwa na kituo kimoja tu cha kutoa matibabu ya *TB* sugu, *Kibong'oto Hospital.* Leo tuna vituo 18 ikiwemo Ifakara, ikiwemo Ifakara kituo cha Kibaoni. Halafu mtu anauliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha Dkt. Mpango nakuunga mkono kaka yangu, Naibu Waziri na wataalam wote wa sekta ya fedha. Endeleeni, mkisikia watu wanasema sema wame-*panic* kwa sababu wanajua Tanzania ya viwanda inafikiwa. Kwangu tukifikia Tanzania ya viwanda najua maendeleo ya sekta ya afya yanafikiwa na Watanzania watakuwa na afya bora na ustawi na hivyo kushiriki katika kujiletea maendeleo yao na maendeleo ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ummy Mwalimu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, nakushukuru sana kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwa siku nne na nusu sisi tulikuwa tunachambua Mpango, sasa hivi tunapata ufafanuzi na mchango zaidi wa Mpango. Kwa hiyo, tutulie tupate mchango sawasawa halafu Waziri mwenyewe atahitimisha. Hawa wengine wote wanachangia mpaka sasa. Mheshimiwa Waziri usisahahu alizungumza habari ya saratani zile za akina mama na nini, sasa nikawaza nikasema asisahau pia na ile saratani ya wanaume sijui inatwa tezi nini sijui ile?

**WABUNGE FULANI:** Tezi dume.

**MWENYEKITI:** Mmh, mMaana imekaa pabaya sana ile,

usitusahau na sisi. Mheshimiwa Charles Mwijage, Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji tafadhali. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa ya kuchangia Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2018/2019, awali ya yote nitoe shukrani na pongezi kwa Mheshimiwa Rais kumaliza miaka miwili na nimshukuru kwa kuendelea kuniamini nipige filimbi ya ujenzi wa Tanzania ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Waziri wa Fedha na Mipango na Naibu wake kwa mpango mzuri ambao ninauafiki. Kwa sababu sitaki kufanya kazi ya kuwasomea watu, kila Mbunge anapaswa kusoma, nitatoa ufafanuzi kidogo juu ya mambo ambayo watu wanayaelewa ndivyo sivyo.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kukariri dhima ya mpango wa pili wa miaka mitano. Dhima ya mpango wa pili wa miaka mitano ni ujenzi wa uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu. Rafiki yangu Mheshimiwa Ummy amezungumzia maendeleo ya watu ambayo yanajikita kwenye elimu, yanajikita kwenye afya, yanajikita kwenye kipato. Sasa mageuzi ya kiuchumi, huu mpango ambao nauunga mkono ni sehemu ya ule mpango mrefu wa miaka mitano ambayo naiunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda tunavyovilenga, nimesikia hoja watu hawajajua mpaka leo viwanda tunavyovijenga. Sitaki kuwasomea watu lakini kwa faida, viko viwanda vya makundi manne na vyote tumevishughulikia. Kundi la kwanza ni viwanda vinavyochakata mazao au malighafi ya wananchi, katika kuhamasisha ni jukumu la viongozi wote na wananchi wote, ninapopiga filimbi nawategemea na ninyi Waheshimiwa Wabunge tuendelee kuhamasisha zile malighafi tuzijengee viwanda.

Kundi la pili ni viwanda ambavyo vinaajiri watu wengi. Yupo Mheshimiwa Mbunge ameniambia kwa nini usilete viwanda vya teknolojia ya juu, hapana! Watanzania wote hawawezi kuendesha mitambo ya teknolojia ya Juu, Watanzania wote hawawezi kuendesha *LNG Plant,* kwa hiyo, nitaendelea kutengeneza viwanda vinavyoajiri walio wengi ili kusudi wale wenzangu na mimi ambao waliishia darasa la saba na darasa la kumi waweze kutumika pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kundi la tatu ni viwanda ambavyo malighafi zake, bidhaa zinazozalishwa zinatumika sana. Katika kundi hili tumefanya vizuri sana katika viwanda ambavyo nilianzisha. Tuna uwezo uliosimikwa wa kuzalisha saruji tani milioni 10.8, tunatumia mahitaji yetu tani milioni 4.87 kwa hiyo tuna uwezo wa kuzalisha kuliko ambavyo tunahitaji kama nchi. Tuna mahitaji sasa ya kujenga viwanda vya tani milioni 10 Sinoma Tanga lakini kuna viwanda vinakuja Chalinze, Mamba na mwenzake Nyati wanaweka viwanda vya tani milioni tatu pale. Kwenye hiyo *industry* ya bidhaa zinazotumika sana tumefanya vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kundi la nne ni kutumia malighafi ambazo tumepewa faida na Mwenyezi Mungu ya kipekee ndiyo inaangukia suala la viwanda vya mbolea inayotumia gesi. Niwaeleze Waheshimiwa Wabunge mmelizungumza, Ferrostaal ameshapewa *clear line* na Wizara ya Nishati kwamba atengeneze mbolea. HELM ya Mtwara na ninyi njooni mjadiliane tuko tayari mzalishe mbolea. Tunapojenga *Bagamoyo Special Economic Zone* viwanda 190 kiwanda kimojawapo kitakuwa cha kutengeneza mbolea. Kwa hiyo, hivyo ndivyo viwanda tunavyoshughulikia. Sasa uhamasishaji ni jukumu lako mimi nikiwa nimetangulia kusudi tujenge Tanzania ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio tuliofanikiwa, tumepata mafanikio. Fanikio moja kila Mtanzania sasa anaimba viwanda. Nchi yote watu wanaimba viwanda na nilifikiria wakati huo nitoe dhana ya isiyokuwa. Unapozungumza Watanzania, kwa mfano viongozi

tunazungumza Watanzania kuanzia ngazi ya kwanza ngazi ya juu, ndiyo maana mimi kiwanda kidogo hata vyerehani vinne naendelea kusema ni viwanda vidogo. Kwa hiyo, usijitambue wewe nafasi yako kwa sababu unazo, lazima tuwalee Watanzania wadogo mpaka wale Watanzania wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa faida ya yule aliyeuliza swali, viwanda vidogo sana vinaajiri mtu mmoja mpaka wanne na *capital* yake ni shilingi milioni tano. Cherehani *industrial* kinauzwa shilingi milioni 3.5 na kinaweza kukutengeneza kipato cha kukutosha wewe na familia yako. Vipo viwanda vidogo vinaajiri watu watano mpaka 49 na mtaji wake ni shilingi milioni tano mpaka shilingi milioni 200. Hivi ndiyo vile viwanda vya kuchakata nyanya, viwanda vya pilipili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna viwanda vya kati vinaajiri watu 50 mpaka 99, vinaanzia shilingi milioni 200 mpaka shilingi milioni 800. Kuna viwanda vikubwa milioni 800 na vinaajiri watu 100 na kwenda zaidi. Hiyo ndiyo naihubiri kwa Watanzania walio wengi. Nikienda kwa wale wenye nazo; kiwanda kidogo wanasema ni shilingi bilioni mbili lakini tunahimiza viwanda vidogo na ukisoma Mpango wa Mheshimiwa Mpango anakuambia *SIDO* itapewa kipaumbele cha kuongoza katika ujenzi wa viwanda, kwa sababu tunatambua kwamba wananchi walio wengi wataweza kupata faida kwa kushiriki katika kuchakata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaeleze Waheshimiwa Wabunge katika ujenzi wa viwanda sekta inayoongoza ni ya uchakataji *(manufacturing)* wanaita *mediating sector,* tunataka tuwalee Watanzania watoke katika uchuuzi wawekeze katika kuchakata katika kutengeneza viwanda. Pale ulipo, uangalie zile *factor* zinazokuwezesha uweze kwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma ule mpango wa pili wa miaka mitano nafasi ya sekta binafsi ndiyo mhimili kwa hiyo msitegemee Serikali ihamasishe, sekta binafsi ihamasishe,

ni jukumu lenu ni jukumu langu na sekta binafsi ndiyo itafanya hayo mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala ambalo kuna watu wamedokeza nawaheshimu sana rafiki zangu, nitawapiga taratibu. Watu wanasema kwamba Serikali haina mahusiano mazuri na sekta binafsi. Hamna taarifa, Serikali inakutana na sekta binafsi na jana wanaosikiliza taarifa za kiingereza katika kipindi cha *This Week In Perspective* wamesema wenyewe watu wa *Tanzania Private Sector* waliokuwa pale kwamba mahusiano ni mazuri sana mpaka Mheshimiwa Rais anawaita wafanyabiashara anazungumza nao. Ila ni kwamba kuna *paradigm shift,* mambo yamebadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatengeneza viwanda ili moja; tutengeneze ajira, tunatengeneza ajira, mbili; tuzalishe bidhaa zenye ubora kusudi tuweze kutosheleza mahitaji ya Watanzania na kuuza nje. Lakini tunatengeneza uchumi wa viwanda na viwanda ku-*broaden* ile *tax base.* Mwisho yote haya mawili ukiyatengeneza utakwenda vizuri. Lakini mwisho lazima umuone Mzee wa mpango uweze kumpa chochote. Kilicho cha Yesu mpe Yesu na cha Kaisari mpe Kaisari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie masuala maalum. Limezungumzwa suala la Mchuchuma na Liganga. Amezungumza Mheshimiwa Mpango, Mchuchuma na Liganga naisimamia mimi na ni suala la muda. Ile sheria mliyoibadilisha Bungeni ya kuhusu rasilimali zetu tupate kiasi gani inahusu Mchuchuma na Liganga. Nikishamaliza mambo yangu, mwekezaji tayari ana pesa ya fidia anaanza na kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *EPZA* watu wanasema tunatumia utaratibu ambao hautumiki dunia nyingine, ndiyo! Mambo mengi tunayofanya Tanzania hayatumiki sehemu nyingine, kama la kuwakoromea wale watu wa makinikia, Marais wachache wanaweza kuwakoromea, kwa hiyo, kuna mambo ni ya kwetu kwetu tu! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachofanyika kwenye *EPZA,* tumekubaliana na wawekezaji wa Bagamoyo waje walipe fidia tutengeneze ile *Bagamoyo Special Economic Zone. Bagamoyo Sepcial Economic Zone* Januari inaanza na nitatengeneza viwanda 190 kwa kuanzia. Tutaharakisha viwanda hivi mwaka 2020 viwe vimeanza. Mwaka 2020 kuna shughuli lazima nihakikishe kwamba viwanda vile vipo ili kusudi niweze kuonesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee. Suala lingine *specific* la uhusiano kati ya sekta ya kilimo na viwanda. Waheshimiwa Wabunge, Serikali (mimi ndiyo napiga filimbi) lakini siwezi kufanya kazi bila kilimo, bila mifugo, bila TAMISEMI, bila miundombinu na miundombinu wezeshi ndiyo maana nahitaji umeme, nahitaji maji, nahitaji reli, nahitaji barabara. Ukijumlisha hayo ndiyo yanaitwa uchumi wa viwanda halafu mimi nakuja najenga viwanda.

Kwa hiyo, wanaosubiri milingoti ya viwanda ukiona reli inajengwa, viwanda vinakuja. Ukiona mabomba ya maji viwanda vinakuja, ukiona umeme unavutwa viwanda vinakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo mahusiano. Serikali ihakikishe upatikanaji wa soko la mazao. Hapa ndipo kuna kazi. Nimei-*position* kwa maelekezo ya Mheshimiwa Waziri, nai-*position* Wizara yangu. Wizara yangu imepewa *mandate* mpya ya kuhakikisha tunatafuta masoko ya mazao, yawe kilimo, yawe wapi ni kazi yangu mpya katika hii awamu mpya kuhakikisha ninapata soko la mazao na nitatoa mwongozo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanda vya kuchakata mazao nimelizungumzia katika zile sekta tatu, watu wanauliza mbona nyama haijazungumzwa? Katika mazao ya wananchi mifugo ni mazao ya wananchi ndiyo viwanda *category number one.* Viwanda vya mbolea vya Ferrostaal na HELM nimevizungumzia ni kiasi cha kusubiri vinakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhamasishaji nimezungumza ni jukumu la sisi wote. Viwanda vilivyokufa tunavifufua na hakuna mjadala. Atakayeshindwa ampe mwenzake na tunahakikisha suala hilo tunalifikiria. Ukisoma *Vision 2020* inaelezea kwa nini tulishindwa lakini ukisoma Mpango wa Pili unakueleza kwa nini hatutashindwa. *Import substitution come export promotion* ni mojawapo ya hatua nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie sekta ya sukari na nizungumze kuhusu Mheshimiwa Mchengerwa. Wale wawekezaji wako watatu siku zao zimehesabiwa, hatutaki watu kuatamia maeneo ya ardhi. Tutashirikiana Wizara ya Ardhi na ile ya Kilimo kuhakikisha kwamba tunazalisha sukari ya kutosha. Watu wa *SADC* wametusaidia kupata uwezo wa kuzalisha sukari bila kuingiliwa. Tanzania tuna uwezo wa kuzalisha tani milioni mbili kwa mwaka kwa kutumia mabonde yetu yote yaliyopo. Mheshimiwa Rais alipokuwa Kagera ametoa *ultimatum* kwa wenye viwanda waongeze uzalishaji na hilo mimi nalisimamia. Kwa hiyo, msiwe na wasiwasi tutazalisha sukari lakini uzuri wa sukari uzalishaji wa sukari unatengeneza ajira nyingi. Kwa hiyo, Kigoma kwetu kule nitapeleka viwanda viwili kusudi watu wa Kigoma badala ya kwenda mbali mkate miwa kwenu na mambo yawanyokee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utendaji wa Wizara nimeshazungumzia naipanga upya, lakini jukumu la *SIDO* kwenye mpango ndiyo inatangulia na niwaambie naanza na Mkoa wa Geita, Katavi, Simiyu, kote huko naweka ma-*shade* mpya. Kwa hiyo, nataka kuwaonesha tunatengeneza *shade,* dada tulia na Kagera nitaweka, tunatengeneza *shade* ambazo mtu unachakata unakwenda pale, ma-*shade* ninayokujanayo ni mapya, unapewa *shade,* unafundishwa na namna ya kuchakata, ukihitimu unatoka na kitu chako. Ni miaka miwili, mwaka wa tatu mtaona wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitambue mchango wa Mheshimiwa Saada. Na mimi nitazungumza na *counterpart* wangu wa Zanzibar namna ya kuweza kuchakata ile karafuu kuiongezea ubora. Napenda kutumia fursa hii kuwaambia

kwamba watumie wataalam wangu, *SIDO* tutaiongezea uwezo iweze kufanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nizungumzie mchango wa Mheshimiwa Mbowe, aliyezungumza kwamba hatuna sera na kwamba tutengeneze sera moja, huwezi kutengeneza sera moja, sera zote zilizopo ni nzuri. Ile mnayoiita *fast tracking* ni kuharakisha na *fast tracking strategy* maana yake ni nini, ni kuondoa vikwazo. Tunayo hiyo na tunayo *blue print* ambayo ukisoma *Easy of Doing Business* tuko *poorly ranked,* sasa kwa sababu tuko *poorly ranked* tumejitambua sisi tukatengeneza *blue print,* ile *blue print* ndiyo inakwambia kasoro yako, usichelewe kutoa kibali, nenda kalipe kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale wanaposema tumepimwa vibaya hata kutolipa kodi wazungu wanatuona ni kasoro. Kwa hiyo, kama mnasema *Easy of Doing Business* tunarudi nyuma ni kwa sababu watu hawalipi kodi. Sasa huwezi kunihukumu Mwijage eti nimerudi nyuma kwenye *Easy of Doing Business* ni kwa sababu watu hawakulipa kodi. Hawa watu nitaendelea kuwabembeleza mimi kusudi walipe kodi niendelee kupata *ranking* nzuri. Kwa hiyo, mikakati iliyopo ni mizuri ila kama mtu anataka nije nimsomeshe, nimwelekeze taratibu, mikakati ile inatosha na niwahakikishie Tanzania sasa tuko kwenye viwanda, siyo kwamba tutajenga viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tutakwenda vizuri, Mpango uko vizuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Charles Mwijage, Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Nikupongeze sana kwa kazi kubwa mnayoifanya.

Waheshimiwa Wabunge, kwenye hili eneo nilipowasikia baadhi ya Wabunge, iko shida kidogo Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa maoni yangu lakini, kwamba baadhi ya watu wanaangalia *Industrial Policy* kama ni *Factory Policy* yaani viwanda vinachukuliwa kama ni

*factories* kitu ambacho siyo sawa. Mtu akijenga shule ya msingi ni *industry,* mtu akijenga ya sekondari, akijenga chuo kile ni kiwanda na ukiniuliza kinazalisha nini, jibu lake liko wazi kabisa. Mtu akijenga hoteli ni kiwanda, kina wafanyakazi, kinalipa kodi, ile ni *service industry, it is a hotel industry.* Mtu akijenga hospitali kubwa kile ni kiwanda. Kina mashine humo ndani za bei mbaya kuliko hicho kiwanda unachosema wewe kiwanda, kiwe ni cha karanga, kiwe ni cha korosho, mashine moja tu ni shughuli. *(Makofi)*

Wakati yule mzee aliyeanzisha wazo na kuendesha *Apollo Hospital in India,* wakati huo Serikali ya India ilikuwa imeanzisha sera kama yetu ya viwanda na Wizara ya Fedha ikawa na mfuko maalum wa viwanda. Kwa hiyo, wakapeleka maombi yao ya kujenga hospitali kwa kukopa kwenye mfuko wa viwanda. Serikali ya India ikamjibu huwezi kukopa kwenye mfuko wa viwanda kwa sababu hospitali siyo kiwanda. Wakafanya juhudi kubadilisha ile sheria yao, ikakubali kwamba hata hospitali ni kiwanda. Leo hii Apollo peke yake wana *chain of hospitals* zaidi ya 50, dunia nzima tunaenda kutibiwa huko na ni utalii mkubwa wa *medical tourism* na kadhalika. Kwa hiyo, hata sisi huu mtazamo wetu tuutazame kwa upana huo kuliko kuutazama kwa Kongwa kuna *factory* gani peke yake, tuangalie katika programu hiyo ya *industry.* Ahsante sana. *(Makofi)*

Tunaendelea na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Selemani Said Jafo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda sana kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa nguvu na uzima kwa kuweza kuhakikisha tunachangia mchango huu. Nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kunipa dhamana na kuniamini kuweza kuhudumu tena katika ofisi yake nikiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Rais kwamba sitamuangusha na nitazidi kumuomba Mwenyezi Mungu siku zote aweze kunipa nguvu na uzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kumshukuru kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango na dada yangu, Naibu Waziri, kwanza kwa kazi kubwa wanayofanya. Leo hii tunajadili Mpango, lakini mimi katika ofisi ninayoiongoza naomba kutoa shukrani za dhati sana kwa Wizara ya Fedha kwa kazi kubwa inayofanya na nishukuru kwa sababu imeendelea kuiwezesha ofisi yangu kwa kipindi chote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mjadala huu wa Mpango wetu, kikubwa zaidi ni kuangalia jinsi gani tutamwezesha mwananchi wa kawaida kuweza kukuza uchumi wake. Mpango wetu wa Taifa unaeleza dhahiri kabisa kuhusu chombo ambacho kiko katika ofisi yangu, tumekianzisha mwaka huu kiitwacho *TARURA.* Malengo yetu ni kwamba ikifika mwaka 2020 tuwe na mabadiliko makubwa sana katika suala zima la miundombinu ambayo hiyo itawawezesha wananchi kukuza uchumi wao kupitia malighafi au mazao yanayozalishwa katika maeneo yao. Nishukuru ofisi hii kwa jinsi ilivyojipanga kwa sababu katika mwaka huu wa fedha peke yake takribani shilingi bilioni 573 tutazielekeza katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa bila kuwa na mipango mizuri, mambo hayo hayawezi yakafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa kiwango kikubwa, nikijielekeza katika sekta ya elimu ambayo nimesikitika sana kwa sababu nimeona baadhi ya Wabunge wenzetu humu ndani wengine wakibeza jambo hili kubwa sana lililoanzishwa na Serikali ya Awamu ya Tano la kuwawezesha Watanzania masikini kwa kuwa na programu ya elimu ambayo inagharamiwa na Serikali, lakini wengine walikuwa wakisema maneno ya kebehi kabisa kama hakuna chochote kilichofanyika. Kwa kweli, kwa dhati kabisa naweza kusema hii si haki hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia katika *chain* yetu hii tunavyozungumza hivi sasa, tujipime sisi tuko humu ndani ya mamlaka Mwenyezi Mungu ametupa fursa tumeingia humu Bungeni, lakini tuwaangalie Watanzania hao wadogo-

wadogo ambao hali yao ni tete, ni taabani, hata ile gharama ya kulipia *certificate* ya *form four* wengine walikuwa wanashindwa. Leo hii programu ya elimu bure ambayo takribani shilingi bilioni 18.77 zimekuwa zinatoka, sasa hivi takribani shilingi bilioni 23 kila mwezi zinatoka, halafu kama Mbunge anasimama humu ndani anabeza kabisa kwamba hakuna lolote, nadhani tuna sababu ya kufanyiwa tathmini sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia kazi kubwa iliyofanyika. Ninyi mnafahamu kipindi kirefu tumesema shule zetu za Serikali hazifanyi vizuri, leo hii Wizara ya Fedha na Wizara ya Elimu kwa ujumla wetu katika suala zima la uwekezaji mkubwa tunaofanya katika sekta ya elimu, shule kongwe takribani 89 zote tunaziboresha ziweze kutoa mazingira ya ushindani. Mpaka sasa tunaenda takribani shule 43 ambazo hali yake ilikuwa ni hoi bin taabani. Shule hizi tunabadilisha miundombinu yake lengo kubwa iwe ni miundombinu wezeshi. Katika Mpango huu unaokuja tunaangalia ni jinsi gani tunaenda kukamilisha shule hizi nyingine tupate shule 89 ambazo zitakuwa na *level* ya kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Waheshimiwa Wabunge, wakati mwingine tupate fursa tutembelee mazingira yetu kuangalia tulipoanzia na wapi tunakokwenda. Nendeni Mpwapwa, Msalato, Mzumbe kwenye hizi shule ambazo Serikali imefanya *investiment* kubwa ya fedha za Serikali karibu shilingi bilioni moja kila shule. Mimi nimewaambia wazi kwamba lengo letu ni kuhakikisha elimu yetu inarudi katika mstari unaokubalika na haiwezi kurudi bila kuweka mipango na mipango yenyewe ndiyo hii inayojadiliwa humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme bahati nzuri Mheshimiwa Mwenyekiti wewe unafahamu shule yetu ya Mpwapwa zamani ilikuwa imechoka kabisa, leo hii ukifika Mpwapwa unashangaa hii shule ya aina gani! Nenda Msalato hapa watoto walikuwa wakifika shuleni wiki moja mtoto anatamani aende nyumbani. Tumeenda na Kamati

ya Bunge kutembelea tumekuta watoto 580 wamekataa kwenda likizo wote wame-*register* kwamba watabaki shuleni kwa sababu wanasema sasa hivi tumekaa shule kama tuko katika hoteli. Hii yote ni *investiment* kubwa inayofanywa na Serikali. Leo Mheshimiwa Mpango amekuja na Mpango wa jinsi ya kuboresha ili suala la elimu liende mbele zaidi. Naomba niseme wazi, tuwe wazalendo katika kuangalia jinsi gani tunafanya nchi yetu iende mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimesikia na bahati nzuri dada yangu Mheshimiwa Ummy Mwalimu, alizungumza katika suala zima la sekta ya afya, kumbukeni huko tulikotoka na sasa hivi tukoje. Ukiachia bajeti ya dawa Mheshimiwa Ummy amezungumza, lakini ajenda ya miundombinu, ninyi wenyewe mnafahamu huko tulikotoka leo hii kupitia fedha za *World Bank,* fedha za ndani na fedha kutoka Canada tunafanya *investment* kubwa katika nchi hii kwa mara ya kwanza haijawahi kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni tumepata karibu shilingi bilioni 10 fedha za ziada kutokana na mipango mizuri ya Serikali, mpaka *donors countries* wanaridhika na utendaji wa Serikali ya Tanzania. Hivi sasa tuna-*scale up* hiyo programu, tunaenda karibu vituo 216 kutoka 172, hii ni kazi kubwa inayofanyika, lakini kazi hii maana yake ni jinsi gani Serikali imejipanga kutekelza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba mimi nimpongeze Mheshimiwa Mpango, ndugu yangu usikate tamaa. Wakati mwingine safari yoyote ukiona unapigiwa kelele ujue kwamba safari hiyo inaenda vizuri, chapa kazi kaka na sisi tuko nyuma yako tunaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie Watanzania, Mpango wetu katika suala zima la miundombinu, bahati nzuri juzi-juzi tulikuwa kule Mwanza *World Bank* wanatusaidia suala zima la uboreshaji wa miji hii Tanzania. Ukienda Mbeya, Tanga, Arusha na miji yote mikuu tumefanya mabadiliko makubwa, lakini Manispaa zetu tunafanya uwekezaji mkubwa wa kujenga barabara za lami,

kuweka taa na kujenga madampo ya kisasa. Mpango huu unaokuja sasa hivi unaangalia ni jinsi gani tunaenda ku-*scale up* hiyo programu yetu ili kuhakikisha Miji, Halmashauri na maeneo mbalimbali yanaimarika katika miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo yote ni kutokana na sera nzuri ya Serikali inavyofanya *resource mobilization* na wadau wetu wanaridhika kwamba kazi zinakwenda. Juzi tukiwa Mwanza, *World Bank* imetoa *extension* ya mradi wetu wa *UGLSP,* badala ya kuishia mwaka 2018 sasa wame-*extend* mpaka 2020, hii ni faraja kubwa kwa Serikali ya Tanzania. *(Makofi)*

Kwa hiyo, jukumu letu kubwa ni lazima tuwe wazalendo tuone tulikotoka, tulipo na tunakokwenda. Kweli, unaweza ukatoa mawazo lakini siyo kukashifu kwamba hakuna jambo linalofanyika. Ingekuwa nchi nyingine kama Wabunge tungesema wapi kuna *gap* kidogo turekebishe twende mbele zaidi, lakini sio kukashifu kama hakuna kinachopatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri nimesikia Wabunge wengine walikuwa wakibeza hata suala zima la uchumi wa viwanda. Nimshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Mwijage amefanya kazi kubwa sana na mimi ni Wizara wezeshi ya kumwezesha kaka yangu Mheshimiwa Mwijage *instrument* yake ifanyike vizuri. Leo hii Mheshimiwa Mwijage na Rais anahangaika ili tuhakikishe tunajenga viwanda ili watoto waweze kupata ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana mimi nikiwa mwenye mamlaka na Serikali za Mitaa, juzi juzi wakati tunawaapisha Wakuu wa Mikoa niliwapa *target* nikasema Mheshimiwa Mwijage anahangaika na viwanda, lazima kama Wakuu wa Mikoa, leo katika bajeti yetu ya mwaka wa fedha 2017/2018, bajeti ya *own source* ni karibu shilingi bilioni 61.5. *A unit plants* ya kiwanda cha kawaida cha kubangua korosho, ukienda Newala, Masasi, ukienda *SIDO* wanakupatia kiwanda cha shilingi milioni 10. Kiwanda cha kukamua mafuta

ya alizeti hapa Singida, uliza zile mashine *SIDO* zinauzwa kiasi gani, *average* ni kati ya shilingi milioni mbili na nusu mpaka milioni sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *own source* yangu ambayo ipo katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa, shilingi bilioni 61, hata kama *unit plants* ya kiwanda kidogo ukiweka shilingi milioni 10 ni sawasawa na viwanda 6,100, ni *beyond expectation* ya viwanda 2,600 kwa mwaka. Hivi vitu ni *just calculation, is just about numbers.* Kwa hiyo, sisi kama Wabunge wetu lengo letu kubwa ni jinsi gani tuna-*play* ile *leadership position,* katika mamlaka zetu jinsi gani tutafanya sasa kuhakikisha tunaweka uwekezaji mkubwa tunaboresha viwanda vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Waziri wa Viwanda na Biashara, juzi wakati tunazindua *operation* ya viwanda 100, Naibu Waziri pale alitoa sera pana sana ya viwanda. Bahati nzuri mama mwenye Mifuko ya Uwezeshaji, dada yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama, ana mifuko 17, tumetoa fursa jinsi gani tutafanya kama Watanzania kwa ajenda ya viwanda ambayo ipo, tukiungana kwa pamoja tunatoka. Tatizo kubwa kuna watu wengine hawataki hili jambo lifanikiwe kwa sababu watasema kuwa Ilani ya Chama cha Mapinduzi imefanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba niwaambie tunaenda kushinda ushindi mkubwa kwa mafanikio makubwa. Kikubwa zaidi kaka yangu Mheshimiwa Mpango chukua yale maoni mazuri ya Wajumbe humu, tuyaweke vizuri tuone jinsi gani tutasonga mbele Mpango wetu uive vizuri. Nikuhakikishie, kwa Mpango huu na juhudi ya Serikali inavyokwenda na naomba niwahakikishie Wizara zote ambapo Wizara yangu ndiyo inakumbatia mambo mengine yote, Wizara wezeshi, tutashirikiana kwa kadri iwezekananavyo Mpango huu na mambo mengine yaende vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matamanio yangu makubwa wafike watu nchi jirani waje Tanzania kuja kujifunza kupitia kwetu. Kuna watu wengine wanaona kwamba eti

kufanya ufahari kwamba lazima uende kwenye kujifunza, hapana tufike muda Tanzania lazima tuache *legacy* nchi yetu. Leo hii tumepata mfano katika mradi wetu wa *DART* unaoendelea Dar es Salaam tumeshinda katika majiji duniani. Mwezi wa pili tunaenda New York, Marekani kuchukua tuzo maalum ni Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoenda katika suala zima la utengenezaji wa barabara za mwendo kasi awamu sita tumemaliza awamu moja lakini awamu hizo zote ndizo ziko ndani ya Mpango ambao leo hii ndiyo Mheshimiwa Mpango anau-*submit* hapa. Si muda mrefu sana tunaenda kuhakikisha tunatekeleza mradi wa barabara ya Kilwa - Mbagala - Gongo la Mboto. Lengo ni kulifanya Jiji letu la Dar es Salaam na maeneo mengine yawe rafiki kwa ajili ya suala zima la kujenga uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Tanzania tumepata ufahari mkubwa, takribani nchi sita na wengine mpaka leo wanazidi kuomba kupitia kwetu TAMISEMI waje Tanzania kujifunza mipango mizuri ya utekelezaji wa miradi yetu. Haya yote yanataka sisi Wabunge ambao ni *decision makers* ambao tunawawakilisha wananchi hapa tufanye maamuzi mazuri, tushirikiane na Serikali, pale penye upungufu tuboreshe vizuri zaidi nini tufanye ili tuifikishe nchi yetu mahali salama ambapo Watanzania watajivunia kwamba wamepata viongozi ambao wako humu na wamekuja kufanya maamuzi sahihi kwa ajili ya maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika haya yote naomba niseme wazi kwamba tunaenda vizuri. Kikubwa zaidi tutaboresha kwa michango mizuri ya Waheshimiwa Wabunge ndiyo maana ya Bunge lazima Wabunge watoe maoni, maoni yale yakikusanywa tunatengeneza Mpango mzuri lakini Mheshimiwa Mwenyekiti naomba nikuhakikishie kwamba Tanzania ikifika mwaka 2020 kuna watu mpaka wengine wataogopa kugombea humu ndani. Wasipoogopa kugombea basi lazima wata-*join* na watu ambao wana uhakika wa kushinda, *election is not a numbers*. Kama

tunaenda katika utaratibu huu mzuri naomba niwaambie hakuna mashaka lazima tutafika mahali muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya niliyoyazungumza, naomba niseme wazi kwamba kama Wabunge tuungane kwa pamoja, tujenge uzalendo wa nchi yetu, tuhakikishe jinsi gani tunafanya na tuweke maslahi ya wananchi mbele. Mungu ibariki Afrika, Mungu ibariki Tanzania, ubariki Mpango huu, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Aah, leo iko kazi hapa. Huyu ni Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Selemani Said Jafo. *(Makofi)*

Sasa twende kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuniamini mimi pamoja na Naibu wangu, Mheshimiwa Antony Mavunde lakini vilevile kwa kututeulia Mheshimiwa Stella Ikupa, jembe la nguvu kushirikiana na sisi katika kuhakikisha kwamba tunamsaidia Mheshimiwa Rais katika majukumu aliyotupatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuwa ni kielelezo cha utendaji bora wa Serikali ya Awamu ya Tano katika kusimamia majukumu makubwa ambayo hayataki mtu aambiwe aone kazi inayofanywa na Serikali hii. Pia namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu pia kwa kutulea vizuri sisi Mawaziri ambao tupo katika Ofisi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu nakutakia kila la kheri na hasa pale unaposhughulika na maswali ya Waziri Mkuu hapa Bungeni umeonyesha kabisa

kwamba wewe ni kiongozi wetu Mawaziri wote. Nakushukuru na nakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Dkt. Mpango. Dkt. Mpango naomba nikuthibitishie usikate tamaa. Wanaouponda Mpango wako wana ajenda binafsi. Dkt. Mpango chukua mawazo mazuri ya Wabunge waliotushauri sisi kwa pamoja kama Serikali, Mawaziri wote pamoja na wewe lakini yale mawazo ambayo kwa dhahiri unaona yanaponda Mpango wako kwa nia ovu achana nayo. Hasa Wabunge wa CCM wamechangia mawazo mazuri sana kwenye Mpango wa Serikali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji hapa wanasema Serikali yetu inakurupuka tu, inakuja hapa haijajipanga, haifanyi utafiti na inapanga mipango tu ambayo haieleweki. Naomba niwaambie hao wanaosema hivyo hawajasoma Mpango wala hawajaangalia mwongozo ulioletwa pamoja Mpango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kwenye sekta moja tu ya ajira, hivi unafikiaje mahali pa kujua hitaji la ajira katika nchi yetu ya Tanzania bila kufanya utafiti na kutengeneza mpango. Leo nitawaambia, Serikali yetu inafanya utafiti na ndio inakuja na mwongozo na inakuja mpango. Kwa mfano, sisi tumeshafanya utafiti wa kujua nguvu kazi iliyopo katika nchi yetu ya Tanzania ni idadi gani ya Watanzania na fedha za utafiti zimetolewa na Mheshimiwa Dkt. Mpango ili awe na mpango mzuri wa ajira katika nchi ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utafiti huo tumegundua Watanzania milioni 25 ndiyo nguvu kazi ya nchi yetu ya Tanzania na tunapozungumzia viwanda hawa milioni 25 ndiyo watakaokwenda kuchukua ajira kwenye viwanda hivyo ambavyo vitajengwa kwenye nchi yetu ya Tanzania. Nani anasema Serikali hii inakuja na mipango bila kufanya utafiti, tunafanya utafiti. Katika hiyo milioni 25 tumegundua asilimia 56 ni vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tumefanya utafiti mwingine, sasa kama tunataka kushughulikia tatizo la ajira, hivi ukosefu wa ajira kwa vijana katika nchi yetu ya Tanzania ukoje. Tumegundua kwamba ukosefu wa ajira kwa vijana kwenye nchi yetu ya Tanzania unazidi kupungua, ulikuwa asilimia 11.7 sasa hivi ni asilimia 10.3 na ni kwa sababu ya mipango mizuri ya Serikali na sekta nyingi za uzalishaji zinavyoongezeka na upungufu wa ajira unazidi kupungua. Hiyo ndiyo mipango inayogharamiwa na Waziri wa Fedha na Mipango katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumegundua sekta ya kilimo ndiyo inayoongeza katika kutoa ajira nyingi kwenye nchi yetu ya Tanzania na tumegundua asilimia 60.7 kilimo kinaongoza katika kutoa ajira. Sasa tunapofanya hivi ndipo tunapowaambia Watanzania baada ya utafiti huo tumemwagiza Mheshimiwa Mwijage aanzishe viwanda lakini viwanda vitakavyotumia malighafi ya kilimo inayolimwa ndani ya nchi ya Tanzania ili tutatue tatizo la ajira kwa vijana wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema Mheshimiwa Mwijage kwa kushirikiana na sekta hizo nyingine zote za umeme, maji na kadhalika atusaidie kutengeneza sera za viwanda unazozizungumza wewe Mheshimiwa Mwenyekiti iwe ni hospitali, gereji au kitu chochote, hivyo vyote ni viwanda vinatofautiana ukubwa na mazingira. Akifanya hivyo viwanda hivi vitazalisha bidhaa ambazo ndizo zinazohitajika zaidi katika soko la Watanzania hapa nchini na hivyo mwisho wa siku tutakuwa tumeweza kutatua tatizo la ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa tumeshafanya nini? Ili kuhakikisha vijana wa Tanzania wanaajiriwa, tumetengeneza programu maalum ya kukuza ujuzi katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitasema mafanikio yaliyopatikana, kwa kutumia Mpango huu wanaouponda wa Mheshimiwa Mpango tumefanya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, tumetambua na kurasimisha ujuzi wa vijana wa Tanzania mpaka sasa 3,900 wameshamaliza mafunzo ya ujuzi katika nchi yetu, 3,440 wanaendelea na mafunzo na vijana 13,432 tumeshawatambua wanasubiri tuwafundishe. Sasa nani anayesimama hapa na anasema eti huu mpango *fake* wakati unajibu mahitaji ya Watanzania. Hawa vijana ambao tumewapa ujuzi wengine wanatoka mpaka kwenye Majimbo ya wapinzani, watawashangaa Wabunge wao kama hawaungi mkono Mpango huu ambao umewapa ujuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao *graduates* wengi katika nchi yetu ya Tanzania lakini wamekosa mafunzo ya vitendo ya kukuza ujuzi wao. Tumeshatengeneza programu ya *internship* ya kuwasaidia vijana wa Kitanzania wakapate uzoefu na inalipiwa na Serikali kwa fedha za Mheshimiwa Mpango Waziri wa Fedha. Vijana 2,122 wameshaomba na Serikali inawapangia utaratibu wa kwenda kwenye mafunzo ya vitendo, hela yote inatolewa na Mpango na iko kwenye Mpango wetu. Nataka kuwaambia Watanzania kwamba tunafanya kazi na Serikali yetu inafanya kazi sana tena kwa kupitia Mpango ambao unaletwa na Mheshimiwa Mpango ndani ya Bunge la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ni machache tu ningeweza kusema mengi, lakini muda tu hauniruhusu. Napenda sana nizungumze jambo lingine hapa kuhusu mwenendo wa shughuli za Bunge. Wabunge hapa na hasa Wabunge wa Upinzani wamelidhalilisha sana Bunge lako eti Bunge hili halifanyi kazi yake sawa sawa, linaingiliwa na Serikali na halina tija yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme, Ibara ya 62 na nakupongeza sana wewe, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge, ndiyo iliyokuweka wewe na Bunge lako hili Tukufu na sio mtu. Hata hivyo, unapimaje tija ya Bunge, hupimi tija ya Bunge kwa kelele nyingi ndani ya Bunge, hupimi tija ya Bunge kwa kuleta fujo na kupambana na askari ndani ya Bunge, hapana. Hupimi tija ya Bunge eti kwa kufunga

midomo ndani ya Bunge kwa plasta na kuvaa nguo nyeusi, hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti,...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri nakuongezea muda, kwa hiyo, endelea vizuri, endelea Mheshimiwa Waziri. *(Makofi/ Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme unapima tija ya Bunge kwa namna Bunge linavyoongoza shughuli za Bunge na shughuli zinazojadiliwa ndani ya Bunge zina manufaa kwa kiasi gani kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nani Mbunge hapa atakayesimama ambaye hatashukuru na kupongeza kazi kubwa iliyofanywa na Wabunge wa Bunge la Kumi na Moja? Niwaombe Wabunge wenzangu na hasa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, bebeni ajenda ya mafanikio makubwa ya Bunge letu ndiyo itakayotuvusha mwaka 2020. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mifano, wewe mwenyewe umedhihirisha kwa mifano dhahiri kabisa kwamba Bunge hili limefanya kazi itakayokumbukwa na vizazi vyote katika nchi ya Tanzania. Umeunda Kamati hapa kwenye Bunge hilihili la Kumi na Moja ambayo imeweza kuisaidia Serikali kuweka mfumo wa kupata faida ya nchi kwenye madini ya vito katika nchi yetu ya Tanzania. Leo hii Mbunge anapata wapi *courage* na kusema Bunge hili halifai, halijawa na mvuto, halifanyi kazi zake linavyotakiwa! Mbunge gani huyo? Leo nitawaeleza Watanzania. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa

Mwenyekiti, Bunge lako hili limeweka historia ya kutunga sheria ya kuhifadhi maliasili za nchi yetu ya Tanzania, ni Bunge hili la Kumi na Moja chini ya uongozi wako Mheshimiwa Job Ndugai na siyo mtu mwingine yeyote. Leo hii Wabunge wanapata wapi *courage* ya kulibeza Bunge hili badala ya kujisifia na kwamba ni kazi nzuri tuliyoifanya ambayo pia inaendana mipango mizuri ya Serikali yetu ya Awamu ya Tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili limetunga sheria ya Msaada wa Sheria kwa Watanzania watakaohitaji kusaidiwa kwenye masuala ya sheria hata wanyonge kwenye maeneo ya vijijini, ni Bunge hili la Kumi na Moja. Nimesema Waheshimiwa Wabunge wenzangu tabia ya kulibeza Bunge letu na mwenendo mzima wa Bunge siyo tabia njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitamalizia la mwisho kwa ufupi sana, wakati tunachangia humu ndani na hasa Kiongozi wa Upinzani alipokuwa anachangia humu ndani alitaka kupotosha umma na kutaka kuyajadili madaraka ya Mheshimiwa Rais ya uteuzi wa viongozi eti kwamba anafanya uteuzi huo kwa upendeleo, hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 36(1), (2), (3) na (4) inatoa mamlaka kwa Rais kuanzisha na kufuta nafasi za madaraka ya namna mbalimbali katika utumishi ndani ya nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hiyo haisemi Rais atakapokuwa anafanya uteuzi eti aangalie ukanda, haisemi hivyo Ibara yetu kwenye Katiba. Ibara hiyo haisemi Rais anavyoandaa na kufanya uteuzi aangalie makabila mbalimbali kwenye nchi ya Tanzania, haisemi hivyo hiyo Ibara. Ibara hii haisemi Rais atakapokuwa anafanya uteuzi eti aangalie rangi ya

Mtanzania, haisemi hivyo. Unasimamaje ndani ya Bunge kuhoji uteuzi wa Mheshimiwa Rais wa nafasi ambazo amepewa Kikatiba, ni upotoshaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme unaona wateule wa Mheshimiwa Rais wanafanya kazi vizuri. Ameteuliwa hapa Mheshimiwa Mwanri kutoka Siha na ni Mkuu wa Mkoa wa Tabora, anafanya kazi nzuri sana. Ameteuliwa Mheshimiwa Mnyeti kuwa Mkuu wa Mkoa wa Manyara, anafanya kazi vizuri sana. Ameteuliwa hapa Mama yetu, Mama Anne Kilango jembe la nguvu kutoka Same anafanya kazi nzuri sana. Nina orodha ndefu nikiisema hapa ni ndefu kweli, lakini uteuzi huo unafuata madaraka ya kikatiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe sana Wabunge wenzangu tusiingilie madaraka ya Rais aliyopewa kwa mujibu wa katiba. Anayafanya kwa utashi wa hali ya juu na ukiangalia Ibara ya 34 inamtaka ateue watu watakaowajibika kumsaidia kubeba dhamana kwa niaba yake yeye mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniongezea muda na baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja iliyopo mbele yetu asilimia mia moja, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Huyo ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama. Kwa wasiofahamu huyu naye ni Seneta pia, ameingia hapa mwaka 2000 mpaka leo miaka mingapi na hajatoka yaani mfululizo. Wengine hapa wapita njia kipindi kimoja tu hamrudi hapa halafu mnazomeazomea Maseneta. Kwa hiyo, tujitahidi na sisi tukirudi mara mbili, mara tatu basi sasa ndiyo tunaruhusiwa kusemasema hovyo kidogo. *(Makofi/ Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tulipokaa siku ile ya mwanzo ya kuchangia Mpango niliwatia moyo sana nikawaambia Wabunge fungukeni, zungumzeni habari ya

Mpango wa Maendeleo. Sasa watoa hoja nao wanakuja hapa mbele na mimi niwaombe sasa fungukeni na ninyi zamu yenu kufunguka hapa msije mkasema ilikuwa upande mmoja, sasa nasawazisha goli. Kwa hiyo, karibu sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, nakupa nusu saa uchangie. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha kufika siku hii ya tano ya mjadala huu muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda na mimi nimshukuru Mheshimiwa Rais wetu kwa kuendelea kuniamini na kuniacha katika nafasi hii ya Naibu Waziri wa Fedha na Mipango ili niweze kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Waziri pamoja na yeye Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nikushukuru wewe kaka yangu Job Ndugai kwa kazi nzuri ambayo unaendelea kuifanya ya kuendesha Bunge letu Tukufu. Kwa kweli hongera sana kaka yangu, Mwenyezi Mungu azidi kukubariki ili tuweze kuifanya kazi hii tuliyoaminiwa na Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu kwa michango yao mizuri ambayo wametupatia sisi kama Wizara ya Fedha ili kuboresha Mapendekezo ya Mpango na tunapokuja mwezi wa Machi/Aprili na Mpango kamili tuweze kuja na Mpango ambao upo imara. Ninaamini wote kwa pamoja wametimiza wajibu wao Kikatiba wa nini walitakiwa kufanya na niwapongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wizara tumeyachukua yote, mimi na Mheshimiwa Waziri hatuwezi kujibu michango yote ya Wabunge zaidi ya 100 waliochangia kwa siku 5. Tutazungumzia machache ili tuweze kuendelea mbele kwenda kuandaa Mpango wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa uniruhusu nianze kuchangia hoja hii iliyowekwa Mezani na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, kaka yangu, Mheshimiwa Philip Isdor Mpango. Nianze kwa kukupongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kazi yako ni njema sana, kazi yako ni nzuri na imeonekana ndiyo maana Mheshimiwa Rais ameendelea kukuamini, hongera sana kaka yangu, simama hivyo hivyo. *(Makofi)*

Sisi watumishi tulio chini yako wewe ndani ya Wizara ya Fedha na Mipango tunajivunia kufanya kazi na wewe. Kwa wale ambao walikuwa hawajui uchumi sasa wanaufahamu uchumi ndani ya Wizara ya Fedha, nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kwanza ambayo napenda kuitolea ufafanuzi ni hoja ambayo ilisema Serikali ione umuhimu wa kufanya malipo ya wakandarasi ambao wametekeleza miradi mbalimbali ndani ya Taifa letu. Serikali yetu ya Awamu ya Tano inatambua sana umuhimu wa kazi zinazofanywa na wakandarasi, lakini pia umuhimu wa kuwalipa malipo yao kwa muda mwafaka ili waweze kuendelea kufanya kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2016/2017 Serikali imeweza kufanya malipo ya shilingi bilioni 3,358.89 kwa ajili ya wakandarasi, kati ya hizo, shilingi bilioni 1,321.47 zililipwa kama madeni ya wakandarasi waliojenga barabara zetu. Tunalipa lakini la muhimu kama ambavyo tumeendelea kusisitiza lazima uhakiki ufanywe ili tujiridhishe nini tunalipa kama Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya kiasi hicho nilichotaja, shilingi bilioni 1,161.32 kililipwa kwa ajili ya Mfuko wa Reli. Kama ambavyo Serikali yetu imedhamiria kuboresha miundombinu ndani ya Taifa letu na tumeanza kulipa, shilingi bilioni 204.90 zililipwa kwa ajili ya Mfuko wa Maji kwa wakandarasi wetu ambao wamefanya kazi ndani ya Wizara ya Maji. Mwenyekiti hili ulilisema na Waheshimiwa Wabunge walilisema kwa wingi kwamba Mheshimiwa Waziri haangalii ni maswali yapi

ambayo yakiulizwa wanasimama Waheshimiwa Wabunge wangapi. Sasa hili naomba kulidhihirishia Bunge lako Tukufu kwamba kama Serikali tumekuwa tukilipa na shilingi bilioni 204 zimelipwa kwa mwaka 2016/2017. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo pia limepigiwa kelele na kama Serikali tunaendelea kulipa na nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati, amesema vizuri na ametoa *order* nzuri sana na kwa mwaka 2016/2017 tulilipa shilingi bilioni 537.95 kwa ajili ya Mfuko wa Umeme Vijijini kuhakikisha vijiji vyetu vyote vinapatiwa umeme wa kutosha. Shilingi bilioni 133.24 tulilipa wakandarasi walioshughulika na miradi ya viwanja vya ndege. Tumesikia kelele nyingi zikipigwa kwa ajili ya shilingi bilioni 39 tu, hapana, tumelipa zaidi ya hizo kwa sababu zilikuwa ndani ya bajeti yetu ya mwaka husika. Kwa hiyo, nilidhihirishie Bunge lako Tukufu kwamba tumekuwa tukifanya malipo haya kwa ajili ya wakandarasi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika robo ya kwanza ya mwaka huu wa 2018/2019 tumelipa pia shilingi bilioni 562.29 kwa robo ya kwanza tu kwa wakandarasi wanaohusika na miradi mbalimbali ndani ya Serikali yetu. Kwa hiyo, nataka kusema kwamba dhamira ya Serikali yetu ni njema sana katika kuhakikisha kwamba watu wote wanaofanya kazi na Serikali yetu wanalipwa malipo yao yale wanayostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jambo hili, liliongelewa pia suala la Serikali kuchukua kodi ya majengo na ni kiasi gani ambacho tumeweza kukusanya kwa Mamlaka ya Mapato na hili aliliongelea vizuri sana kaka yangu Mheshimiwa Lubeleje.

Napenda kusema kwamba katika ukusanyaji wa Kodi ya Mapato niliambie Bunge lako Tukufu kwamba hatukunyang'anya Halmashauri zetu chanzo chake cha mapato. Nasema hivyo kwa sababu moja kubwa, dhamira ya Serikali ya kuchukua chanzo hiki ilikuwa ni kuongeza ufanisi wake ili sasa tuone ni jinsi gani tutaweza kuzirejesha pesa hizi katika Halmshauri zetu. Kwa mwaka 2016/2017 kwa

Halmashauri 30 tu tumeweza kukusanya shilingi bilioni 34.09 ukilinganisha na shilingi bilioni 28 ambazo zilikusanywa na Halmashauri husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema dhamira ilikuwa ni kuongeza ufanisi na ufanisi tumeuongeza zaidi ya asilimia 20 lakini ukiangalia Mamlaka ya Mapato Tanzania ilianza kukusanya kodi hii mwezi Oktoba. Kwa hiyo, nilidhihirishie Bunge lako Tukufu kwamba kwa mwaka huu ambao tumeanza tangu mwezi Julai, mapato yetu kutoka Kodi ya Majengo yatakuwa ni mazuri sana. Mifumo yetu imekamilika, tumeanza kufanya kazi kwa umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo lilikuwa linaulizwa kuhusu hili ni kwamba zimerejeshwa kiasi gani? Kama nilivyosema, dhamira kuu ilikuwa kuongeza ufanisi lakini kuhakikisha pesa hizi zinarejea kwa wananchi kwenda kufanya kazi. Baada ya kuzikusanya shilingi bilioni 34.09 pesa zote zilirejeshwa kulingana na bajeti za Halmashauri zetu kama Sheria yetu ya Fedha tuliyopitisha ilivyotuelekeza. Kwa hiyo, katika hili pia napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba hayo ndiyo mambo ambayo Serikali yetu ya Awamu ya Tano inayafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo napenda kuitolea ufafanuzi ilikuwa ni kuhusu Serikali kutounga mkono sekta binafsi kwa kuwa Mapendekezo ya Mpango hayaongelei sekta hiyo wala kuainisha miradi ambayo Serikali itashirikiana na sekta binafsi katika kuitekeleza. Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda amelielezea suala hili lakini pia niwaombe Waheshimiwa Wabunge ni muhimu wanapokuja kuchangia wawe wamepitia Mpango kuanzia *page* ya kwanza mpaka ya mwisho kuliko kuja kutuhumu bila kuwa na *facts* wakizifahamu. Hilo ni jambo la msingi sana. Nilichoki-*note,* watu wanasoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri halafu wanakuja kuchangia Bungeni, hapana, hotuba ya Mheshimiwa Waziri ni *summary* ya kitabu kizima cha Mapendekezo ya Mpango, kwa hiyo wakipitie kwa umakini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivi? Nasema hivi kwa sababu ndani ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2018/2019 tumeainisha sekta binafsi itahusika na miradi ipi na katika awamu ipi. Tumeonesha waziwazi kabisa ukurasa wa 26 hadi 28 wa Mapendekezo ya Mpango, tumeonesha sekta binafsi ilivyoshirikiana na Serikali kutekeleza bajeti yetu ya 2017/2018. Tukatoka hapo, ukurasa wa 58 hadi 59 tukaainisha sasa kwa haya Mapendekezo ya Mpango tunayokwenda nayo, Mpango wetu unaokuja tunataka sekta binafsi ishiriki katika miradi ipi. Kwa hiyo, ndiyo maana nimesema wawe wanapitia kitabu kile tulichokileta Bungeni kwa ajili ya kujadili hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu kwa kutambua umuhimu wa sekta binafsi katika kuleta maendeleo, hatukuishia tu kuainisha baadhi ya miradi lakini tumekwenda mbele na kuainisha na mikakati ni jinsi gani sekta binafsi na Serikali zitashirikiana ili tuweze kufanya kazi pamoja. Kwa hiyo, niombe sana hilo lifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika hoja hiyo liliongelewa pia suala zima la kwa nini Serikali inawekeza kwenye miradi mikubwa ya maendeleo ikatolewa mfano mradi wa reli yetu ya kati *(Standard Gauge Railway),* ukatolewa mfano pia mradi wa *Stiegler's Gorge* kwa ajili ya kuzalisha nishati ya umeme. Katika hili, naomba niseme jambo moja, ipo katika dunia nzima katika uchumi kwa nchi ambazo zimeendelea na sisi tunaendelea kuendelea, miradi hii ya miundombinu huwa ina sifa zake kuu tatu au nne ambazo ndizo zinazotoa mwelekeo kwamba ni nani atawekeza katika miradi ya miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Waheshimiwa Wabunge hasa waliosema katika jambo hili, waende wakasome *The Economics of Infrastructure Projects* ili waweze kuelewa. Katika *economics of infrastructure projects,* Maprofesa wabobezi wa uchumi wanasema miradi yote ya miundombinu ambayo ni ya kimkakati duniani kote huwa ina hatua zake tatu. Hatua ya kwanza, huwa ni *planning phase,*

hatua ya pili huwa ni *construction* na hatua ya tatu huwa ni *operation. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *planning phase* wabobezi wa uchumi wanasema miradi hii, naomba ku-*quote,* sifa moja katika *planning phase* ni nini kilichopo. Wanasema; *many strategic infrastructure projects generate cash flows after many years, and the initial phase of this project is subject to high risks.* Hii ina maana kwamba miradi yetu hii ya miundombinu ya kimkakati katika *initial phase* huwa ina *risk* kubwa sana na *risks* hizi hakuna kampuni yoyote ya binafsi ambayo iko tayari kuchukua *risk* hii katika *initial phase* ya miradi hii. Ndicho ambacho Serikali yetu imeona nini cha kufanya, lazima uoneshe nia wewe kama Serikali. Tunaihitaji miradi hii, tunahitaji *Standard Gauge Railway,* nani wa kuwekeza kwa sifa hizi, hayupo, *except the government itself.* Katika hili, tumeanza vizuri na imeanza Serikali yetu *at the initial phase, the planning phase, we planned,* sasa hivi tuko kwenye *construction phase,* tunafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sifa ya pili ya miradi hii ya kimkakati, hasa ya miundombinu, wachumi wabobezi wanasema; *even though the direct payoffs to an owner of an infrastructure project may cover its costs, the indirect externalities include beneficial for the economy as a whole.* Nini maana yake? Inamaanisha kwamba sawa gharama zake ni kubwa na *risks* zake ni kubwa lakini miradi hii ya miundombinu ina faida nje ya ile sekta husika. Sasa hivi tulikuwa tukilalamika mahindi yanayozalishwa Sumbawanga hayawezi kusafiri, Serikali ime-*invest* kwenye miundombinu ya barabara sasa mahindi yetu yanaweza kusafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kaka yangu Mheshimiwa Lubeleje, amelalamika asubuhi kwamba mahindi kule kwake Mpwapwa hayapo. Kwa *infrastructure* zilizowekezwa na Serikali ndugu zangu wa Mpwapwa watapata mahindi kwa bei nafuu. Ndiyo maana ya Serikali kuwekeza katika *infrastructure projects* kubwa kama *standard gauge* katika *initial phase* na *construction phase* lazima Serikali iweke mkono wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida hizi ni kubwa kama nilivyosema. Kwa hiyo, la msingi, tunapokwenda kwenye *operational phase* ambapo sasa tayari miradi hii itaanza ku-*generate revenue, cash flow* inaingia, ndipo utakapoyaona makampuni binafsi yanaingia ili sasa kuweka mabehewa mazuri kwa ajili ya kusafirisha wananchi wetu na bidhaa zao. Hakuna kampuni au mfanyabiashara ambaye anakuja kuwekeza akijua ataishi yeye, atakufa, ataishi mtoto wake atakufa halafu awekeze mtaji, hilo halipo. Ni Serikali tu kwa sababu ya faida pana ya mradi husika kwenye uchumi, tunataka kujenga nini, uchumi wa viwanda, bila *standard gauge* hatuna uchumi wa viwanda. Ndiyo maana Serikali yetu imefanya hicho ambacho tumekifanya. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge waendelee kutu-*support* ili tuweze kufanya kazi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala hilo, naungana kabisa asilimia 100 na kaka yangu, Mheshimiwa Bashe, aliposema *economics is not a rocket science, we agree a hundred percent. Economics is not a rocket science but economics is a social science, you need to understand the agency you are dealing with, the behavioral economics,* unafanya kazi na watu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wifi yangu anasema nirudie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema naungana na Mheshimiwa Bashe aliposema *economics is not a rocket science, that's quite right* lakini *economics is a social science,* unahitaji nini, unahitaji kuelewa *the social actors you are dealing with.* Unakaa chini unaendelea kusubiri *Stiegler's Gorge* tangu alivyouanzisha Mheshimiwa Baba wa Taifa letu, Mwalimu Nyerere mpaka leo hakuna mwekezaji aliyejitokeza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nasikia kelele huko, hebu tutulie tusikilize yaani huyu ni mwalimu wa *Mzumbe University. (Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, endelea.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Serikali imeanza kuwekeza *Stiegler's Gorge,* tutakapoanza *initial phase, the construction phase, operational phase,* tutapata wawekezaji na uchumi wetu utaruka, *that's where now the rocket science will come, not at the initial phase.* Niwaombe sana na mimi napenda kusema katika jambo hili sababu tunayo, nia tunayo, dhamira tunayo na uwezo tunao wa kuwekeza katika miradi mikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema dhamira tunayo, sababu tunayo na uwezo tunao kwa sababu bado hatujafika asilimia zaidi ya 40 ya kukopa kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania. Tukope, tuwekeze ili Watanzania wafikiwe na maendeleo kule walipo. Kama tungekuwa tunakopa na kulipana posho tungeweza kuogopa, lakini tunakopa tunawekeza kwenye *standard gauge* tusafirishe bidhaa zetu. Tunakopa tuwekeze kwenye *Stiegler's Gorge* tuzalishe umeme wa kutosha viwanda vya shemeji yangu, Mheshimiwa Mwijage, vifanye kazi, hatuna sababu ya kuogopa. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, niko na wewe nitafanya kazi pamoja na wewe katika jambo hili, naamini hilo limeeleweka. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Kabisa.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye hoja nyingine ambayo ilisemwa na Kambi Rasmi ya Upinzani, wakasema kwamba Serikali inafanya matumizi ya fedha ambazo hazikuidhinishwa na Bunge kinyume na utaratibu wa Sheria ya Fedha ya Matumizi ya Umma ya 2011. Napenda kwanza kukanusha hiki kilichosemwa na Watanzania wafahamu Serikali yao ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi iko makini katika kutekeleza sheria zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujafanya jambo hilo, hata siku moja. Kitu ambacho wanasahau ndugu zetu hawa

na kuja kudanganya wananchi, Mheshimiwa Waziri wa Fedha kapewa mamlaka ya kufanya uhamisho kutoka kifungu kimoja kwenda kwenye kifungu kingine, amepewa hiyo dhamana. Mheshimiwa Silinde, sikiliza nikufundishe uchumi. *(Makofi)*

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha amepewa hayo mamlaka, anayo mamlaka, labda kama mnataka kumpoka lakini anayo hayo mamlaka. *(Makofi)*

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Anafanya *reallocation* kutoka kifungu kimoja kwenda kifungu kingine ndani ya bajeti ya Serikali iliyopitishwa na Bunge lako.

**MWENYEKITI:** Mbona hasimami huyo anayetaka kutoa taarifa basi? Mheshimiwa Naibu Waziri, hebu kidogo tumpe nafasi, kuna binti mmoja wa Kisukuma hapa anataka kukupa taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ningependa kumpa taarifa mzungumzaji Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba aliyetuambia pesa za *standard gauge* hatujakopa ni Mheshimiwa Rais mwenyewe. Kwa hiyo, siyo Upinzani ndiyo tumepotosha, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania John Pombe Magufuli alihutubia akasema pesa za *standard gauge* hatujakopa ni pesa za ndani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa sitaruhusu tena taarifa kwa sababu taarifa iliyotolewa yaani haieleweki kabisa. Naibu Waziri anachoeleza ni kwamba kuhamisha mafungu Mheshimiwa

Waziri wa Fedha ana mamlaka hayo anasimama Mheshimiwa Mbunge anaongea mengine. Mheshimiwa Naibu hebu endelea *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naomba nim-*quote* kaka yangu Jafo alivyosema wanaanza kupata kiwewe kwamba hawezi kutukamata wapi tunakwenda. Hii *speed* siyo ya kawaida hakuna wa kutusogelea ndugu zangu. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kutoa darasa, Sheria ya Bajeti kifungu cha 48 kinampa mamlaka hiyo Waziri wa Fedha, kikisomwa pamoja na Kanuni zake, Kanuni ya 26(1) inamwelekeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha nini cha kufanya. Kanuni ya 26(2) inamwelekeza aweze kufanya *reallocation* kwa kiwango gani, ndicho ambacho amekuwa akifanya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Serikali yetu haijawahi kutumia fedha hizi nje ya bajeti iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hiyo inaunganishwa na naona ndicho wanachokitafuta lakini wanashindwa kufika, kwamba Serikali sasa ilete Bungeni *adjustment* ya bajeti kwa sababu wamesahau mamlaka haya ya Waziri. Naomba niseme jambo moja, nini maana ya bajeti ya nyongeza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhamisha kifungu hiki, kupeleka kifungu hiki siyo bajeti ya nyongeza ndugu zangu. Maana ya bajeti ya nyongeza ni kwamba Serikali ndani ya mwaka husika imekusanya mapato ya ziada ambayo hayakupitishwa na Bunge lako Tukufu na sasa inataka kuyafanyia matumizi. Hiyo ndiyo bajeti ya nyongeza ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha kama anataka kutumia hayo mapato ya ziada tutalazimika kuja kwenye Bunge lako lakini kwa *reallocation of funds between votes* tunatakiwa tu tunapokuja hapa katika *mid year review* tu-*report* nini tumefanya, wala siyo kuleta bajeti ya ziada, hatuna bajeti ya ziada ndugu zangu. Tuko ndani ya bajeti iliyopitishwa na Bunge, ndani ya matumizi husika, tunatumia katika miradi yetu ya kipaumbele ndani ya Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri tukawa na uelewa wa pamoja wa Sheria tunazopitisha sisi wenyewe halafu tunaposimama tuseme kwa Watanzania nini Serikali inafanya kwa niaba yao. Hilo ni jambo la msingi sana nilitaka kuliomba Bunge lako Tukufu tukubaliane na hiki ambacho kiko ndani ya Sheria iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu na siyo kuja hapa na kuwadanganya Watanzania kwamba Mheshimiwa Rais anatoa *order,* hawezi kutoa *order* bila kujua hiyo pesa ipo na ilipitishwa na Bunge lako Tukufu. Hilo ni jambo la msingi sana katika utekelezaji wa shughuli za Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo iliongelewa kwa uchungu na kwa sauti kali ilikuwa ni kwamba Mipango ya Maendeleo ya mwaka 2016/2017, 2017/2018 na 2018/2019 yote inafanana. Nianze kwa kukuomba kwamba tuwe tunapitia vitabu hivi ili tuweze kujua lakini tusisahau msingi wa mipango hii mitatu na sasa tumebakisha mipango mingine miwili ni Mpango wa Pili wa Maendeleo wa miaka mitano. Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano ndiyo unatupa sisi *base* ya miradi ipi itekelezwe, kwa kiwango kipi na imeelekezwa kabisa. Ukichukua Mpango ule wa Miaka Mitano mimi nausoma vizuri sana na baada ya kusikia hili nilienda nikarudia kusoma mara mbili, mara tatu kuna nini? Nikagundua miradi mingi iliyopo kwenye Mpango wa wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano inatekelezwa kwa kipindi cha kuanzia miaka mitatu mpaka mitano, nini maana yake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016/2017 tulileta mradi ule ukiwa katika *initial phase*, mwaka 2017/2018 tumeleta mradi ule katika hatua zake za mwanzo za utekelezaji, mwaka 2018/2019 tunaleta sasa wapi tumefika baada ya kufika nusu ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano, miradi ni ile ile. Tofauti ya miradi hii inayoripotiwa ni utekelezaji wake hatua moja kwenda hatua nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukianza ku-*crash* miradi ambayo ipo kwenye Mipango yetu ya Maendeleo ya mwaka mmoja tunawambia nini Watanzania? Hatukuwa

makini kupitisha Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano kwa sababu hakuna sehemu Waziri wangu wa Fedha anaweza kwenda kuchukua mradi ambao hauko kwenye Mpango wa Pili wa Maendeleo.

Kwa hiyo, lazima tulifahamu hilo, twende tusome *content of the document not what the Minister has presented in the Parliament,* tutapata *content* na tutaelewa sasa wapi tupo na miaka mwili inayobaki nini tutafanya, je, tutaweza kutimiza kile tulichodhamiria? Hicho ndicho kilichopo, ukisoma tu bila kubeba jicho la *planning* ndani ya mipango hii utagundua hatuna utofauti ndani ya mipango yetu lakini ukiweka jicho la *planning (the planners)* utaona nini kilichopo ndani ya mipango yetu na wapi tunaelekea sasa katika kuhakikisha Tanzania ya viwanda tunaifikia kabla ya mwaka 2020. Dhamira yetu ni moja tu, kabla ya mwaka 2025 tunahitaji kuona Watanzania wenye kipato cha kati, kabla ya mwaka 2020 tunadhamiria kuona Watanzania wa Tanzania ya viwanda, hilo ndiyo jambo la msingi na ndiyo kazi tunayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya niseme jambo lingine ndogo ambalo liliongelewa katika ile ile hoja ya kupotosha Watanzania na nini Serikali yetu inafanya. Ilikuwa ni hoja kwamba Serikali imeendelea kudharau mamlaka ya Bunge lako Tukufu kwa kuacha kuleta sheria ya kusimamia mipango tunayopitisha ndani ya Bunge lako. Naomba kusema Serikali yetu ni sikivu sana hasa Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa John Pombe Magufuli. Ni Serikali sikivu sana na hatuna ujanja huo wa kulidharau Bunge lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema kwamba, katika hili turejee kwenye Sheria ya Bajeti Na.11 ya mwaka 2015, kwa nini ilitungwa Sheria ya Bajeti, ni kusimamia mipango na bajeti tunayopitisha humu ndani. Tunahitaji sheria nyingine ipi na kufanya lipi? Pia kwa kila mwaka tuna *Appropriation Act* kwa ajili ya kusimamia matumizi ya Mpango tunaojadili leo, sasa tunahitaji sheria nyingine kufanya nini? Hatuhitaji sheria nyingine. Tunayo Sheria ya Bajeti na

tunayo *Appropriation Act* ya kila siku. Sheria ya Bajeti inatuwezesha kubainisha kisheria majukumu na mipaka ya kiutendaji ya wahusika wakuu katika mchakato mzima wa kibajeti na kimpango. Sheria ya Bajeti inaweka uwiano kati ya mipango yetu, mapato yetu na matumizi yetu, tunahitaji sheria nyingine ya kufanya nini? Sheria ya Bajeti pia inaweza kutueleza na sisi tukatambua mzunguko wa kisheria wa kibajeti nini kilichopo, tungekaa tukaisoma vizuri wala tusingefika sehemu ya kuja na *personal issues* za kumtuhumu Waziri wa Fedha hata siku moja, turejee tu kwenye sheria tunazozipitisha sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naomba nikushukuru kwa kupata nafasi hii. Kama nilivyosema mwanzo yako mengi tutayafanyia kazi kwa umakini yote kwa pamoja na tutakuja na Mpango unaoakisi mapendekezo mazuri yaliyotolewa na Wabunge hasa wa Chama changu, Chama cha Mapinduzi walioongea mengi kwa ajili ya kuboresha Mpango wetu. Yale machache ya upande wa pili tutayachukua yale mazuri, yale mabaya naomba tuyaache humu humu tunapotoka tutoke na ushirikiano wetu na udugu wetu ili tuweze kutekeleza azma ya Serikali yetu na Hapa Kazi Tu itafanikiwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Wapo rafiki zangu upande huu walikuwa wanamwangalia kma vile hawamfahamu Dkt. Ashatu Kijaji kwamba alaa, kumbe ana uwezo wa kujieleza kiasi hicho. Kanikumbusha miaka ya 70 palikuwa na bendi moja sijui ilikuwa inaitwa Mangelepa, sijui bendi gani, palikuwa na wimbo unaitwa sindano ya moto, leo Mheshimiwa amekuwa sindano ya moto. Ahsante sana Mheshimiwa kwa *presentation* hiyo, hiyo shule ambaye hakuelewa basi tena jamani, ahsante sana. Katibu. *(Kicheko)*

**NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:** Kamati ya Mpango sasa imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge sasa linarejea.

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae.

Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa nimuite mtoa hoja ambaye ni Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango karibu utoe hitimisho lako, una dakika 45. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naomba na mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniruhusu kusimama leo tena hapa jioni kuhitimisha hoja ambayo niliiwasilisha tarehe 7 Novemba, 2017 kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2018/2019.

Aidha, napenda kutoa shukrani za dhati kabisa kwako wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kusimamia vyema mjadala wa hoja. Vilevile niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote 124 waliochangia katika mjadala huu ambapo Wabunge 103 wamechangia kwa kuzungumza ikijumuisha Mawaziri na Naibu Mawaziri ambao kwa kweli mmenipa raha, lakini pia wapo Waheshimiwa Wabunge 12 ambao wamechangia kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyobainisha katika hoja yangu kuwa lengo lilikuwa ni kuomba maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge wakiwa ndiyo sauti za mawazo na matakwa ya wananchi wetu kuhusu maendeleo ya nchi yao, lakini pia mgawanyo wa rasilimali fedha ili yazingatiwe katika hatua ambayo itafuata baada ya kikao hiki cha Bunge ambayo itakuwa ni kazi ya kuandaa Rasimu ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na kiwango na ukomo wa bajeti kwa mwaka ujao wa fedha ambavyo kwa mujibu wa Kanuni za Bunge hili zitawasilishwa kwa Wabunge tarehe 11 Machi, 2018 na kufanyiwa uchambuzi na Kamati ya Bajeti kuwezesha ukamilishwaji wa Mpango na Bajeti ambavyo vitawasilishwa wakati wa Bunge la bajeti. Kwa niaba ya Serikali nakiri kuwa lengo hilo limefanikiwa kwa kiwango kikubwa na narudia kusema ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mhesimiwa Spika, niruhusu kipekee nitambue mchango wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini. Kamati ilitupatia ushauri wa msingi ambao niliuelezea kwa kifupi wakati natoa hoja, lakini vilevile tulipokea mchango uliotolewa na Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Momba kwa niaba ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Wizara ya Fedha na Mipango. Aidha, nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara mbalimbali waliotoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja zilizotolewa zinazogusa sekta zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani kwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji kwa kunisaidia kusikiliza kwa makini maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge kwa siku zote tano na kutolea ufafanuzi kwa umahiri hoja zilizotolewa hapa ndani muda mfupi uliopita. Nitumie pia fursa hii kuwashukuru kwa dhati watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu, Bwana Dotto Mgosha James kwa kuchambua na kutafuta takwimu na taarifa ambazo zilihitajika kwa ajili ya kutolea ufafanuzi wa hoja mbalimbali. *(Makofi)*

Katika majadiliano ya hoja niliyowasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Serikali imepokea maoni mengi sana. Naomba nitaje baadhi tu kwa kifupi maoni ambayo yalitolewa na Wabunge wengi na hii ni kuthibitisha tu kwamba Serikali inasikia. Maoni hayo ni kama ifuatavyo:-

(i) Mmetushauri kwamba tuweke msukumo pekee kwenye sekta ya kilimo. *(Makofi)*

(ii) Mmetushauri tujumuishe mkakati mahsusi wa kumaliza kilio kikubwa cha upatikanaji wa huduma za maji nchini kote. *(Makofi)*

(iii) Mmetuambia kwamba fursa ya uwepo wa rasilimali kubwa ya gesi asilia nchini ni lazima sasa itumike vizuri zaidi. *(Makofi)*

(iv) Mmetuelekeza tutekeleze kwa dhati utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi yaani *PPP. (Makofi)*

(v) Mmetuelekeza na kutushauri tuongeze kasi ya kutekeleza miradi ya miundombinu ya kiuchumi na kijamii ikiwa ni pamoja na ile ya Umeme Vijijini *REA III* lakini pia barabara muhimu za kuchochea uchumi katika mikoa mbalimbali. *(Makofi)*

(vi) Mmetushauri tuongeze kasi ya kulipa madeni yaliyohakikiwa.

(vii) Mmetushauri tuhakikishe kuwa Deni la Taifa linaendelea kubakia kuwa himilivu na kuanza kupunguza kasi ya kuongezeka kwa Deni la Taifa.

(viii) Mmetushauri tukabiliane na tatizo la ukosefu wa ajira nchini. *(Makofi)*

(ix) Mmetushauri kuwekeza na kutumia kikamilifu rasilimali za bahari na maziwa *(the blue economy).*

(x) Mmetushauri kubainisha mkakati wa kuongeza idadi ya watalii na mchango wa sekta ya utalii katika uchumi. *(Makofi)*

(xi) Mmetushauri kuhusu kuimarisha uhifadhi wa ardhi, kupima na kupanga matumizi yake.

(xii) Mmetushauri kuchukua hatua za kupunguza kasi ya ongezeko la idadi ya watu.

Mheshimiwa Spika, hayo ni baadhi tu, ni masuala kumi na mbili muhimu ambayo tumesikia ushauri wenu lakini yako mengi sana tutayafanyia kazi. Kwa niaba ya Serikali naahidi kuwa wakati wa kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2018/2019 tutazingatia ipasavyo maoni na ushauri uliotolewa na Bunge lako Tukufu lilipokaa kama Kamati ya Mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kazi yangu, kazi ya Naibu Waziri na wataalam wetu wa Wizara kwa siku hizi tano ilikuwa ni kupokea maoni na ushauri ambao tunakwenda kutafakari na kufanyia kazi, nitapenda nitoe ufafanuzi kwa baadhi tu ya hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge mlizitoa. Kwa kweli hoja ni nyingi kama nilivyosema na kwa muda ambao nimepewa si rahisi kujibu zote na naomba niwahakikishie kwamba tutawasilisha majibu na maelezo ya hoja zote kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijafanya hivyo, naomba nisisitize tena mambo matatu kwa sababu yanajirudiarudia kila mwaka, ni vizuri tukawa tunaelewana kwa faida ya Taifa letu.

Kwanza, nilichowasilisha Bungeni ile tarehe 7 Novemba, 2017 siyo Mpango ni mapendekezo ya mambo ya msingi na vipaumbele vinavyotakiwa kuzingatiwa katika kuandaa Mpango wenyewe na bajeti ya Serikali kwa mwaka ujao wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, Mapendekezo ya Mpango na Mwongozo wa kuandaa bajeti yalipitia katika hatua zote ambazo ni kupata maoni ya wadau wa ndani na nje ya Serikali, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, Kikao cha Makatibu Wakuu *(IMTC)* na kupata ridhaa ya Baraza la Mawaziri kabla ya kujadiliwa na Kamati ya Bajeti na hatimaye Bunge. Hivyo, mapendekezo ya Mpango siyo mpango wa Dkt. Mpango bali ni Mapendekezo ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la tatu, Mapendekezo haya ni mwendelezo wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano 2016/2017 - 2020/2021 kwa mwaka wa tatu. Kwa hiyo, wale wanaodai ni *copy and paste* kutoka Mpango wa mwaka jana ni vema wakazingatia hili.

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya maelezo haya, naomba nijielekeze kujibu baadhi ya hoja na nitaomba nianze na ile hoja ambayo naiona ni muhimu sana kwamba Serikali iache kupeleka fedha kugharamia miradi mikubwa

ya kielelezo kama *Standard Gauge Railway*, ununuzi wa ndege mpya, uzalishaji wa umeme *Stigler's Gorge,* miradi ambayo inaweza kutekelezwa kibiashara na sekta binafsi. Ilisemwa hapa kuwa utaratibu huo unapunguza fedha kwa ajili ya kugharamia huduma za msingi kwa jamii kama maji na afya na utapelekea kuongezeka kwa mzigo wa Deni la Taifa.

Mheshimiwa Spika, hoja hii ni vema tukaitafakari vizuri. Serikali inathamini sana mchango wa sekta binafsi na tunafahamu kuwa huko ndiko kwenye pesa na mitaji mikubwa na hasa ukizingatia *size* ndogo ya uchumi wa Taifa letu kwa hivi sasa lakini pia mahitaji makubwa ya wananchi wetu. Hata hivyo, ni muhimu mawazo hayo yapimwe kiuhalisia na bila kusahau historia na uzoefu wa nchi nyingine. Wote mtakumbuka kwa tulikuwa na *RITES of India* hapa, hivi naomba niulize walijenga kilomita ngapi za reli? Tumesahau kwamba treni karibu zote zilisimama, mizigo ikawa inasafirishwa kwa malori mpaka Serikali ilipofanya uamuzi wa kuondokana na *RITES of India.* Hivi sasa kweli hata tukikaa hapa si nalisikia linapita hapo, hatuoni treni za abiria na mizigo zinatimua vumbi. Tena nasikia zinaimba kadogosa kadogosa kadogosa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri wangu ameeleza vizuri wazo la kuzalisha umeme eneo la *Stigler's Gorge* lilikuwepo kwenye makaratasi kwa miaka mingi. Hivi sekta binafsi si ilikuwepo na ilikuwa inasikia kilio cha kutokuwepo kwa umeme wa uhakika na wa gharama nafuu hapa nchini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na Kampuni hapa ya *City Water* kwenye sekta ya maji mbona kilio cha maji Dar es Salaam hakijaisha? Yaliyotokea *ATCL* na *TTCL* vivyo hivyo, mbona tunasahau haraka hivi? Hata hivyo, sasa tumefanya mabadiliko na tumeanza kufaidi huduma za Bombardier kuja Dodoma, Songea, Kigoma na kwingineko. Aidha, hivi sasa nasubiri gawio mwaka huu shilingi bilioni moja kutoka *TTCL* kwa mara ya kwanza. Najiuliza hivi umeme huu utakaozalishwa *Stigler's Gorge* hautaimarisha upatikanaji wa

huduma za afya, elimu na maji kwa gharama nafuu zaidi? Nawasihi ndugu zangu hebu tutafakari vizuri, tusisahau historia, *we have the experience. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwasihi sana Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla kuwa ni kweli kabisa sekta binafsi ndiyo injini ya uchumi lakini zipo changamoto kiuhalisia. Mzee Kikwete alituambia akili za kuambiwa lazima tuchanganye na za kwetu kabla hatujafika hatua ya kuwa na sekta binafsi yenye nguvu. Kweli natamani sana wawekezaji wa ndani na nje watatupunguzia huu mzigo. Waheshimiwa Wabunge nilieleza mwaka 2016/2017 kujenga *Standard Gauge Railway* kwa bajeti ya Serikali ni mzigo mkubwa mno, lakini sekta binafsi tuliyonayo bado inahitaji kulelewa ili iweze kubebea jukumu hili na sekta binafsi kutoka nje hawaji wakati tunapowahitaji na hata wakija wana masharti ambayo baadhi ni magumu kwelikweli na mengine hayana maslahi kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miezi michache ilyopita Mheshimiwa Waziri Mkuu aliita makampuni ili watujengee mtambo wa kuchenjua makinikia na alikuwepo mfanyabiashara mmoja kutoka Dubai, kitu cha kwanza alichoanza nacho anasema pesa ninayo lakini sharti la kwanza *sovereign guarantee*, aah, magumu haya jamani.

Kwa hiyo, katika mazingira haya hivi kweli tutakaa miaka na miaka *indefinitely* tukisubiri wawekezaji washuke ndiyo tuijenge upya reli ya kati ambayo ina zaidi ya miaka 100. Uamuzi wa Serikali ni kwamba tuanze kujenga kwa vipande yaani *lots* wakati tunaendelea na jitihada za kuwashawishi wawekezaji na taasisi za fedha ambazo zinaweza kutukopesha kwa masharti ambayo ni ahueni, hatuja-*rule out private sector,* hapana, lakini hatuwezi kuendelea kusubiri miaka mingine 50 ndiyo tupige hatua ya kujenga reli yetu ya kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba ninong'one na Bunge lako Tukufu, Mheshimiwa Rais Magufuli aliposikia huu mjadala alinipigia simu na aliniambia hivi, Waziri mwambie ndugu

yako Mheshimiwa Nape na Mheshimiwa Bashe kuwa nawataka sana hao wawekezaji kwenye ujenzi wa *Standard Gauge Railway*, wawalete hata kesho, niko tayari kuwapa reli ya Kaliua - Mpanda au Isaka - Mwanza au reli ya Mtwara - Mchuchuma - Liganga wajenge. Hayo ni maneno ya Mheshimiwa Rais. Natumaini Waheshimia husika *will raise up to this challenge from His Excellence the President*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikwa na hoja ya Deni la Taifa linakua kwa kasi kubwa wakati uchumi unakua kwa kasi ndogo na kwamba hali hii itafanya ulipaji wa Deni la Taifa kuwa mgumu sana. Deni la Taifa liliongezeka kutoka dola za Marekani milioni 22,320.76 mwaka 2016 na kufikia dola za Marekani milioni 26,115.2 mwezi Juni, 2017 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 17% na deni hilo ni sawa asilimia 31.2 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na ukomo wa uhimilivu wa asilimia 56. Uhimilivu wa Deni la Taifa hupimwa kwa kuzingatia uwezo wa nchi kulipa deni husika katika muda mfupi, wa kati na muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kulinganisha Deni la Tanzania na nchi nyingine za Afrika Mashariki ni kama ifuatavyo; Uganda ni asilimia 35.4, Rwanda asilimia 36.6, Burundi asilimia 43.4 na Kenya asilimia 50.4. Hali hii ya nchi za Afrika Mashariki bado ni nzuri ikilinganishwa na baadhi ya nchi nyingine kama Zambia ambayo ni asilimia 57.2, United Arab Emirates asilimia 60.3, Marekani asilimia 73.8, Morocco asilimia 77, Uingereza asilimia 92.2, Misri asilimia 92.6, Msumbiji asilimia 100.3, Italia asilimia 132.5 na Ugiriki asilimia 181.6. Kwa takwimu hizi sisi bado tuna nafasi kubwa ya kuendelea kukopa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, tutaendelea kukopa kwa sababu kuu moja tu, ni kukuza uwezo wetu wa baadaye wa kumudu uendeshaji wa nchi yetu na kulinda uhuru na heshima ya nchi yetu. Napenda nisisitize hakuna dhambi ya nchi kukopa ili mradi nchi husika itumie fedha hizo za mkopo kukuza uwezo wa uchumi, kuzalisha na kurejesha hiyo mikopo, ni lazima iwe *prudential borrowing.* Kama Mheshimiwa Rais alivyosema alipokuwa ziarani kule Kagera

kwa kweli tutaendelea kukopa mpaka kieleweke ili mradi Deni la Taifa tuhakikishe linaendelea kuwa himilivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda nitoe angalizo kuwa ukokotoaji wa uhimilivu wa Deni la Taifa japokuwa siyo *rocket science* unahitaji utaalam. Kujua hesabu za kikwetu haitoshi kufahamu namna ya kukokotoa deni *in present value terms* maana masharti ya mikopo na muda wa kuiva wa madeni haya yanatofautiana sana. Siyo suala la kujumlisha mkopo fulani *in nominal terms* na kuamua kuwa deni halitakuwa himilivu. Namuomba Mheshimiwa Kishoa na wengine kama wanataka *lecture* bure kuhusu *debt sustainability analysis* waje pale Hazina tuko tayari kuwafundisha bila malipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuliombwa hapa tutoe ufafanuzi kwa nini takwimu za Deni la Taifa katika vitabu vya Mpango vya mwaka 2016/2017, 2017/2018 na 2018/2019 zinatofautiana. Katika kitabu cha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa 2017/2018 takwimu zinaonyesha kuwa Deni la Taifa hadi kufikia Juni, 2016 ni dola za Marekani milioni 18,614.93 wakati katika Mwongozo wa Maandalizi wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2018/2019 takwimu zinaonyesha Deni la Taifa hadi Juni, 2016 ni dola za Marekani milioni 22,320.76. Deni la Taifa linajumuisha deni la Serikali la ndani na nje pamoja na deni la nje kwa sekta binafsi. Deni la Serikali la nje linajumuisha mikopo kutoka nchi wahisani, mashirika ya fedha ya Kimataifa pamoja na mabenki ya kibiashara ya kimataifa. Wakati deni la ndani la Serikali linajumuisha dhamana za Serikali za muda mfupi na hati fungani za Serikali pamoja na madeni mengineyo.

Mheshimiwa Spika, takwimu zilizopo katika kitabu cha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2017/ 2018 za dola za Marekani 18,614.93 ni deni la Serikali na siyo Deni la Taifa kwa kuwa halikujumuisha deni la sekta binafsi. Aidha, mtoa hoja angepitia kifungu hicho hadi mwisho angeona Deni la Taifa hadi Juni, 2016 ni dola za Marekani milioni 23,093.3 na kiasi hiki ni tofauti na kile kilichoripotiwa katika Mwongozo wa Maandalizi na Mpango wa Bajeti wa

mwaka 2018/2019 ambapo Deni la Taifa kwa kipindi hicho ni dola za Marekani 22,320.76. Tofauti hii ya dola za Marekani 772 inatokana na kubadilika kwa deni la sekta binafsi na kupungua kwa deni la Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kufuatia kukamilika kwa uhakiki wa madeni hayo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya taarifa za benki za biashara nchini zinaonyesha kuporomoka kwa kiasi kikubwa kwa mikopo binafsi, mikopo ya biashara na mikopo kwa sekta za uzalishaji. Hali ya kupungua kwa kasi ya ukuaji wa mikopo imetokea katika nchi kadhaa ikiwemo Tanzania kwa kipindi cha takribani mwaka mmoja na nusu sasa. Katika miezi kumi na mbili iliyoishia Septemba, 2017 wastani wa ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi nchini Kenya ilikuwa asilimia 3.8, Tanzania asilimia 5.0, Uganda asilimia 5.2 na Rwanda asilimia 10.3. Katika nchi zote hizi ukuaji wa mikopo katika kipindi kilichotajwa ulikuwa chini ya nusu ya ukuaji katika kipindi kama hicho kilichotangulia.

Mheshimiwa Spika, kushuka huku kuna sababu mbalimbali ikiwemo kupungua kwa utashi duniani yaani kwa kiingereza *general decline and global demand* ambako kunajidhihirisha kwa bei za bidhaa duniani kuwa chini kiujumla. Hii inaathiri mapato ya sekta binafsi yaani *cash flows* na kufanya zisichikue mikopo kwa kasi ile ile.

Pili, mabenki kuongeza tahadhari katika shughuli zao kutokana na hali ya wasiwasi duniani yaani *global uncertainty.* Matokeo ya kuongezeka kwa hali ya wasiwasi ni pamoja na benki kadhaa kupoteza mahusiano na benki za kimataifa yaani *correspondent banks* katika kile kinachoitwa *de-risking.*

Tatu, ni kupungua kwa fedha za bajeti za Serikali kutoka nje ya nchi ambako kumepunguza ukwasi uliokuwa ukisababishwa na matumizi ya fedha hizo na hivyo kuathiri utashi ndani ya nchi kiujumla yaani *domestic demand*. Mfano, fedha za bajeti kutoka nje zilizotumika zilipungua kutoka shilingi bilioni 2,711 mwaka 2013/2014 hadi kufikia shilingi bilioni 1,774 mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua za kuongeza ukwasi na zinafahamika, Benki Kuu imeshusha riba yake yaani *discount rate* kutoka asilimia 16 Machi, 2017 hadi asilimia 9 Agosti, 2017. Pia kupunguza kiwango cha kisheria cha sehemu ya amana kinachotakiwa kuwekwa Benki Kuu na benki za biashara *(Statutory Minimum Reserve Requirement - SMRR)* kutoa asilimia 10 mpaka 8 Aprili, 2017. Benki Kuu pia imeendelea kutoa mikopo ya muda mfupi kwa benki za biashara pamoja na kununua fedha za kigeni kutoka kwenye soko la jumla la mabenki.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hatua hizi, hali ya ukwasi katika mabenki imekuwa ni ya kuridhisha kuanzia kipindi cha nusu ya pili ya mwaka 2016/2017 na hii inadhihirika katika kupungua kwa riba ya mabenki yaani *interbank market rate* kutoka wastani wa asilimia 13.49 Disemba, 2016 hadi asilimia 3.72 Oktoba, 2017. Kupungua huku kwa riba katika soko la mabenki kumedhihirika pia katika soko la dhamana za Serikali ambako wastani wa riba umeshuka kutoka asilimia 15.12 - Disemba, 2016 hadi asilimia 9.45 - Oktoba, 2017. Matumaini ya Serikali ni kuwa hatimaye matokeo ya hatua hizi yatajionesha katika ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwa nini Benki Kuu imeacha kutoa takwimu za uuzaji na uingizaji wa bidhaa nje *(import and export data).* Ripoti za uchumi za Benki Kuu za kila mwezi *(Monthly Economic Reviews)* za Julai, Agosti na Septemba ni kweli hazikuonesha takwimu za biashara ya bidhaa nje ya nchi *(trade statistics)* na sababu yake ni changamoto za *data (harmonization)* ambazo zilijitokeza katika kukamilisha takwimu hizo baada ya kuanza kutekelezwa mpango wa Himaya Moja ya Forodha ya Afrika Mashariki yaani *EAC-Single Customs Territory.* Changamoto hizi zinashughulikiwa na mara zitakapokuwa zimetatuliwa takwimu hizi zitaendelea kutolewa, Serikali haina sababu ya kuficha chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, palikuwa na hoja kwamba mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa

hayakugusa Zanzibar. Niseme tu kwamba tumesikia hoja hii na tutajadiliana na wenzetu upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar namna bora ya kulishughulikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Mheshimiwa aliyetoa hoja anafahamu kuwa ilivyo sasa Zanzibar ina Tume ya Mipango Huru lakini pia ina Ofisi ya Takwimu ambavyo sio vya Muungano. Aidha, Zanzibar ina Dira yake ya Maendeleo 2020 na ina Mkakati wa Kupunguza Umaskini (MKUZA) na Maandalizi ya Mipango ya Maendeleo ya Zanzibar inaongozwa na nyaraka hizo na taasisi nilizozitaja, *of course,* pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtakumbuka kuwa yalikuwepo mawazo katika Katiba Pendekezwa kwamba Taifa lifikirie kuwa na Tume moja tu ya Taifa ya Mipango lakini mchakato haukufika mwisho. Aidha, kuna vikao vya pamoja vya Kiwizara na Kitaifa vinavyoratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais kujadili changamoto mbalimbali za Muungano wetu zikiwemo zile zinazohusu masuala ya kodi ambazo Waheshimiwa Wabunge walizisema, biashara na kadhalika na Wizara ninayoiongoza tunashiriki kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, kikao kijacho kimepangwa kufanywa tarehe 17 na 18 Novemba, 2017 Dar es Salaam na nishauri tu kwamba baadhi ya mambo na hoja ambazo zilisemwa ziwasilishwe kwenye jukwaa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Waziri wa Fedha wa Serikali ya Muungano kwenda Zanzibar napenda sana na nimekwishakwenda mara mbili na napanga kwenda huko mara baada ya kikao hiki cha Bunge. Namuomba sana Mheshimiwa Saada aniandalie urojo tu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, aidha, tumefanya vikao na wenzetu wa Zanzibar si chini ya mara nne ndani ya miaka miwili hii ikiwa ni pamoja kikao ambacho aliongoza Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, nyumbani kwake Oysterbay mwezi uliopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, palikuwa na hoja muhimu ambayo mimi nasema ni ya msingi sana kwamba sekta ya kilimo, ufugaji na uvuvi vipewe kipaumbele katika Mpango na Bajeti kwa kuwa mchango wake ni muhimu sana katika kuwezesha harakati za kufikia uchumi wa viwanda na kupunguza umaskini. Serikali inakubaliana kabisa na hoja hii na tutaizingatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba toka mwanzo na pia katika wasilisho langu wakati natoa hoja, sekta ya kilimo, ufugaji na uvuvi ni moja ya maeneo ya kipaumbele katika kukuza uchumi na ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda. Kwa msingi huo, eneo hili litafafanuliwa katika Mpango wa mwaka ujao na litahusisha maeneo yote ambayo Waheshimiwa Wabunge waliyasisitiza ikiwemo upatikanaji wa uhakika wa chakula, malighafi za viwanda, miundombinu ya umwagiliaji, upatikanaji wa pembejeo, utafiti wa kilimo na mbegu bora na pia kuboresha huduma za ugani, usindikaji wa mazao, miundombinu, hifadhi ya masoko pia kuboresha miundombinu ya uzalishaji wa mifugo na kuongeza bidhaa za mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, hoja ni nyingi na ningependa tungepata muda zaidi wa kuzifafanua lakini tutazifafanua kwa maandishi.

Kabla ya kuhitimisha hoja yangu, napenda kwa mara nyingine tena kutoa shukrani za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2018/2019 na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2018/2019. Nasema hivi kwa dhati ya moyo wangu. Aidha, naomba sana Mbunge yeyote asisite kunikosoa katika utendaji wangu wa kazi kwa maslahi ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudia tena, naomba sana Mbunge yeyote asisite kunikosoa katika utendaji wangu wa kazi kwa maslahi ya Taifa letu. Hata hivyo, nawasihi mnikosoe au kunipongeza kwa haki na hofu ya Mungu. Namuomba sana Mungu, napata kigugumizi kusema maneno haya lakini

nitasema tu. Namuomba Mungu anipe moyo wa kuyapokea yale yote yaliyonenwa juu yangu pasipo kweli, japokuwa kama binadamu yalinisononesha, napenda nilihakikishie Bunge hili na Watanzania kwa ujumla kwamba mwenendo wa mjadala wa hoja hii umeniimarisha zaidi kuendelea kutimiza wajibu wangu kwa Taifa na naamini Mungu atanisaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea kumsihi Mungu awabariki Waheshimiwa Wabunge wote bila kuwabagua wale walionivika joho la ujeuri yaani *arrogance* na uziwi. Hii imenifanya nikumbuke kuwa watoza ushuru walichukiwa hata kabla ya wakati wa Yesu na hivyo mimi nikiwa msimamizi wa watoza kodi inabidi tu niyapokee. Bahati nzuri ni kuwa wananchi wenu ambao fedha hizi za kodi tunazielekeza kwenye maendeleo yao ikiwemo kununua dawa na vifaatiba, elimu msingi bure, umeme vijijini, kuboresha huduma za maji na kadhalika wamewasikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hapo awali, Serikali itazingatia maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge katika kukamilisha maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2018/2019. Kuthibitisha hili, napenda nirudie kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Mpango ujao utazingatia kwa kadri inavyowezekana ushauri uliotolewa na Kamati ya Bajeti na Bunge zima likikaa kama Kamati ya Mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siwezi kuhitimisha hoja hii bila kumshukuru kwa dhati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake wa karne, ni chuma kweli kweli. Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete aliposema hayo hakukosea kabisa. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kunitia moyo niendelee kutekeleza majukumu yangu ya msingi ya kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Serikali na kudhibiti matumizi ya fedha za umma bila uoga kwa faida ya wananchi wanyonge hata pale wachache wanaponidhihaki binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kadhalika namshukuru sana Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Mbunge wa Ruangwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nimejifunza katika miaka hii miwili kwamba kweli Waziri Mkuu wetu ni kocha na kapteni mahiri wa utendaji Serikalini kama alivyo kwenye medani za mpira wa miguu. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuendelea kunipa *confidence* katika utumishi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wito wangu ni kwa Waheshimiwa Wabunge wote kuendelea kuunga mkono Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi wa Rais wetu Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli katika dhamira yake ya kujenga Tanzania mpya ambapo wananchi wote watanufaika na rasilimali za Taifa ili kuwaondoa kwenye lindi la umaskini. Pamoja na mambo mengine, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, kuendelea kuwahimiza wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo ili kuleta mabadiliko chanya katika maisha yao na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, rai yangu kwa Watanzania wote ni kuwa tuungane kwa pamoja na kufanya kazi kwa bidii, uaminifu na uadilifu mkubwa kwa nchi yetu. Mageuzi makubwa anayoyaongoza Rais wetu ni magumu tena magumu sana lakini ndiyo njia sahihi kuelekea Tanzania mpya. Kwa mfano, uamuzi wa kuhakikisha fedha za Serikali zinarejeshwa Serikalini ili zitumike kuwahudumia wananchi haukupokelewa vizuri na wahusika lakini ukweli utasimama. Haiwezekani, labda wasubiri nitakapoondolewa kwenye Uwaziri huu, akaunti za Serikali, mfano fedha za polisi zikaendelea kushikiliwa na kampuni binafsi inaitwa *Max Malipo* kwa ambao hawaijui. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawaahidi kuwa yale yote yaliyo chini ya mamlaka niliyopewa nitayasimamia bila kutetereka ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa tunapiga hatua kubwa zaidi katika ukusanyaji wa kodi na mapato yote ya Serikali, kudhibiti mianya ya uvujaji wa mapato na kupanua wigo wa kodi sambamba na kusimamia matumizi ya fedha za umma kama Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 inavyotuongoza.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Nimewaona Waheshimiwa, ahsanteni sana. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kuhitimisha. *(Makofi)*

Ahsante sana kwa wasilisho hilo muhimu sana, najua muda ulikuwa hautoshi, Waheshimiwa Wabunge wangependa kusikia kila mmoja kile ambacho kimezungumzwa lakini Mheshimiwa Waziri wa Fedha ametuahidi kuwa baadhi ya mambo haya yatakuwa katika majibu ya kimaandishi. Nitawaomba majibu hayo yakipatikana basi tusome jamani maana nina hakika wapo wanaoyaacha kwenye *pigeon holes* pale halafu tukirudi tena mwakani yanazungumzwa yale yale kumbe baadhi yake yanakuwa yamejibiwa vizuri.

Kwa hatua hii niwashukuru sana, mwenyewe Waziri wa Fedha, Naibu Waziri wa Fedha na timu yako yote ambayo ilikuja Dodoma, najua mmekesha. Niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wote, Naibu Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge ambao tumechangia vizuri sana katika Mpango huu. Katika kumbukumbu zangu za hivi karibuni, Mpango huu ndiyo umechangiwa kwa hamasa ya kipekee kabisa. *(Makofi)*

Niwahakikishieni kazi yetu haikuwa bure. Wizara imesikia, wataalam wa Wizara wamesikia na mlichokizungumza ndiyo *reflection* ya Watanzania wanachokizungumza. Kwa hiyo, wameyachukua kama walivyotuahidi hapa, wataenda kuyazingatia na ndiyo maana kwa siku ya leo sitawahoji kuhusiana na jambo hili kwa sababu tulichokuwa tukikifanya hapa ni kujadili Mapendekezo ya Mpango, kwa hiyo, hatuwezi kuhojiana kuhusu Mapendekezo. Tutakaporudi wakati ule wa bajeti, utakuja sasa ule Mpango ambao unatokana na mapendekezo yetu haya na bajeti yenyewe itafuatia *immediately* baada ya pale. Ndiyo maana nikasema

nawashukuru sana wote, Waheshimiwa Wabunge tuzidi kushirikiana na mpaka sasa tunaenda vizuri. Nawapongeza sana wote na kipekee nawapongeza sana Mawaziri, mmevumilia kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jamani, hata upande huu tuwapigieni makofi, wamekaa siku nne hapa mnapiga madongo, Mpango bado yupo. Yapo mazingira hata wa upande wa pili unampigia makofi kwamba kwa hili umevumilia. *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Tumepiga.

**SPIKA:** Mmepiga. Si mnaona Mheshimiwa Waziri amepungua kilo mbili hapa. Mheshimiwa Waziri, haya yote yalikuwa kwa nia njema na ni kwa ajili ya kujenga nchi yetu. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa jinsi hiyo, kwa sababu ya muda wetu hatuwezi kuongeza shughuli yoyote. Niseme sasa kwamba naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.36 Jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 14 Novemba, 2017, Saa Tatu Asubuhi)*